

# Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Arobaini na Nne - Tarehe 11 Agosti, 2011

(Mkutano Ulianaza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

*Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha, 2011/2012.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA -MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:** Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka 2010/2011, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI - MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Taarifa ya Msemadi Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge leo ni Alhamisi, kufuatana na Kanuni tunaendelea kwenye kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu, siyo hotuba bali ni maswali. Swali la kwanza litaulizwa na Mheshimiwa Martha Moses Mlata.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mheshimiwa Waziri Mkuu sote tunakumbuka kwamba mwaka 2008 dunia ilikumbwa na m dororo wa uchumi. Lakini Mataifa makubwa kama Marekani na nchi zingine ikiwemo Tanzania iliweza kusaidia mabenki pamoja na watu waliokuwa na hisa kukabiliana na m dororo huo. Lakini sasa hivi Tanzania yetu pia imekumbwa na tatizo kubwa la mgao wa umeme. Wafanyabiashara wengi ambao wamekopa mitaji yao kwenye mabenki hususan wajasiriamali kama akinamama wanaofanya biashara ndogo ndogo, wanakabiliwa na tatizo hilo kwa sababu wao mikopo yao ni ya muda mfupi na wanatakiwa warudishe kwa mfano waliokopa *Pride* wanatakiwa kila baada ya wiki arudishe...

**NAIBU SPIKA:** Sasa swali Mheshimiwa.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Hivyo Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali inatoa tamko gani kwa watu kama hawa kuwasaidia ili kuweza kukabiliana na m dororo huu? Ahsante.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Martha Mlata kwa swali lake zuri na labda niseme tu kwamba, pengine si rahisi sana kwa Serikali kuweza kutoa kauli ya uhakika juu ya jambo hili. Wajasiriamali wako wengi na ukizua jambo hilo nadhani itakuwa ni kazi kubwa kweli kuweza kujua unamsaidia nani na kwa namna gani. Lakini

kama ni hili suala la pengine riba kwa kipindi hiki ambacho wameona kama kuna m dororo sana sana ninachoweza kusema hapa ni kwamba, pengine naweza nikasaidiwa tu na vyombo vinavyohusika *Pride* kwa maana hiyo na vyombo vingine kuwaomba kama inawezekana basi kwa kutambua hili angalau waweze kusukuma mbele ule muda wa marejesho ya mikopo hiyo. Nafikiri tunaweza tukazungumza na mabenki vile vile tukawasihi wakaliona hilo pengine hiyo ndiyo ingekuwa njia bora na rahisi ya kuweza kuwa-*cover* walio wengi. (*Makofii*)

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa Jiji la Arusha liliamilisha uchaguzi wake wa Meya na Kamati zake zote kwa mujibu na Kanuni za Serikali za Mitaa. Lakini hivi karibuni tumesikia tamko la CHADEMA kwamba wewe Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mbobe mmeingia kwenye muafaka wa kutaka uchaguzi wa Meya pamoja na Kamati zote za pale Arusha urudiwe. Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu tunaomba utufafanulie kwenye Bunge hili Tukufu. Hizi taarifa zinazosemwa na CHADEMA je, ni za kweli au si za kweli? Ahsante. (*Makofii*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Mwanjelwa kwa jambo hili kwa sababu na mimi wakati niko Morogoro niliona tu sehemu ya taarifa hiyo kwenye runinga ya *TBC*, ikigusia suala kama hilo unalolizungumza. Lakini kuna baadhi ya magazeti vile vile amba walikuja kuniona wakiulizia nini hasa kilichotokea. Nikajaribu kulifafanua. Kwa hiyo, nadhani hii ni fursa nzuri pengine Watanzania wajue kilichotokea ni nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kulisema hili jambo siku za nyuma kwamba kwa kadri tunavyolija jambo hili uchaguzi ule ulifanyika, ulikamilika na ndiyo maana nilisema kama kulikuwa na mtu anaona hakutendewa haki njia rahisi na kiutaratibu wa kisheria ilikuwa ni kukata rufaa au kwenda kudai Mahakamani kile ambacho hukuridhika nacho. Bado naona ni msimamo wangu na ni msimamo wa Serikali kwa sababu ndiyo utaratibu ulivyo. (*Makofii*)

Sasa juzi Jumamosi tarehe 6 baada ya kuwa nimeombwa na Mheshimiwa Mwenyekiti wa CHADEMA Mheshimiwa Mbobe, siku ya Ijumaa jioni kwamba angependa kuniona, nilikubali. Akaniomba kwamba naweza kuja na Katibu Mkuu, ndugu yangu Dokta Slaa, nikamwambia njoo naye tu. Kwa hiyo, Jumamosi asubuhi saa tatu walikuja kuniona. Kwa hiyo, walipofika katika mazungumzo yao likajitokeza suala la hali isiyoridhisha ya kisiasa katika Manispaa ya Arusha. Kwa maana kwamba vyama ambavyo ni vikubwa pale ni Chama cha Mapinduzi pamoja na CHADEMA. Wao waliona kama hali iliyopo pale hajatulia, bado haitoi fursa kubwa kwa chombo hili kuweza kushughulika na mambo ya kiutendaji na kwa maslahi ya wananchi wa Manispaa.

Kwa hiyo, nikawaambia kwamba *okay fine* kama ni suala linalogusa masuala ya siasa, hilo haliko ndani ya uwezo wangu mimi. Hapa tunachoweza kukubaliana tumwombe Msajili wa Vyama ambaye ye ye ndiye amepewa jukumu la kuratibu na kuona matatizo yanayotokana na mambo kama haya ya mitafaruku kati ya vyama, pengine ye ye huyo angeweza kutusaidia vizuri zaidi. Nikamwahidi kwamba nitamtafuta huyu bwana, nitamweleza kwamba wamekuja kuniona, rai yenu ndiyo hiyo. Yeye sasa ataandika barua kwenda Chama cha Mapinduzi, kwa Katibu Mkuu Taifa na CHADEMA, halafu vyombo hivi viwili vitatengeneza utaratibu wa namna ya kushughulikia au kukutanisha vyama hivi viwili. Mimi ndiye niliyesema kwamba naamini katika hatua zote itabidi kuwepo na timu ya pamoja pande zote *at technical level* ili waweze kubaini ni *agenda* gani mnataka kuzipeleka kwenye mazungumzo hayo.

Agenda hizo zitapanda kwenda ngazi ya Taifa ili viongozi wa ngazi ya Taifa wakisharidhia utaratibu wa kuzungumza hicho walichokiita hali ya kuonekana kwamba kuna mtafaruku, hapajatulia kisiasa, liweze kuzungumzwa. Sasa, juzi nilipomsikia Mheshimiwa Mbobe kwenye TV, nikaona mmh mbona kwanza amekwenda mbali. Hili jambo liliikuwa ndiyo kwanza limeanza safari kwenda kwa Msajili. Lakini huku limetoka kana kwamba tumeshakaa, tumekubaliana, itakuwepo na timu ya Kitaifa. Haikuwa sahihi hata kidogo na nasema *it is very unfortunate* kwa jambo hili. (*Makofii*)

Kwa hiyo namshukuru sana Mheshimiwa Mwanjelwa kwamba umelileta jambo hili kwa sababu ukweli wa mambo yalivyokuwa ndiyo hivyo. Sasa kama hilo ndiyo tafsiri yake nadhani *it is wrong*. (*Makofii*)

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa sasa tumejua kwamba kauli zilizotolewa na CHADEMA zinazosemwa za Arusha siyo za kweli. Je, wewe kama Mheshimiwa Waziri Mkuu, una ushauri gani kwa Madiwani wote wa Arusha, wananchi wa Arusha na wale Madiwani ambao inadaiwa wamefukuzwa. Tunaomba tamko. (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Labda niseme nilichokuwa nimemshauri Mheshimiwa Mbewe, kwa sababu aliniambia kwamba anakwenda kukutana na Kamati Kuu na kwamba *agenda* kubwa ni hii ya Madiwani sita. Nilichomshauri, nikamwambia ndugu yangu mnakwenda kuamua nini, hilo ni juu ya CHADEMA. Lakini nikasema panahitajika busara kubwa. Maana yangu ilikuwa ni kwamba wakati mnaomba pengine kuwepo na mazungumzo kati ya vyama hivi viwili kwa jambo ambalo linagusa hali ya kislasa pale, fikra zangu ilikuwa ni kwamba, busara nzuri ilikuwa ni kuendelea na hali iliyokuwepo hadi hapo mtakapokuwa mmefikia hatua fulani. Sasa niliposikia kwamba wamefukuzwa, aah basi nikasema hata mazungumzo yenewe sijui yatakuwaje sasa. *Okay!* (*Makofi*)

Sasa nadhani tumejiingiza kwenye mtego mkubwa tu. Lakini kwa hili aliloliuliza, ninachowea kushauri tu ni kwamba tufuate sheria. Kwa hiyo, Madiwani hawa kama wanaona hawakutendewa haki katika mchakato wa kufukuzwa kwao, njia rahisi waende Mahakamani. Wahoji uhalali, Mahakama ndiyo itakayowasaidia kuona kwamba walichofanyiwa ni sawa ama si sawa. Huo ndiyo ushauri wangu kwa Madiwani wote. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Madiwani wahoji kuchaguliwa kwa nguvu ya umma na kufukuzwa kwa nguvu ya Kamati ya Siasa. Swali linalofuata la Mheshimiwa Stephen Hilary Ngonyani.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu juzi Serikali ilitoa taarifa hapa Bungeni kwamba baada ya mchakato wa mafuta mpaka kufika juzi bei ya mafuta ingekuwa imeshuka na mafuta yamekuwa yako sawa na ulitoa tamko hapa kwamba yejote ambaye atakuwa amekiuka misingi basi Serikali itamchukulia hatua. Sasa nataka kujua kwamba wale ambao wamekiuka misingi ya mafuta umewachukulia hatua gani?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumshukuru Mheshimiwa Ngonyani, Mjumbe wa Kamati mwenzangu, Kamati ile tunayojuwa wote hapa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ni kubwa na wote limetugusa sana. Lakini nataka niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba baada ya Bodi ya *EWURA* kutoa amri ambayo ilipaswa kuzingatiwa na vyombo vyote vinavyohusika katika sekta hiyo kutolewa na kuweka mwisho wa muda ule. Kwa taarifa nilizo nazo mimi mpaka jana saa 10 makampuni karibu yote hasa yale manne, yalikwishaanza kusambaza mafuta kutoka kwenye maghala. (*Makofi*)

Lakini tutaendelea kulifuatilia kwa maana ya kuona sasa mafuta yanayotoka kama yanauzwa kwenye vituo vyote bila kubagua. Maana katika mazingira haya kunaweza kukawa na hatari, unatoa lakini unapeleka kwenye vituo vyako tu, unawanyima fursa wengine kuweza kupata huduma kama hiyo. Lakini kwa ujumla mpaka jana saa 10 makampuni yalikuwa yameshaanza kutoa mafuta. Kwa taarifa niliyopewa jana lita karibu milioni tano zilishatoka na magari kama 250 hivi yalishachukua mafuta yale tayari kwa ajili ya usambazaji na yale ni mafuta ambayo tayari yalikuwa yamewekwa ile alama kwa ajili ya kuhakikisha kwamba hayachakachuliwi.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu kila siku Serikali ikitaka kutoa maamuzi yake inasubiri *EWURA*, *EWURA*, *EWURA*. Kwa nini Serikali isiamue yenewe kutoa maamuzi mpaka isubiri *EWURA*. Tutasubiri *EWURA* mpaka lini?

**WAZIRI MKUU:** Swali la Mheshimiwa Ngonyani ni zuri. Lakini ni gumu kidogo kulitekeleza kwa namna anavyolitazama. Kwa sababu nchi hii tunaongozwa hasa na utawala wa Sheria na ndiyo maana uwepo wa Bunge hili ni muhimu sana. Sasa Waheshimiwa Wabunge kama mnavyojuwa 2001 ndipo mlitunga Sheria inayohusu *EWURA* na imekuja kutekelezwa *effectively*

mwaka 2005/2006. Sasa chini ya Sheria hiyo ndiko mamlaka yote yanayohusu suala zima la udhibiti wa zao hili la mafuta llimowekwa. Sasa zamani kabla ya Sheria hiyo kuanzishwa mwaka 2001 ni kweli mambo kama haya yalikuwa yanafanya na Serikali moja kwa moja na kama mtakumbuka hata bei ya umeme, ilikuwa labda ipate kibali cha Rais, ndiyo tunapandisha *tariffs*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika hali ya soko huru ambapo kunakuwa na makampuni na tumeruhusu sekta binafsi kuingia katika uzalishaji wa umeme na maeneo mengine. Duniani kote ni lazima vyombo huru, vyombo vinavyoonekana vinafanya kazi kwa mujibu wa Sheria bila kuingiliwa na mifumo mingine vinalazimika kuanzishwa. Ndiyo msingi wa kuanzishwa *EWURA*. Kwa hiyo, *EWURA* ndiyo yenyeye mamlaka kamilii sasa hivi na inasimamia hata vyombo vyetu vya Serikali. Kwa hiyo, *TANESCO* akitaka kufanya lolote ni lazima na yeye apeleke suala lake kwenye mamlaka ya udhibiti. Ndiyo maana unaona katika mchakato mzima sisi kama Serikali muda wote tumekuwa tunaishi *EWURA* iharakishe, itoe maamuzi. Bodii ikae kwa sababu hakuna namna sisi tunavyoweza kuingia pale na kunyakua madaraka yale ambayo ni ya kimamlaka. Nadhani ni vizuri tukaendelea hivyo, kwa sababu vinginevyo tutajikuta tena tunaleta mambo ambayo si halali sana. Ndiyo maana hata hii kampuni ambayo tumesema itaanzishwa ni lazima na wao vile vile waende *EWURA* kwa ajili ya kupata leseni, kwa ajili ya kufanya nini, hata bei zitapangwa kulingana na maelekezo ya *EWURA*. Nataka kuwasihii Wabunge, Sheria mkizitunga wajibu wetu sisi ni kuzitekeleza. (*Makofii*)

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa, Serikali ilitangaza bei ya mahindi kwamba, itakuwa sh. 350/= kwa kilo. Lakini tumesikia wakulima hawa wadogo kwa sasa wanatakiwa kulipa tozo la asilimia mbili wanapouza mahindi yao. Lakini vile vile wanalamizika wajisajili wawe na *TIN Number*, kama wafanyabiashara wa muda mrefu. Je, Serikali haioni kwamba, inawaonea sana hawa wakulima wadogo? Mheshimiwa Waziri Mkuu, una kauli gani juu ya jambo hili? (*Makofii*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Nkumba, kwa swali hili, lakini naomba niharakishe kusema tu kwamba, juzi nilimsikia Waziri wa Kilimo akilielezea hili jambo. Lakini pengine niseme tu kwa kulisitsitza ili niweze kwa kweli kuwafanya Watanzania wawze kutulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mkulima mdogo anapokwenda kuuza gunia lake moja, magunia yake mawili au matatu, nasema hata kama chombo hicho kilikuwa na hamu ya kutafuta hiyo asilimia mbili unaona kabisa kwanza ni kupoteza muda wa chombo chenyewe! Inaonekana kama hakina kazi, kwenda kutafuta kwa gunia moja la mkulima wangu, eti umpokonye kile kidogo ambacho tumesema kibaki. Tangu mwanzo tulisema, zao hili la mahindi la mkulima huyu, hata mazao mengine ambayo wakulima wadogowadogo wanalima, halitakatwa, halitatozwa hata senti tano, lengo ilikuwa ni kuwezesha kile kilichopangwa kama bei, akipate chote kwa sababu, ndio namna ya kumsaidia. Tukasisitza kwamba, huyu mfanyabiashara anayekwenda kununua kwa huyo mkulima, yeye ndiye atakayetozwa kama ni ushuru, kama ni nini, yeye ndiye atabeba mzigo huo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tulishaliweka liko wazi. Sasa inawezekana bado kuna pengine mkanganyiko kidogo, lakini nataka nirudie kauli ambayo Serikali iliwhi kuisema siku za nyuma, tunataka bei ya mkulima ile anayoipata pale imuache akiwa amepata kamilii kabisa bila kupunguziwa hata senti tano. Nitajaribu kulifuatilia kuona tatizo limeanzia wapi ili tuweze kuwa na uhakika kwamba, halirudii tena.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, lakini vile vile nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, taarifa tulizonazo sasa hivi ni kwamba, nyaraka hizi za kuwataka wakulima hawa wadogo watozwe tozo hii ya asilimia mbili zimesambazwa katika maeneo mbalimbali nchini katika vituo vyote vya ununuzi vya Kitengo cha Hifadhi ya Chakula ya Taifa na maelezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, yanaonesha kwamba, Serikali haikubaliani na jambo hili. Sasa Waziri Mkuu, anaweza akatoa kauli ya kufutwa mara moja nyaraka hizi ili Watanzania hawa wadogo wanaoshughulika na kilimo hiki wawze kufaidika kama jinsi anavyotoa maelekezo yeye mwenyewe?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, tutamwelekeza tu Kamishna wa *TRA*. Nina hakika atalitekeleza, halina mgogoro hata kidogo. Ila naelewa inawezekana tu katika ngazi ya chini pale halikuwa pengine limeelewека vizuri. Hata kwa maelezo haya najua Kitilya ananisikia, kwa hiyo, ni lazima jambo hilo walirekebishe haraka ili mwانanchi huyu aweze kuendelea kuuza zao lake lile la kimaskini bila kubughudhiwa na mtu yeyote.

**MHE. SUSAN L.A. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika Wilaya ya Kilombero kuna mgogoro mkubwa sana wa ardhı ulioanza mwaka 2009 mpaka hivi sasa katika Vijiji vya Namwawala, Mofu, Mbingu, Kisegese, Miyomboni, Idandu na Chiwachiwa na wananchi wako hoi kweli. Lakini mgogoro huo umetika mpaka kwa Rais na Mkuu wa Wilaya anajua na Mkuu wa Mkoa anajua. Lakini ni taarifa tu nimepata kwamba, tarehe 15 Agosti, Mkuu wa Wilaya anakwenda kule na watu wa *SUDECO* kwenda kutaka kuchukua hiyo ardhı ya hawa watu karibu asilimia 95. Je, Waziri Mkuu, unasema nini kuhusu matatizo haya wanayoyapata wananchi wa Kilombero na wengine wameshafunguliwa kesi nyinyi?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kiwanga, angekuwa amenitendea haki kweli kama angekuwa amenipa jambo hili mapema. Kwa sababu, anachohitaji kwa kweli ni taarifa kamili juu ya nini Serikali ingetakiwa ifanye katika tatizo hili la kwake. Sasa akinikurupusha saa hizi na maelezo hayo ya vijiji hivyo, kwangu siyo rahisi kama sijalipata. Lakini nikuhidi tu kwamba, maadamu umelisema nitafuatilia na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro nione tatizo ni nini; maana hukueleza hasa chimbuko ni nini na kwa nini, hatua hiyo imechukuliwa. Mwisho, nitakwambia sasa nimejifunza nini na nimeelekeza nini kifanyike.

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama nilivyotoa taarifa kwamba, Mkuu wa Wilaya anakwenda kule tarahe 15 Agosti, na watu wa *SUDECO* kwenda kufanya maamuzi. Kwa hiyo, nina nyaraka mbalimbali hapa na naomba kwamba, kwa muda wangu nitakuletea hizo nyaraka ili uzipitie uone namna ya kuwaokoa wananchi wa Kilombero. Ahsante.

**MHE. AGNESS E. HOKORORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kauli Mbiu ya Serikali ni Kilimo Kwanza na kwa Mkoa wa Mtwara ni Korosho Kwanza, Serikali iliahidi itapeleka pembejeo za korosho Mkoani Mtwara. Tunaomba utwambie leo, je, Serikali imelitekeleza hilo?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, tulitoa kauli ya kutia matumaini kwamba, jambo hili lingeweza likashughulikiwa mapema iwezekanavyo. Lakini mpaka jana wakati najaribu kutafuta suluhu ya suala hili, angalau nilikuwa nimepata faraja kwa sababu, niliambiwa kwa Mkoa wa Mtwara, *sulphur* ya kutosha imeshasambazwa lakini Lindi, ndio niliambiwa bado hali hajawa nzuri. Lakini leo asubuhi, nilikuwa nimemuuliza Waziri wa Kilimo, suala hili limefikia wapi? Akanihakikishia kwamba, kuna meli imeshaingia bandarini leo ambayo imebeba *sulphur* na imepewa kipaumbele ili *sulphur* ile iweze kutolewa pale haraka iwezekanavyo kwa ajili ya kuelekezwa katika mikoa hii ya Kusini kwa maana ya Mtwara na Lindi. Nitakachomuahidi tu Mheshimiwa dada yangu Hokororo, baada ya hapa pengine nitafuatilia sasa kuona meli hiyo kama upakuaji umekamilika na wameanza *off loading* ili kuweza kuharakisha kupeleka pembejeo hii katika eneo linalohusika.

**MHE. AGNESS E. HOKORORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Namshukuru pia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majibu mazuri na matumaini mapya anayotupa leo kwa Mkoa wa Mtwara, naomba niulize swali dogo la nyongeza. Katika Sheria ya Korosho ya Mwaka 2006, inayotaka sehemu fulani ya fedha za *export levy* zishuke katika Halmashauri za Wilaya na hilo halijafanyika kuanzia mwaka 2006 mpaka sasa. Je, nayo Serikali inatwambia nini katika hilo? Fedha zetu hizo ziko wapi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, umeleta swali jipya! Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri nalielewa jambo hili kwa sababu tangu lilipoibuka tumeanza kulihangaikia sana, tayari nimeshamwandikia barua Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, aweze kufanya ukaguzi wa hesabu zinazohusiana na fedha ambazo kwa mujibu wa Sheria zilitakiwa, kama unavyosema, ziwe zimepelekwa kwenye maeneo

yanayohusika kuanzia mwaka 2006 mpaka hivi sasa. Tumemwambia ajitahidi kuchukua muda mfupi kwa sababu, tunataka tu tujue kama zilipelekwa zimefanya nini? Nani alizishughulikia?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa upande mwingine labda niongeze tu kwa sababu, umelizungumza hili suala, niseme tu, juzi nimeona barua ya Profesa Maghembe, akiwataka wadau wote nadhani na Wabunge wote wa Mikoa hiyo inayolima korosho, mikutane katika Mkutano atakaufanya tarehe 20 Agosti, ule wa wadau, kwa lengo la kupitia zile Kanuni. Kanuni zile ndio zitakazobainisha utaratibu mzima wa namna ya mgawo wa fedha hizi zinazotokana na *export levy*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, labda niwasihii tu Wabunge wote wa Mikoa hiyo miwili na ile mingine inayolima korosho, mshiriki kikamilifu kwenye Mkutano huo ili Kanuni hizi ziweze kweli kujibu hoja na matakwa ya Watanzania.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, utakubaliana na mimi kwamba, Tanzania ni nchi ambayo ilikuwa inaheshimika sana duniani, hususan kipindi cha Mwalimu Nyerere, yaani Awamu ya Kwanza. Lakini heshima hiyo imeendelea kushuka kwa sababu mbalimbali, zikiwemo suala la ufsadi, rushwa. Lakini sasa hivi kuna kubwa zaidi la nchi yetu kuwa mapitio ya dawa za kulevyaa, lakini vile vile kuwa na watu amba wanashiriki katika dawa za kulevyaa. Hili limetamkwa hadharani na Mheshimiwa Rais, mwaka huu, akisema pia Viongozi wa Dini wanashiriki katika biashara hiyo. Mheshimiwa Waziri Mkuu, naamini na wewe kama Mtendaji Mkuu wa Serikali unayaafahamu majina hayo na hata kama huyafahamu Kiongozi wa Nchi anayaafahamu. Sasa naomba kujua ni lini majina hayo tutafahamishwa au ni lini watu hao watapelekwa katika vyombo nya Sheria?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka nitofautiane kidogo na Mheshimiwa Dada yangu Susan Lyimo kwamba, eti heshima ya Tanzania imeshuka kweli kwei! Si kweli, si kweli hata kidogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mmoja kati ya watu wachache amba Nabahatika sana kukutana na Viongozi wa kila aina, nakwenda kwenye mikutano mbalimbali, chati ya Tanzania iko juu sana. Tatizo ninaloliona kwa Watanzania ni kutothamini heshima mnayopewa na watu wanaojua mnachofanya. Ndio maana kila mtu akisimama hoja yake inakuwa ni hiyo ya kujidhalilisha yeche mwenyewe; wakati ukweli sio hivyo! (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua ni jambo moja kuwa na tukio, kwa sababu nchi zote matukio ya hapa na pale yapo. Lakini yapo mambo ya msingi ambayo yanaendelea kujenga heshima ya Taifa hili. Amani na utulivu katika nchi hii, huwezi ukai-*compare* na nchi nyingine zozote kwenye Kanda hii wala mahali popote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Susan Lyimo, katika nchi ambazo bado tunapata *foreign direct investment* licha ya kwamba, dunia nzima imetikisika, Tanzania peke yake katika *Sub-Saharan Africa*, Afrika nzima, ndio bado sisi tuko karibu tunapokea asilimia 90 na wote wanajua kwamba, *we are doing very well*. Uchumi wa nchi hii dada yangu Mheshimiwa Lyimo, ni kati ya nchi bora ambazo tunaaminika kwamba, ndani ya kipindi kifupi kijacho tukienda kwa kasi tunayokwenda nayo tutakuwa ni nchi ambayo tutaingia katika ngazi ya juu zaidi kuliko hivi leo. Sasa wanaowajua ndivyo wanavyowa-assess. Ninyi wenyewe ndio mnaendelea kujiona kwamba, mambo yenu hapa ni hovyo, hayaendi popote! Sasa *this is unfortunate, very unfortunate*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa hili aliloliuliza dada yangu, ungekuwa unasoma taarifa za Tume inayohusika na dawa za kulevyaa, kwani watu hawapelekwi Mahakamani kwa sababu hiyo? Watu hawakamatwi kwa sababu hiyo? Kesi ziko nyingi tu, ambazo tumepeleka watu Mahakamani, kwa hiyo, kubwa hapa ni kuhakikisha tu kwamba, vita hii ujue wala si ya Tanzania peke yake na lenyewe ni tatizo linagusa nchi nyingi. Vinginevyo utauza wapi? Vinginevyo inatoka wapi? Kwa hiyo, ni lazima kutakuwepo na nchi nyingine zaidi, sisi tukazane ku-*fight* kupigana kweli kwenye kuhakikisha hili jambo haliendelei kukua mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini umegusa kidogo juu ya Madhehebu ya Dini. Nataka jamani tuseme ukweli, Rais alipolisema lile wakati alipokuwa amealikwa kwenye shughuli ile ya dini, hakuwa anayashitaki Madhehebu ya Dini yote kwamba, ni watu wanaojihusisha na dawa za kulevyo, hata kidogo! Alitumia nafasi ile kwa sababu, liko dhehebu moja na lilikuwa *reported* sana kwenye gazeti na wote tunajua; kidhehebu kidogo sana, ambacho kilijitokeza na askofu mmoja hivi, Mswahili, Mswahili hivi, kumbe mambo yake ni kutaka kufichama tu kwa kificho cha dini. Alikuwa anatoa angalizo ni *caution* tu! Lakini hakuwa ana-*accuse* Madhehebu, Madhehebu mengi ni mazuri, hawafanyi hizo biashara hata kidogo, lakini alitaka tu wajue kwamba, baadhi yao hasa vikanisa vidogovidogo vinawenza kuwa vinatumia fursa hiyo vibaya. *That's the message* ambayo nilliona alitaka Viongozi wa Madhehebu ya Dini waipate na waisadie Serikali kuweza kusimamia jambo hili kwa pamoja.

Vile vile nakushukuru sana maana nimegusa mambo mengi. Utaniwia radhi kama nimesema mengi kuliko ulivyotegemea. Nakushukuru sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Tunashukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama heshima imeshuka, lakini sio ya Bunge hili. Nakushukuru sana kwa majibu mazuri kwa kipindi hiki muhimu sana kwa nchi yetu, majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunakushukuru sana. (*Makofii*)

Tulikuwa na wauliza maswali tisa, saba wameweza kupata nafasi ya kuuliza, wawili kwa bahati mbaya muda wetu umekwisha. Katibu.

### **MASWALI YA KAWAIDA**

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Baada ya Kipindi cha Maswali, ndio nitapokea Taarifa. Maswali ya Kawaida, swali la kwanza ni la Mheshimiwa Rachel Mashishanga Robert.

Na. 402

### **Matumizi Mabaya na Wizi wa Fedha Za Umma**

**MHE. RACHEL M. ROBERT** aliuliza:-

Taarifa ya CAG na Kamati ya Bunge ya LAAC ya 2007/2008, 2008/2009 inaonesha matumizi mabaya na wizi wa fedha za umma:-

(a) Je, ni Halmashauri zifi (kwa majina) 10, zinaongoza kwa matumizi mabaya (ya aina gani) ya fedha za umma na Serikali imechukua hatua gani kati ya Januari 2008 hadi 30 Disemba 2010, kwa waliohusika kusababisha matumizi mabaya na wizi huo?

(b) Je, Serikali inazichukulia hatua gani Halmashauri hizo?

(c) Katika Manispaa ya Ilala, yapo matumizi ya miradi hewa ya sh. 180,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa zahanati ambazo hazipo kwenye Kata zake. Je, Serikali ina taarifa hiyo? Kama ipo taarifa, itachukua hatua gani kwa Halmashauri hiyo kwa kutumia kiasi hicho cha fedha kwa miradi hewa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA - ELIMU)** aliibuu :-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rachel Mashishanga Robert, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu tatu, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri zilizobainika zaidi kuwa na matumizi ya fedha yasiyordhisha ni pamoja na Halmashauri za Wilaya za Kishapu, Kilosa, Bagamoyo, Mkuranga, Ileje, Geita, Rombo, Tarime, Bunda na Ronya.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zinazochukuliwa kwa watumishi wote wanaosababisha matumizi mabaya ya fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ni pamoja na kufanyiwa uchunguzi na vyombo vya kisheria kama TAKUKURU, kupewa onyo kali, kushushwa ngazi za mishahara, kuvuliwa madaraka na kufikishwa Mahakamani.

Aidha, Kamati ya kudumu ya Bunge, ya Hesabu za Serikali za Mitaa, hupendekeza kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa kwa watumishi wote waliosababisha ubadhirifu, kukatwa asilimia fulani ya mshahara wa mtumishi ili kufidia upotevu huo.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuwepo kwa miradi hewa, Halmashauri ya Manispaa ya Ilala, wakati wa maandalizi ya taarifa ya mafanikio ya Serikali katika mwaka 2005 ilifanya kosa la kiuandishi kwa kuhusisha Mtaa wa Mogo katika Kata ya Kipawa kuwa na Zahanati. Ukweli ni kwamba, Halmashauri hii imetekeleza miradi saba ya ujenzi wa zahanati katika kipindi hicho. Hivyo, nabitishwa kuwa zahanati ya Mogo haipo na hakuna mipango ya hivi karibuni ya kujenga zahanati katika Mtaa huu kwa mujibu wa Halmashauri ya Wilaya ya Manispaa ya Ilala.

**MHE. RACHEL M. ROBERT:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nashukuru Mheshimiwa Waziri, ameitaja Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu kuwa ni kinara wa ubadhirifu wa fedha na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali mwaka 2009/2010, ameendelea kuitaja Halmashauri hii ya Kishapu na Mkuu wa Mkoa, Mheshimiwa Balele, alipigia kelele sana hili jambo na baada ya kulipigia kelele, baadhi ya watumishi walihamishwa. Sasa nataka kuiuliza Serikali, kwa nini imekuwa na huu utaratibu wa kuwashamisha watumishi wa Halmashauri, hasa wanaoonekana wamefanya ubadhirifu kwenye Halmashauri?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, katika majibu yake ya msingi, Mheshimiwa Waziri, amekubaliana na mimi kwamba, zahanati ya Mogo katika manispaa ya Ilala iliyoko katika Jimbo la Segerea, haipo. Lakini Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya *TAMISEMI* na ninalo gazeti hapa la Januari, alikubali kwamba, hizi pesa ziliidhinishwa na zikatumika. Sasa nataka kujua ni akina nani walizitumia na zilitumika kwa ajili ya nini?

**NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU (TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA - ELIMU):** Mheshimiwa Naibu Spika, ubadhirifu wa fedha za Halmashauri ya Kishapu ambao pia ulishafanyiwa ukaguzi, lakini pia Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa alishalitoa kauli nataka nikujulishe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba hatua dhidi ya wale wote ambao wanabainika kufanya ubadhirifu wa fedha zinaendelea kuchukuliwa, wala si tu kwa kuwashamisha watendaji lakini pia kwa kufanya uchukuzi na pindi inapobainika hayo huwa hatua zinachukuliwa. Kwa mfano, katika kipindi cha mwaka 2006 mpaka 2010 tuna jumla ya Halmashauri 30 ambazo hatua mbalimbali za kinidhamu zilichukuliwa kwa Wakurugenzi wao. Wengine wameshavuliwa madaraka lakini wengine kesi zao zinaendelea Mahakamani na michakato ya kinidhamu inaendelea na wale walioshinda kesi labda wale ndiyo ambao wanaweza kuhamishwa kupelekwa mahali pengine. Lakini kama kuna tuhuma yoyote ile adhabu kali inachukuliwa. Lakini pia kwa watumishi wa kawaida ambao pia wanaingia kwenye ubadhirifu wa mali lakini pia na kutokuwa na nidhamu mahali pa kazi nao pia hatua mbalimbali zinachukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, yanayozungumzia fedha za Halmashauri ya Manispaa, ni kweli kwamba Naibu Katibu Mkuu aliwahi kutoa taarifa, sasa nataka nikupe taarifa kwamba katika kipindi kile kulikuwa na fedha jumla ya bilioni 1,206,000,338 ambazo ziliokuwa zimetengwa kuendesha miradi mbalimbali kwenye eneo lile. Nilipozungumza kwamba kuna tatizo la maandishi ambalo lilijitokeza na kwamba hakuna zahanati kwenye Mtaa wa Mogo, ni kwamba Halmashauri ilitumia zile fedha zote zilizokuwa zimetengwa kuititia Baraza la Madiwani na fedha zote zilitumika katika Kata ya Ukonga, Kata ya Segerea, Kinyerezi, Kivule na Chanika na miradi yote imebainishwa na jumla ya fedha imekwenda na ile ambayo iliridhiwa. Kwa hiyo, kuingia kwa zahanati ya Mogo ilikuwa ni kwa makosa kama ambavyo nimeeleza. Ahsante.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa sisi Waheshimiwa Wabunge, mara nyangi tunapoidhinisha bajeti zetu hapa tunaelewa wazi kwamba fedha nyangi zinakwenda katika Halmashauri kwa ajili ya kuleta maendeleo. Lakini imebainika kwamba wizi na ubadhifuru unafanyika kwenye Halmashauri mbalimbali unakosesha wananchi maendeleo. Kuanzia Juni, 2009 hadi 2010 Juni, jumla ya Halmashauri 30 zilibainika na ubadhifuru na ujisadi, watumishi 921 walifikishwa Mahakamani, 14 wakapewa onyo, mmoja akashushwa madaraka na mmoja akashushwa mshahara. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri haoni basi hatuendi sambamba na maneno ya uzinduzi wa Bunge hili kwa Mheshimiwa kwamba hatutovumilia wizi na ubadhifuru, tutakuwa wakali sana na kumhamisha Mkurugenzi kwenda Halmashauri nyngine ili aende akaibe zaidi, Serikali haloni inachochea zaidi ubadhifuru uendele? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA -ELIMU):** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nieleze tu kwamba ni kweli sisi ndiyo tunaidhinisha fedha au bajeti kwa ajili ya kwenda kwenye matumizi ama kwa ajili ya maendeleo kwenye Halmashauri na fedha inatumwa kwenye Halmashauri. Matarajio ya Serikali ni kwamba fedha zile zitatumika kama ambavyo imekusudiwa. Inapotokea kwamba kuna ubadhifuru na hawa kwa kuwa ni watumishi, hatua za kisheria zinatumika. Kama ambavyo nimetoa maelezo hapa ya msingi ya mifano ya wale watumishi Wakurugenzi watumishi katika Halmashauri zile 30 nimeeleza kwamba baada ya uchunguzi wa kina na ni jambo la msingi sana kufanya uchunguzi badala ya kuchukua hatua za haraka kwa sababu unawenza kusababisha hasara ndani ya Serikali kwa kufanya maamuzi ya haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya zile Halmashauri 30 nimeeleza kwamba Wakurugenzi 14 walivuliwa madaraka na hii ni baada ya uchunguzi na kuona kwamba kuna ubadhifuru. Kwa hiyo, unamwondoa wadhifa au madaraka lakini pia unawenza kumfikisha Mahakamani kama vyombo vya uchunguzi vitakuwa vimependekeza kufanya hilo na vyombo hivyo pia ni vya kisheria. Kwa hiyo, Wakurugenzi wawili, kesi zao zinaendelea lakini Wakurugenzi nane, mchakato wa kinidhamu bado unaendelea lakini Wakurugenzi wawili ndiyo waliokuwa wameshinda kesi zao na tuliwarudisha kazini na Mkurugenzi mmoja alishushwa mshahara, Mkurugenzi mmoja alipewa onyo na Mkurugenzi mmoja pia alifunguliwa mashtaka ya nidhamu na sasa ameshafikishwa Mahakamani na kazi hii itaendelea. Endapo itabainika kwamba, kuna Mkurugenzi ametumia vibaya fedha au madaraka yake, hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa swali 402 ukilitazama sana, jinsi lilitiyotungwa, lina maswali madogo sita ndani yake na majibu yaliyotolewa, kwa kweli na muda ambao tumetumia ni mrefu. Basi, tuvumiliane na tusonge mbele. Sasa ni zamu ya Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay.

Na. 403

#### Umuhimu wa Kuwa na Ndege za Taifa

**MHE. JOSEPH R. SELASINI - (K.n.y MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY)** aliuliza:-

Sekta ya Utalii imechangia pato la Taifa kwa Dola bilioni 1.3 mwaka 2010, mapato yanayotokana na watalii kutoka nje kuingia nchini kwa ndege za mashirika mengine na ya Kimataifa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwa na ndege za Taifa ili kuhakikisha usafiri wa uhakika na watalii na wasafiri wengine kuja Tanzania wakati wote na kuzidi kuinua pato la Taifa?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay, Mbunge wa Mbulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imechukua hatua za makusudi za kuwa na ndege za Taifa ili kuinua pato la nchi kwa kuishirikisha Sekta binafsi ili kutoa huduma za usafiri wa anga badala ya kuitegemea Serikali. Kupitia Sekta binafsi, nchi yetu imeweza kuwa na kampuni za ndege kama vile *Precision Air*, *Coastal Travel*, *Zan Air*, *Safari Plus Air* na mengineyo ambayo yamesaidia katika shughuli za kiuchumi na kuinua pato la Taifa. Serikali pia imeendelea kuwahamasisha wawekezaji kutoka nje ya nchi kuanzisha kampuni binafsi zitakazomilikiwa kwa asilimia mia moja na wawekezaji hao au kwa kushirikiana na wananchi wa Tanzania katika umiliki. Katika utaratibu huo, makampuni hayo huandikishwa nchini na shughuli zake kuu kufanyika hapa hapa nchini. Huduma za makampuni hayo hudhibitiwa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (*TCAA*) kwani, hutambulika kama makampuni ya ndani na hivyo kupata haki kama kampuni za ndege za Tanzania, bila kujali umiliki wake. Kupitia utaratibu huu, tangu Novemba 2010, kampuni za *Fly 540* na *Jet Link* zimesajiliwa na zinatoa huduma ndani ya nchi. Tuna kampuni nyingine *Africa Air Line International* ambayo sasa inafanya *fly test* mpaka Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia imekuwa ikifanya jitihada za kuimarisha Kampuni ya Ndege Tanzania (*ATCL*) kwa kutoa fedha za matengenezo ya ndege, kulipia mishahara na kuchukua baadhi ya madeni ingawa hatua hizo bado hazijaza matunda yaliyokusudiwa. Serikali itaendelea kuisaidia kampuni kwa kutenga fedha za kuiwezesha kuendelea kutoa huduma za usafiri wa anga wakati mchakato wa kumtafuta mwekezaji ukiendelea. Pamoja na hayo, Serikali inafanya mazungumzo na wawekezaji mbalimbali ili kumpata ambaye tutasaidiana naye kuiboresha *ATCL* na huduma zake.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ningependa kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo: Kwa kuwa Shirika letu la Ndege (*ATC*) bado halijaanza kufanya kazi na kwa kuwa Serikali imeanza kuhamasisha makampuni binafsi kusajiliwa kwa ajili ya kusafirisha watalii, je, Serikali inaweza kuwahakikishia vipi wadau wa utalii, yaani Tanzania *Tourist Board TANAPA* na makampuni binafsi kwamba makampuni hayo binafsi ya ndege yatakuwa yanafanya kazi hii kwa hakika yaani kuwatoa watalii kwenye nchi zao mpaka hapa nchini, bila kuathiri biashara yenewe ya utalii?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa makampuni binafsi ya utalii, mashirika kama Tanzania *Tourist Board* na *TANAPA*, watalii wanapatikana hasa nchi za bara la Marekani, Ulaya pia na Asia, tunao mpango na Marekani wa *open sky*, pia tuna mkataba na China pamoja na India kupitia *bilateral air service agreement (BAS)* ili tuweze kufanikisha watalii wa kutosha wanakuja hapa nchini na kutembelea mbuga zetu za wanyama.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru naomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa Kigoma hatuna ndege ya moja kwa moja kutoka Dar es Salaam kwenda Kigoma na watu kule wanatumia mabasi kutoka Kigoma kuja Dar es Salaam na treni inayokwenda ni ya daraja la tatu, je, Waziri atatupa lini daraja la pili ili wale wagonjwa wanaopewa *referral* kutoka Kigoma, Tabora kuja Dar es Salaam ili waje wamelala?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli usafiri wa anga ulikuwa umesitishwa kwa muda lakini *ATC* muda si mrefu itaanza usafiri wake Kigoma na Tabora. Lakini pia tuna ndege moja inayotoka Mwanza kwenda Kigoma, najua bei ni kubwa zaidi, pia nimezungumzia kwamba kuna hili shirika la *African Air line International* ambalo tayari limeshafanya *test flight* kwenda Kigoma. Tunajua mashirika mengine pia yatashiriki katika usafiri wa anga. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge mara baada ya bajeti yetu kupitishwa, tutakuwa na mabehewa ya kutosha ya daraja la tatu, pili, na la kwanza treni zinazokwenda Kigoma ili ndugu zangu wa Kigoma na Tabora waweze kusafiri vizuri katika kupata huduma katika hospitali za rufaa wanapotoka maeneo hayo kuja Dar es Salaam.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa watalii wengi nchini huwa wanatoka na ndege zao kutoka nchi zao mpaka katika maeneo ya utalii nchini kama kwenye mbuga zetu za wanyama. Je, sasa Serikali haioni ni wakati muafaka wa kutunga sheria inayowataka watalii wote wanaokuja nchini kutumia usafiri wa ndani ili kusaidia sekta ya utalii kukua zaidi, ambayo itasaidia kuongeza pato la Taifa na wananchi wote wanaohusika na sekta hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, makubaliano ya usafiri wa anga hayawesi kutukataza sisi tusimruhusu mtu ambaye ana ndege anataka kuja nayo hapa. Kwanza, tunapata malipo kwa kutua ile ndege na kupaki ile ndege na atanunua mafuta hapa lakini pia anapofanya hivyo anatutangazia kule wanakotoka ili watalii wengi zaidi waje. Kwa hiyo tunampa *option* yule mtalii kama akitaka kutumia usafiri wa ndani hapa pia tunaruhusu, wazo ni zuri lakini Sheria za Usafiri wa Anga, hazitukatazi kumruhusu mtu kuja na ndege yake, *in fact* mapato yanakuwa mengi zaidi kwa kufanya hivyo.

Na. 404

### **Utengenezaji na Uuzaji Vyakula Kiholela**

**MHE. LUCY P. OWENYA** aliuliza:-

Kumekuwepo na utengenezaji na uuzaji wa vyakula kiholela jambo ambalo ni hatari kwa walaji kama hakuna uangalifu katika zoezi hili:-

Je, ni kwa jinsi gani mamlaka husika (*TFDA*) inachangia kwa kutoa elimu au kuzuia ukiukwaji wa taratibu na kanuni za utengenezaji wa vyakula?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, usindikaji, hifadhi, usafirishaji wa chakula unasihamiwa kwa mujibu wa Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Na. 1 ya mwaka 2003 pamoja na kanuni zilizo chini ya Sheria hiyo. Lengo ni kuhakikisha kuwa chakula kinachowafikia walaji ni salama ili kulinda afya zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutohana na kukua kwa sekta isiyo rasmi, kumekuwa na ongezeko la wafanyabiashara wanaotengeneza na kuuza vyakula bila kuzingatia masharti yaliyowekwa chini ya sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya mwaka 2003. Pamoja na kuwepo kwa sheria hiyo kumekuwepo na changamoto ya wajasiriamali wadogo wa vyakula wanaoshindwa kutimiza masharti ya biashara kutohana na mitaji midogo waliyokuwa nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya mbinu zinazotumiwa na *TFDA* kukabiliana na changamoto hiyo na kuimarisha usalama na ubora wa vyakula vinavyozalishwa na sekta isiyo rasmi ni kama ifuatavyo:-

(i) Kutoa mafunzo kwa wajasiriamali wanaojihusisha na uzalishaji wa vyakula hususan viwanda vidogo, juu ya mbinu za utayarishaji wa chakula salama na bora, hata katika mazingira magumu. Mafunzo haya hutolewa kwa ushirikiano na *SIDO*. Aidha, elimu hutolewa kupitia maonesho mbalimbali kama wiki ya Utumishi wa Umma, Sabasaba na Nanenane.

(ii) Kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari juu ya misingi ya usindikaji bora, kanuni za usafi na matakwa ya sheria katika uanzishwaji wa biashara za usindikaji kwa lengo la kuwapa wananchi uelewa wa kubaini vyakula ambavyo vinaweza kuhatarisha afya zao.

(iii) Kuendesha ukaguzi wa mara kwa mara kwenye maeneo ya kutengeneza na kuuza vyakula na pale inapoonekana mazingira ni tishio kwa afya ya jamii biashara hufungwa na hatua zaidi za kisheria kuchukuliwa.

(iv) Ili kuimarisha ukaguzi huu *TFDA* imanzisha Ofisi za Kanda, Kanda za Ziwa, Kaskazini, Mashariki na Nyanda za Juu Kusini. Matarajio ni kuongeza Ofisi za Kanda ya Kati, Magharibi na Kusini. Hatua hii itaongeza udhibiti wa bidhaa ikiwa ni pamoja na vyakula. Aidha, mamlaka inakasimu baadhi ya majukumu kwenye ngazi ya Halmashauri kwa lengo la kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, natoa rai kwa wananchi wote pamoja na Waheshimiwa Wabunge, kutoa taarifa za ukiukwaji wa sheria kwenye Ofisi ya *TFDA* Makao Makuu, Ofisi za Kanda na Ofisi za Afya za Mkoa na Halmashauri, wanapogundua ukiukwaji wa sheria ili kuwezesha mamlaka ya kuchukua hatua zinazostahili na kulinda afya za wananchi. Aidha, nawashukuru wote ambao wamekuwa wakitoa taarifa kwani kwa kufanya hivyo, wanatoa mchango chanya katika shughuli za udhibiti na usalama wa vyakula.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Sina uhakika kama *TFDA* huwa inawaangalia mama nitilie, mama nitilie huwa wanapika vyakula kwenye mazingira ya hali ngumu sana na sehemu nyingine huwa hawana hata maji ya kusafishia vyombo vile, hali ambayo inapelekeea saa nyingine kupata magonjwa ya mlipuko, sijui Serikali inawasaidiaje ili kuhakikisha kwamba wanatengeneza vyakula vile kwenye mazingira ya hali ya usafi ili kupunguza magonjwa ya mlipuko? (*Makofi*)

Pili, ningependa kupata jibu kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, ni kwa jinsi gani vyakula hivi vinachangia magonjwa sugu kama vile kisukari, *blood pressure* ya juu, saratani pamoja na hayo magonjwa ya mlipuko?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba, hawa akinamama nitilie wanapika kwenye maeneo ya Halmashauri ama Serikali za Mitaa, majukumu haya tumeyakasimu kwa bwana afya wa Halmashauri ndiye anayetakiwa kuwa anawazungukia na kuwapa elimu. Pale ambapo anaona kwamba mazingira ni machafu kabisa basi watafute maeneo mbadala ili wale akinamama waweze kujikimu kiuchumi siyo kuwafungia, ila nasema kwamba wapate elimu na wahamishiwe sehemu ambazo ni salama. Jukumu hili limekasimiwa Halmashauri.

Swali la pili, ni kwa kiasi gani vyakula hivi ambavyo vinapikwa, nafikiri siyo mama nitilie tu, hebu tuulize kwamba ni vyakula gani ambavyo au ni kwa namna gani vyakula vinaweza vikachangia maradhi ya kisukari, vikachangia saratani na maradhi mengine sugu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila kitu ambacho binadamu anakula hakina usalama ndani ya mwili wake kama hatakula kwa kiasi, ila naomba kusema kwamba kuna aina nyingine za mafuta ambayo tunafuatilia sasa hivi ambayo najua kwamba, kama tukifuatilia vizuri tutaona kwamba kuna mchango gani katika kuchangia sukari, kuchangia *hypertension* pamoja na maradhi mengine ambayo ni sugu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema kwamba, sisi kama Watanzania tuangalie ni namna gani tunarudi kula vyakula walivyokuwa wanakula wazazi wetu wa zamani vya kuchemsha, tusipende sana kukaanga ila napenda kutoa tahadhari kwamba hizi biashara za Chips Mayai zinazokaangwa barabarani, naomba kusema kwamba havina usalama sana ila juhudi tutakayofanya kama Wizara ya Afya ni kuwaelimisha waweze kupika chakula ambacho ni salama.

**NAIBU SPIKA:** Tuitendee haki Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu, swalii la mwisho asubuhi ya leo na linaulizwa na Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa.

Na. 405

#### **Walimu wa Ufundu Kutoajiriwa**

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA** aliuliza:-

Walimu wote wanaomaliza mafunzo ya ualimu wa ufundu hukosa ajira Serikalini ingawa Serikali ina upungufu mkubwa wa walimu wa ufundu.

Je, ni sababu zipi zinaifanya Serikali isiajiri walimu hao, mfano walimu waliomaliza *VETA* Morogoro mwaka 2010?

## **NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa, Mbunge wa Kibiti kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo ya ualimu wa ufundi nchini yapo ya aina mbili na hutolewa katika vyuo viwili tu. Chuo cha Ualimu Kleruu hutoa mafunzo ya ualimu katika ngazi ya stashahada na Chuo cha Ufundi Stadi Morogoro hutoa mafunzo ya Ualimu wa Ufundi katika ngazi ya Cheti na Stashahada. Walimu wa ufundi huandaliwa kufundisha katika shule za sekondari za ufundi na walimu wa ufundi stadi huandaliwa maalum kufundisha katika vyuo vya ufundi stadi na kujajiri wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, wahitimu wa Chuo cha Ualimu cha *VETA*, Morogoro wa mwaka 2010 walikuwa 87, kati yao 35 walitoka vyuo mbalimbali vya ufundi stadi yaani *in service*, hivyo baada ya kuhitimu walirudi kazini. Hata hivyo, wahitimu 13 kati ya 52 walijigharamia wenyewe walijiriwa katika vyuo vya *VETA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha *VETA*, Morogoro kinaandaa walimu wa ufundi stadi kwa ajili ya soko la ajira ambalo linapanuka na vilevile kuwawezesha kuajiriwa katika vyuo binafsi vya ufundi ambavyo kwa sasa ni 672 nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa lengo kubwa la Serikali ni kuwawezesha wahitimu wanaomaliza mafunzo hayo ya ufundi stadi kuingia katika ujasiriamali au kushindana katika soko huria. Hivyo, walimu wa ufundi wasio na ajira ambao pia ni mafundi wanaweza kutumia fursa zilizopo kujajiri au kujunga pamoja na hivyo kuweza kupata mikopo kutoka Taasisi za fedha kuendesha maisha yao.

**NAIBU SPIKA:** Afisa Elimu, Mheshimiwa Abdul Marombwa!

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi na pia nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyonipatia. Pamoja na majibu mazuri hayo nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Serikali yetu inatarajia kuanzia mwakani kufungua vyuo vya ufundi katika kila Wilaya. Je, Serikali imejibandaa namna gani ili kuhakikisha kuwa Walimu wanapatikana, yasije kutokea kama yaliyotokea katika mpango wa MMES ambao tulijenga shule za sekondari bila kuwa na Walimu. Je, Serikali ina mpango gani kuhusiana na hilo?

Pili, ni kwamba kwa kuwa mpaka sasa bado katika vyuo vyetu vingi sana vya ufundi vya Serikali vina upungufu mkubwa na kwa kuwa Walimu waliobaka ni 39 tu. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwachukua Walimu hawa kwa dharura ili waweze kuajiriwa na kufundisha katika Vyuo vya Ufundi vya Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa Serikali imedhamiria kujenga au kuanzisha Vyuo vya Ufundi Stadi kila Wilaya na pale ambapo tutashindwa kwa miaka hii miwili au mitatu basi tunavibadilisha vile vyuo vya *FDCs* kuwa Vyuo vya Ufundi, *VETA*. Lakini tuna changamoto hii ya Walimu kama anavyosema kwamba katika Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES), tatizo lilikuwa ni Walimu, tulianza kujenga kabla ya Walimu lakini vile vile hata katika mpango huu wa hivi vyuo vya *VETA* tumeshapata fundisho hilo na tunajitahidi sasa kudahili Walimu wengi wa ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inao utaratibu wa kupata Walimu wa ufundi stadi kama nilivyosema Vyuo vya Kleruu, Iringa na Chuo cha Morogoro kwa ajili ya ualimu. Lakini vile vile tunavyo vyuo vingi, tunacho Chuo cha *DIT* yaani *Dar es Salaam Institute of Technology*, tuna *MIST* Chuo cha Ufundi, Mbeya yaani *Mbeya Institute of Science and Technology*, tunayo *AIT* yaani *Arusha Technical College* na *St. Joseph*. Vyote hivyo tumeongeza udahili na maana yake kila mwaka tunategemea Walimu wa vyuo wamalize kuanzia 550. Kwa hiyo, nina uhakika ndani ya miaka miwili mpaka mitatu tutapata Walimu wengi wa Vyuo vya Ufundi *VETA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda kutoa elimu kidogo kwa Wabunge wenzangu kwamba *ratio* ya Walimu wa vyuo ni tofauti kidogo na *ratio* ya Walimu wa sekondari. *Ratio* ya Walimu wa sekondari tunasema Mwalimu mmoja awe na wanafunzi 40 darasani lakini kwenye vyuo vya ufundi tunasema Mwalimu mmoja kwa *ratio* ya wanafunzi 16 tu. Kwa hiyo, udahili wa walimu utakuwa unaendelea kuongezeka kadri ya changamoto hii ya *ratio* ya Walimu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge maswali ya leo yamekwisha na muda wetu nao umekwisha, nimekuona Mheshimiwa Silinde umesimama.

## TAARIFA

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, wakati kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu kinakwisha nilisima kutaka kutoa taarifa na taarifa yangu ni kama ifuatavyo.....

**NAIBU SPIKA:** Kabla hujatoa taarifa, taarifa hiyo unampa nani?

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hiyo ninaipeleka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusiana na jibu alilolitoa.....

**NAIBU SPIKA:** Unatumia kifungu gani cha Kanuni, naomba ukisome.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni ya 68(8).

**NAIBU SPIKA:** Naomba uisome.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Kanuni ya 68 inasema; Vilevile Mbunge yejote anaweza kusimama mahali pake na kusema taarifa na kwa ruhusa ya Spika atatoa taarifa au ufanuzi wa Mbunge anayesema ambapo Spika atamtaka Mbunge anayeketi kusikiliza taarifa hiyo.'

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ukisoma kifungu hiki kinahusu Mbunge anayechangia wakati akizungumza katika mazungumzo yake kama kuna jambo ambalo unahitaji kumpa taarifa utamtaarifu Spika ili amwambie huyo anayesema wakati huo aketi ili umpe taarifa yako. Lakini huwezi kuitumia kifungu hiki baada ya jambo hilo kuwa limepita, inatakiwa utafute utaratibu tena mwingine lakini siyo utaratibu wa taarifa.

Naomba niendelee na matangazo baada ya hapo tutaendelea kama kuna jambo lingine, uendelee kujipanga lakini kwa Kanuni hiyo umechemsha.

Lakini la pili si rahisi Mbunge yejote kumpa taarifa Waziri kwa sababu Waziri anachokisema ni msimamo wa Serikali. Wewe umeuliza swali, Waziri anakujibu kutokana na Serikali ambavyo imeona kufuatana na jambo hilo, sasa utampa taarifa ipi? Lakini kama ni uchangiaji wa kawaida au mambo ya namna hiyo inatakiwa utumie jambo lingine lakini taarifa kidogo inakuwa haikai sawasawa. Kipindi cha maswali kwa kawaida *tradition* ya Bunge hili huwa hatutoleani taarifa, kuna mtu anatikisa kichwa nadhani ni Esther Matiko au nani? Ninapoelekeza sibishani, ninapoelekeza, unaniskiliza vizuri, unakwenda na ninachokisema ili hoja yako iweze kufika vizuri na ili uweze kuzitumia Kanuni hizi vizuri kwa sababu siyo la kwake ni la Serikali.

Sina haja ya kufundisha ziko namna na vifungu vingine vya kuvitumia ili ujumbe wako uweze kufika lakini taarifa siyo mahali pake, waulizeni Wabunge ambaao ni Ma-senator hapa watawaeleza.

Waheshimiwa Wabunge nina matangazo, wageni walipo katika jukwaa la Spika ni wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Dokta Emmanuel Nchimbi ambaao ni pamoja na Ndugu Jane Kijazi Nchimbi ambaye ni mke wake, Mama Nchimbi karibu sana. Alex Nchimbi ambaye ni mdogo wake na Dokta Margreth Mtaki, Mwenyekiti wa *TUGHE*. Karibuni sana. (*Makofii*)

Pili, Wakurugenzi na Wakurugenzi wasaidizi, Wakuu wa Asasi na Taasisi zilizo chini ya Wizara pamoja na wadau wote wa Habari, Utamaduni na Michezo wakiongozwa na Sethi Kamhuanda, Katibu Mkuu na Sihaba Nkinga, Naibu Katibu Mkuu. Karibuni sana. (*Makofî*)

Kwa hatua hii niwatambue endapo wapo jukwaa la Spika, Wahariri wote mliopo humu ndani na naomba kama mpo msimame mahali mlipo. Ahsanteni na karibuni sana katika Bunge letu. (*Makofî*)

Naomba niwatambue Wenyeviti wa Bodi na Mabaraza ambaao ni Ndugu Rose Sayore, Dokta Frowin Nyoni, Profesa Elias Jengo, Ndugu Lalua Simba na Ndugu Kanali Iddi Kipingu. Karibuni sana. (*Makofî*)

Nne, ni wageni wa Mheshimiwa Joseph Mbilinyi Mbunge wa Mbeya, Mheshimiwa Sugu, Waziri Kivuli wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ambaao ni Ndugu Thabit Mtambuzi, Baba mlezi wake wakati akiwa nchini Marekani. Ahsante sana kwa kumlea Mheshimiwa Mbunge. (*Makofî*)

Wasanii wa Bongo Fleva pia wamefika ukumbini hapa, lakini naomba niwatambue wachache mionganoni mwao ni Ndugu Afande Selle oooh! Uko kwenye Jukwaa jekundu! Karibu sana. Pia ndugu Soggy Doggy, Dokta Levy, Ndugu Dani Msimamo, Ndugu Hisabati na Ndugu Rama Dee. Ahsante sana. (*Makofî*)

Wapo pia watangazaji wa Mbeya FM Ndugu Stan Lambat na Ndugu Jackline. Karibuni sana. (*Makofî*)

Pia kuna wageni wa Mheshimiwa Charles Muhangwa Kitwanga, Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia (Mawe Matatu) Ndugu Pammila Petruka, *Associate Professor, University of Saskatchewan*. Ahsante sana. (*Makofî*)

Ndugu Emmanuel Makongoro *Programme Coordinator, Green Hope Tanzania*, Ndugu Tumaini Lusenga *International Liaison Director Green House USA* na Ndugu Juma Waziri Ndondé *Coordinator*. Karibuni sana. (*Makofî*)

Lakini pia wapo wageni muhimu sana asubuhi ya leo nao ni, Kamati ya Utendaji ya Umoja wa Vijana Chama cha Mapinduzi Taifa, wanaongozwa na Mfaume Ally Kizito, Naibu Katibu Mkuu Bara. Karibuni vijana tunajua mnafanya kazi nzuri na hivi karibuni tunawatarajia katika baadhi ya maeneo kule Tabora na Arusha, kazi nzuri. (*Makofî*)

Pia kuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge waliopo katika jukwaa la wageni ni pamoja na wageni wa Mheshimiwa Angella Jasmine Kairuki kutoka Taasisi ya Kijerumani ya FES hapa nchini wakiongozwa na Dokta Stephan Chrobot Mkurugenzi Mkazi. Ahsante sana. (*Makofî*)

Wageni waliofika kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 70 kutoka Shule ya Sekondari ya Jamhuri Dodoma, kama kawaida yenu wanafunzi wa Jamhuri kwa kweli mko *smart*, naomba wanafunzi wanaoona sasa hivi nchi nzima waangalie wanafunzi wa Shule ya Jamhuri Dodoma na waige utaratibu huu. Karibuni sana Bungeni, wanafunzi wengine nao wanakaribishwa Bungeni na u-*smart* huu uendane na utendaji mzuri zaidi katika kufaulu mitihani yetu. Tunawataktak kila la kheri wanafunzi na Walimu wote mliokuja. (*Makofî*)

Vile vile kuna Wasanii sita wa KISUVITA kutoka Manispaa ya Dodoma na Wasanii wa tasnia ya filamu kutoka, Dar es Salaam, karibuni sana. (*Makofî*)

Pia kuna wageni wa Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu ambaao ni Baraka Kange, Rais wa wanafunzi India, karibu sana utupelekee salam kwa vijana wenzako. Waziri Mushashi mwanafunzi wa CBE na Ahmed Mikhe mwanafunzi wa Kairuki *University*. Karibuni sana. (*Makofî*)

Matangazo ya kazi naanza na tangazo la Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika Mheshimiwa Profesa Jumanne Abdallah Maghembe ambaye anatangaza kwamba kikao cha wadau wa Korosho kitafanyika hapa Dodoma, Jumamosi tarehe 20 Agosti, 2011.

Mheshimiwa Profesa David Homeli Mwakyusa, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, anatangaza kuwa kikao cha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, anawatangazia Wajumbe wa Kamati yake kwamba, saa 7.15 mchana leo kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo katika ukumbi wa Pius Msekwa C.

Makamu Mwenyekiti, Diana M. Chilolo, Kamati ya Nishati na Madini anawaomba Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini tarehe 11 Agosti, kutakuwa na kikao cha Kamati, ukumbi namba 231 bila kukosa.

Baada ya matangazo hayo, nitamwita... Karibu.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mwongozo wa Spika!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika unasimama mahali pako kwa kawaida nitakuona huja haja ya kuweka *microphone on*, nikishakuona nitakupa nafasi. Sasa nakupa nafasi!

Kwa Mbunge mwengine yejote, usiwashe *microphone* mpaka nimekuruhusu ufanye hivyo.

Mheshimiwa Mnyika!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 68(7) na Kanuni ya 133.

Kanuni ya 68(7) inasema; "Halikadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwengine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea mapema Bungeni ili Spika atoe ufanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa na kama haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa papo kwa papo au kadri atakavyoona inafaa."

Kanuni ya 133 inasema; '.....

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana huja haja ya kwenda huko kwa kuwa hii imekidhi.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kanuni ya 133(1) inasema; "Mbunge yejote anaweza kutoa taarifa ya maandishi kwa Spika ya kutaka kuleta hoja ya kutokuwa na imani na Waziri Mkuu kwa mujibu wa Ibara ya 53(a) ya Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na kawaida katika kipindi cha maswali na majibu kwa Waziri Mkuu, kwa Waziri Mkuu kutoa majibu yenye upotoshaji...

**NAIBU SPIKA:** Hebu kaa chini! Mheshimiwa John Mnyika, nawaombeni tuheshimu sana kikao hiki. Kanuni unayotaka kuitumia hiyo ya huko mbele inasema: "Mbunge yejote aweza kuleta taarifa ya maandishi" kama hivyo ndivyo unatakiwa ukaandike uilette katika maandishi. Huwezi kutumia fursa hiyo badala ya kuleta taarifa ya maandishi, wewe unaanza kusema humu ndani. Ni kutumia vibaya Kanuni. Usitikise kichwa! Hapanai! Unachotakiwa utumie hapa ni hiyo ulioanza nayo Kanuni ya 7 ya Mwongozo, lakini kama ni ya maandishi hebu isome tena. Irudie hiyo ya maandishi!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba unisikilize.

**NAIBU SPIKA:** Isome tena na Wabunge wote wafungue Kanuni zao ili tuendelee.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Naomba unisikilize kama nimekiuka Kanuni unihukumu baada ya kumaliza maelezo yangu.

**NAIBU SPIKA:** Isome tena tusibishane!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimenukuu Kanuni ya 133.

**NAIBU SPIKA:** Kanuni ya 133

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Ambayo nainukuu tena.

**NAIBU SPIKA:** Subiri kidogo! Kanuni ya 133, kila mwenye Kanuni yake aifungue.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Ambayo nainukuu tena.

**NAIBU SPIKA:** Subiri nitakupa nafasi. Kila mtu afungue Kanuni ya 133. Kanuni ya 133, sasa unaruhusiwa kuisoma.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** "Mbunge ye yeyote anaweza kutoa taarifa ya maandishi kwa Spika ya kutaka kuleta hoja ya kutokuwa na imani na Waziri Mkuu kwa mujibu wa Ibara ya 53A ya Katiba." Mwisho wa kunukuu.

**NAIBU SPIKA:** Sasa kaa chini.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Naomba unisikilize!

**NAIBU SPIKA:** Kaa chini!

**WABUNGE FULANI:** Mmmh!

**NAIBU SPIKA:** Naomba sana Mheshimiwa John Mnyika na Waheshimiwa Wabunge wote mwelewe na tuheshimiane. Ni vizuri kuzitumia Kanuni kadri ambavyo zinatakiwa zitumiwe. Kanuni inasema: "Mbunge ye yeyote anaweza kutoa taarifa ya maandishi kwa Spika ya kutaka kuleta hoja ya kutokuwa na imani kwa Waziri Mkuu kwa mujibu wa Ibara ya 53A ya Katiba.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Nisikilize.

**NAIBU SPIKA:** Nisikilize nini wakati Mbunge ye yeyote unaruhusiwa kuleta hoja ya maandishi? Unachopaswa ni kuleta hoja ya maandishi. Basi! Yah! (*Makof!*)

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo kwenye Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, naomba sasa kutoa hoja ya kuliomba Bunge lako likubali kuitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na Asasi zake katika mwaka wa fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kutumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwangi wa rehema, kwa kutuwezesha kukutana tena kwenye Bunge lako Tukufu tukiwa wenye afya na uzima. Namshukuru pia kwa kujalia nchi yetu kubaki katika amani na utulivu hasa baada ya kupita katika kipindi muhimu cha Uchaguzi Mkuu mwezi Oktoba, 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kuwa Rais kwa kipindi cha pili na Mheshimiwa Dokta Mohamed Gharib Bilali, kuwa Makamu wake. Pia,

napenda kutumia nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Dokta Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Katavi kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kwa mara nyingine kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha, naomba nimpongeze Mheshimiwa, Anna Makinda, Mbunge wa Njombe, kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa kwanza mwanamke wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nakupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. Nawapongeza pia waliochaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge na Wenyeviti wa Kamati mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwa namna ya pekee niwapongeze viongozi wote walioeteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuongoza Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali. Pongezi za pekee pia ziwaendee Wabunge wote waliochaguliwa na wananchi na wengine kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na ambao wamejunga katika Bunge lako Tukufu kutoka katika Chama cha Mapinduzi na Vyama vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa mara ya kwanza kama Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Napenda kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, kwa heshima aliyonipa ya kunteua kuwa Waziri anayesimamia majukumu ya Wizara hii na pia kumteua Mheshimiwa Dokta Fenella Mukangara kuwa Naibu Waziri.

Aidha, nawashukuru kipekee wananchi wa Jimbo langu la Uchaguzi la Songea Mjini, kwa moyo wao wa upendo wa kunichagua tena ili niendelee kusaidiana nao katika utekelezaji wa majukumu ya kuleta maendeleo katika Jimbo letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru pia Watanzania wote hususan Vijana, Wanamichezo, Wasanii na Wanahabari kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kuniapatia tangu nilipoteuliwa. Kwa namna ya pekee, naomba nikishukuru Chama Cha Mapinduzi, kwa kunteua kuwa mgombea wa Jimbo la Songea Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, sitaisahau familia yangu, hasa mke wangu mpendwa, Jane Kijazi Nchimbi na watoto wangu, kwa uvumilivu wao wa kukosa kuwa nami muda mwingi ninapokuwa nikitekeleza majukumu ya Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuzindua rasmi, Rasimu ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambayo kwa mara ya kwanza inatoa vipaumbele na mwelekeo wa nchi yetu kwa miaka mitano ijayo. Nawapongeza Mawaziri waliotangulia kuwasilisha hoja zao, hususan Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, kwa hotuba yake fasaha yenye maelekezo ya utekelezaji wa kazi za Serikali kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012. Waziri Mkuu ameanisha malengo ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo, Malengo ya Milenia na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA II).

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nampongeza Mheshimiwa Stephen Wasira, Waziri, Ofisi ya Rais Mahusiano ya Jamii; kwa kuwasilisha rasmi Rasimu ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano kwenye Bunge lako Tukufu. Namshukuru pia, Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkullo, Mbunge na Waziri wa Fedha kwa hotuba yake nzuri inayoonesha hali ya uchumi nchini na mipango ya maendeleo ambayo imetoa mwelekeo wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hiyo pia imetoa mwelekeo wa hali ya uchumi wa nchi ulivyo na mapato ya Serikali. Naomba kwa namna ya pekee niwashukuru Waheshimiwa Wabunge waliochangia hotuba za Mawaziri wallonitangulia. Maoni waliyotoa yamesaidia kuboresha mipango ya Serikali katika sekta mbalimbali, zikiwemo sekta zilizoko chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya awali, naomba sasa kutumia fursa hii kuipongeza na kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, ambayo

inaongozwa na Mbunge wa Jimbo la Peramiho, Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama na Makamu Mwenyekiti wake Mbunge wa Jimbo la Kondoa Kusini, Mheshimiwa Juma Nkamia kwa kuchaguliwa kwao kuiongoza Kamati hii. Aidha, naishukuru Kamati hii kwa kujadili na kutoa ushauri kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara tarehe 2 hadi 3 Juni, 2011. Wizara inaendelea kufanya kazi ushauri pamoja na maelekezo yaliyotolewa na Kamati ya Bunge lako Tukufu wakati wa kujadili bajeti ya mwaka huu ili kuendelea kuboresha zaidi utekelezaji wa majukumu yetu kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba yangu imegawanyika katika maeneo makuu manne kama ifuatavyo: Sehemu ya kwanza majukumu ya Wizara, sehemu ya pili ni Mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011, sehemu ya tatu inahusu Malengo ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2011/2012 na sehemu ya nne ni makadirio ya bajeti kwa mwaka wa Fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inatekeleza majukumu yafuatayo:-

- Kuendeleza, kusimamia, kutathimini na kupitia utekelezaji wa sera, viwango na miongozo ya Sekta za Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.
- Msemaji Mkuu wa Serikali juu ya masuala ya sera na programu zake.
- Kuandikisha Magazeti, Majarida na Machapisho mbalimbali.
- Kuratibu vitengo vya mawasiliano vya Serikali.
- Kuendeleza, kuwezesha na kuratibu masuala ya kuwajengea uwezo watumishi wa Idara za Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.
- Kufuatilia na kutathmini utendaji kazi wa vyombo vya habari.
- Kuainisha na kuishauri Serikali juu ya namna ya kuendeleza juhudhi binafsi na kubuni mikakati ya kuwaendeleza Vijana.
- Kuainisha na kuendeleza fursa mbalimbali za uwezeshaji wa vijana.
- Kuwezesha kwa kuhusisha masuala ya maendeleo ya vijana katika sekta zote.
- Kuhuisha utengenezaji wa cinema, maigizo, maonyesho na utoaji wa leseni.
- Kufuatilia na kuratibu utendaji kazi wa Taasisi zinazohusiana na Utamaduni chini ya Wizara.
- Kuanzisha njia za kusukuma ubadilishanaji wa programu za Utamaduni wa Kimataifa.
- Kuainisha mahitaji na kutoa misaada na zawadi kwenye maeneo yanayoonesha ufanisi katika masuala ya Utamaduni.
- Kutoa miongozo ya maadili Kitaifa.
- Kuweka njia za kukuza tamaduni, mila, sanaa, lugha na michezo.
- Kuanzisha, kuendeleza na kuratibu usambazaji wa habari zinazohusiana na michezo kutoka ngazi ya Kijiji hadi Taifa; na
- Kuanzisha miundombinu endelevu ya michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2010/2011, Wizara ilipanga kukusanya Mapato ya jumla ya shilingi 697,601,000 kutoka vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Juni, 2011 jumla ya sh. 442,899,176/= zilikuwa zimekusanya ambazo ni sawa na asilimia 63 ya lengo la makusanyo ya mwaka. Mchanganuo wa makusanyo hayo upo kwenye Kiambatisho Na I. Kadhalika Wizara ilitengewa jumla ya sh. 18,786,123,491/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, fedha hizo zilijumuisha mishahara ya Wizara sh. 2,204,370,168/= na ya Taasisi sh. 5,322,056,000/=. Matumizi Mengineyo (*OC*) ya Wizara sh. 7,017,626,323/= na ya Taasisi sh. 4,242,071,000/=. Hadi kufikia mwezi Juni, 2011, jumla ya sh. 17,993,171,000/= zilikuwa zimetolewa na kutumika. Mchanganuo wa matumizi kwa kila Idara upo katika Kiambatisho Na. II.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2010/2011 Wizara ilitengewa jumla ya shilingi 7,982,562,000 fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza Miradi kumi na moja ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Juni 2011, shilingi 5,600,000,000 zilikuwa zimetolewa na kutumika. Mchanganuo wa matumizi kwa kila Mradi upo katika Kiambatisho Na III.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2010/2011, Wizara ilitengewa jumla ya sh. 7,982,562,000/= fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza Miradi kumi na moja ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Juni, 2011, Sh. 5,600,000,000/= zilikuwa zimetolewa na kutumika. Mchanganuo wa matumizi kwa kila Mradi upo katika Kiambatisho Na. III.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sekta ya habari. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara ilitoa mafunzo ya kuwajengea uwezo maafisa habari wapatao 150 kutoka katika Vitengo vya Habari vya Wizara mbalimbali, Idara, Wakala, Taasisi za Umma, Mashirika ya Umma, Mikoa, Majiji, Miji na Halmashauri za Wilaya. Hivi sasa, Wizara inaendelea na mchakato wa kukamilisha Sera mpya ya Habari na ukamilishaji wa rasimu ya mapendekezo ya kutunga Sheria ya Kusimamia Vyombo vya Habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Idara ya Habari imefanikiwa kukusanya taarifa mbalimbali za Serikali, kuandika habari na kuzitoa katika vyombo vya habari, kupiga picha za matukio mbalimbali ya Kitaifa, kuzitoa katika magazeti na kuzihifadhi katika maktaba ya kumbukumbu ya picha kwa njia ya elektroniki. Aidha, Wizara imeboresha uchapishaji wa jarida la Nchi Yetu na kuhakikisha linachapishwa kwa wakati uliopangwa. Matoleo mawili yenye nakala 8,000 za jarida hili yamechapishwa na kusambazwa. Kadhalika Wizara imechapisha bango la Baraza la Mawaziri linalowatambulisha kwa wananchi Mawaziri na Naibu Mawaziri na Wizara wanazoziongoza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tovuti ya wananchi imeanzishwa na Serikali ili kuhakikisha kuwa wananchi wanapata haki yao ya kikatiba ya kutoa maoni kwa uhuru katika masuala yanayowahusu. Tovuti imewawezesha wananchi kuwa na mawasiliano ya moja kwa moja na Serikali. Changamoto iliyopo kwa sasa ni kuhakikisha kwamba hoja za wananchi zinajibowi kwa wakati na kwa ufasaha ili kutatua matatizo yanayowakabili. Wizara inaendelea kuzihamasisha Wizara nyingine, Idara zinazojitegemea, Taasisi na wadau wengine ili kujibu hoja zote zinazotolewa na wananchi kwa muda muafaka. Kwa kipindi cha mwaka ulioanza mwezi Julai, 2010 hadi Juni, 2011 jumla ya hoja 11,934 zimepokelewa kupitia Tovuti ya wananchi na kujibowi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuna uelewa mzuri wa matumizi ya Tovuti ya Wananchi, Wizara imetoa mafunzo juu ya tovuti hiyo kwa watendaji waandamizi wa Wizara mbalimbali, Idara na Wakala. Aidha, ili kuhakikisha kuwa kumbukumbu za matukio mbalimbali ya Kitaifa zilizohifadhiwa tangu mwaka 1948 katika mfumo wa picha na *negatives* hazipotei, Wizara ilianzisha mradi wa maktaba ya picha ili kuhifadhi picha zote kwa njia ya digitali. Jumla ya picha 2,500,000 zilizokuwepo zimehifadhiwa kwa teknolojia hiyo. Hivi sasa picha zote zinazopigwa kwa kutumia kamera za kisasa za digitali zinaendelea kuingizwa katika maktaba hiyo.

Aidha, Wizara imeanza mchakato wa kuanzisha mtandao wa kulinda na kuuza picha popote duniani kupitia *internet, e-commerce project*. Utaratibu huu utahakikisha kuwa picha za kumbukumbu za Kitaifa na Kimataifa zinapatikana kwa urahisi mahali popote duniani lakini hazichukuliwi kwa njia ya mtandao bila idhini ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha upatikanaji wa habari na picha Wizara imetoea jumla ya vibali 111 vya kuandika habari na kupiga picha. Kati ya vibali hivyo 102 ni vya waandishi kutoka nje na tisa ni wa ndani na vitambulisho (*press cards*) 400 vya waandishi wa habari vimetolewa kwa wanataaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendeleza uhuru wa upatikanaji wa habari na vyombo vya habari, Wizara imeendelea na usajili wa magazeti na majarida. Hadi Juni, 2011 jumla ya magazeti na majarida 711 yalikuwa yamesajiliwa yakiwemo yale ya kila siku na ya kila wiki. Usajili wa magazeti kwa mwaka 2010/2011, ulikuwa mdogo kutokana na Serikali kusitisha usajili huo kwa muda ili kupitia upya taratibu za usajili.

Aidha, katika kipindi hicho gazeti moja lilitutwa kutoka katika kitabu cha Msajili kutokana na kwenda kinyume na masharti ya usajili na maadili ya uandishi. Magazeti mengine nane yaliyokiuka maadili ya uandishi wa habari yalipewa onyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa utangazaji kuna vituo 70 vya radio vilivyoandikishwa na 26 vya televisheni. Vituo vingine saba vinatoa huduma ya kupokea matangazo ya vituo vya nje vya televisheni (*Cable pay TV*) na kuwauzia wananchi. Aidha, Shirika la Utangazaji Tanzania (*TBC*) limetimiza miaka mitatu tangu liliopbadilishwa na kuzinduliwa rasmi tarehe 26 Machi, 2008 na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete. Kuanzia kipindi hicho, Shirika limejitatihidi kutimiza malengo yake kwa kupanua usikivu wake ili uweze kuwafikia wananchi nchini kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kushirikiana na uongozi wa Serikali Mikoani, *TBC* imepata maeneo na kujenga vyumba vya kufunga mitambo ya *FM* katika Mikoa ya Shinyanga, Manyara, Kilimanjaro, Morogoro, Iringa, Rukwa, Mtwara na Ruvuma. Shirika limenunua mitambo ya *FM* 18 yenye uwezo wa *kilowatt* mbili ambayo imefikishwa kwenye vituo vya Shinyanga, Babati, Moshi, Morogoro, Iringa, Mpanda, Newala, Songea na Tunduru. Kila kituo kina mitambo ya *transmitters* mbili, moja kwa ajili ya matangazo ya *TBC<sub>Taifa</sub>* na nyingine kwa ajili ya *TBC<sub>FM</sub>*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufungaji wa mitambo hiyo katika Mikoa ya Morogoro, Iringa, Kilimanjaro na Manyara umekamilika. Kuanzia Novemba, 2010 vituo vya Morogoro, Iringa, Moshi na Babati vimeanza kurusha matangazo. Mchakato wa kufunga mitambo kwa vituo vya Newala, Tunduru, Songea, Mpanda na Shinyanga umeanza mwezi Mei, 2011 na unatarajiwa kukamilika hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Magazeti ya Serikali, (*TSN*) inayochapisha magazeti ya *Daily News*, *Sunday News* na HabariLeo inaijiendesha kwa faida bila kutegemea ruzuku kutoka Serikalini. Tangu mwaka 2004 Kampuni imekuwa ikitoa gawio kwa Serikali kupitia Hazina. Kampuni ya Magazeti ya Serikali imeendelea na mchakato wa kuzalisha magazeti na kufunga mashine ya pili ya kompyuta (*CTP*) ili kuongeza uwezo wa kuchapa magazeti. Kampuni pia imekamilisha ununuvi wa majengo kwa ajili ya mtambo wa uchapaji na imekabidhiwa hati ya umiliki wa majengo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati wa jengo la ofisi lilioko Barabara ya Mandela Jijini, Dar es Salaam unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2011. Kampuni ya *TSN* imeendelea na harakati za kutafuta wabia wa kuendeleza viwanja vya kampuni vilivypo Dar es Salaam na Dodoma. Amepatikana mbia wa uhakika ambaye ameonyesha nia ya kuendeleza kiwanja cha Dodoma. Kampuni pia imetoea mwaliko na imetangaza kwa wabia wengine watakaohusika na uendelezaji wa viwanja viwili vya Dar es Salaam. Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Kampuni imekamilisha na kuzindua maktaba ya Elektroniki. Aidha, taratibu za kuzindua huduma ya picha zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendeleza Sekta ya Habari, Wizara inashirikiana kwa karibu na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, (*TCRA*) katika kusajili na kutoa leseni kwa vituo vya radio na televisheni nchini. Pamoja na kutoa leseni kwa vituo vya radio na televisheni, *TCRA* kupitia Kamati ya Maudhui inaratibu utendaji wa vituo hivyo na kuhakikisha kuwa vyote vinazingatia maadili

yaliyoainishwa katika Sera ya Utangazaji ya mwaka 2003, Sheria ya Bunge namba (3) ya mwaka 2010 pamoja na Kanuni za Utangazaji za mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/11, Kamati ilishughulikia malalamiko ya ukiukwaji wa maadili ya utangazaji na kuhakikisha kuwa kanuni za utangazaji zinazingatiwa. Jumla ya malalamiko ya maudhui ya vipindi tisa (9) yalipokelewa. Kati ya hayo malalamiko nane yalishughulikiwa na lalamiko moja linaendelea kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wa vyombo vya Habari binafsi. Tangu mabadiliko ya sera za kiuchumi na kisasa ya miaka ya 90 kumekuwa na ukuaji mkubwa wa sekta ya habari nchini. Mabadiliko hayo yameshudua kuanzishwa kwa vyombo vingi vya habari binafsi, hususan magazeti. Hivi sasa Tanzania ni moja ya nchi chache Barani Afrika zenyenye idadi kubwa ya vyombo vya habari na uhuru mpana wa vyombo hivyo. Hali hiyo imechangia sana katika kukuza na kupanua uelewa wa wananchi wa mambo mbalimbali yanayohusu maisha na maendeleo yao. Watanzania wengi hivi sasa wana uelewa wa hali ya juu wa mambo yanayotokea hapa nchini na duniani kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhima ya vyombo vya habari duniani kote ni kuhabarisha, kuelimisha na kuburudisha. Wizara yangu ambayo ina dhamana ya kusimamia vyombo vya habari nchini itahakikisha kuwa dhima hiyo inatekelezwa kikamilifu kwa kuzingatia weledi na maadili ya taaluma ya habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa sababu hiyo Wizara imeamua kuimarisha utaratibu wa kuwasiliana na vyombo vya habari hususan vyombo vya habari binafsi na wadau mbalimbali wa habari kwa lengo la kuboresha utendaji wa vyombo hivyo ili viwahudumie wananchi kwa ufanisi zaidi. Katika hili, Wizara yangu imedhamiria kwa dhati kushirikiana na wadau wote wa habari katika kuweka mazingira endelevu yatakayowezesha kuwepo kwa ukuaji zaidi wa uhuru wa vyombo vya habari hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa sehemu kubwa ya vyombo vya habari nchini inamilikiwa na watu binafsi. Wizara yangu inatambua na kuthamini mchango mkubwa na muhimu wa vyombo hivi katika kutoa habari na taarifa mbalimbali kwa wananchi. Vyombo vya habari binafsi vinafanya kazi nzuri kwa Taifa letu ukiondoa kasoro ndogo ndogo zilizopo ambazo Wizara yangu inazifanya kazi kwa ushirikiano wa karibu na vyombo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mchango wake mkubwa katika maendeleo ya Taifa letu, vyombo vya habari vya binafsi pia vimekuwa tegemeo la ajira kwa wanahabari wengi vijana. Idadi kubwa ya vijana wanaohitimu mafunzo ya uandishi wa habari wanapata ajira kwenye vyombo hivyo, jambo ambalo limesaidia kwa kiwango fulani kupunguza tatizo la ajira mionganoni mwa vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kuhakikisha kwamba mafunzo ya uandishi wa habari yanaboreshwala ili kuwawezesha vijana wengi zaidi kupata ajira kwenye sekta hii muhimu. Tayari Wizara yangu imanzisha mazungumzo na Mfuko wa Habari Tanzania (*TMF*) kuhusu uwezekano wa Mfuko huo kufadhili mafunzo ya muda mrefu kwa baadhi ya waandishi wa habari wenye sifa stahiki.

Aidha, vyombo vya habari kwa ujumla wake vinaida Serikali katika kupata mrejesho kutoka kwa wananchi kuhusu sera na mipango ya maendeleo inayotekelizwa nchini. Kwa mfano, katika miaka ya karibuni tumeshuhudia jinsi vyombo vya habari vilivyokuwa katika mstari wa mbele kupiga vita dhana potofu kama vile mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi (*albino*) kwa shabaha za kupata utajiri; vikongwe kwa kuwatuhumu uchawi; unyanyapaa dhidi ya waathirika wa UKIMWI na watu wenye ulemavu pamoja na unyanyasajii wa kijinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi za Wanahabari zisizo za Kiserikali. Mionganoni mwa taasisi na vyombo vinavyosaidia katika kuboresha utendaji wa vyombo vya habari hapa nchini ni Baraza la Habari Tanzania (*MCT*), Jukwaa la Wahariri (*TEF*) na Chama cha Wamiliki wa Vyombo vya Habari (*MOAT*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Habari Tanzania limekuwa likifanya kazi kwa ushirikiano na Wizara yangu na tumekuwa tukishauriana katika mambo mbalimbali kwa manufaa ya taaluma ya habari. Hivi sasa Baraza, chini ya ushauri wa kitaalam wa *National Council for Technical Education (NACTE)* na udhamini wa *UNESCO* limekamilisha mtaala wa mafunzo ya uandishi wa habari kwa ngazi za 4 hadi 6 (level 4 – 6) ambazo ni ngazi za cheti (*basic certificate*), cheti cha juu (*advanced certificate*) na *diploma*. Mtaala huu utaviwezesha Vyuo vya Uandishi wa Habari ambavyo vimesajiliwa kuweza kupata ithibati ya *NACTE* na hivyo yeti vyake kutambuliwa rasmi. Wizara inafuutilia kwa karibu mchakato huu amba Serikali inaamini utasaidia kukuza kiwango cha taaluma ya habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inapenda pia kulipongeza Baraza la Habari kwa kazi nzuri linaloifanya ya kusikiliza malalamiko ya wananchi amba hawatendewi haki na baadhi ya vyombo vya habari. Baraza linafanya kazi hiyo nzuri licha ya kutokuwa na uwezo wa Kimahakama wa kutoa adhabu. Wizara itaendelea kushirikiana na Baraza katika utekelezaji wa jukumu lake hilo muhimu kwa manufaa ya wananchi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa maadili katika kuendeleza taaluma ya habari nchini, Wizara inashirikiana na Jukwaa la Wahariri na chama cha wamiliki wa vyombo vya Habari katika kuelimisha na kuhimiza waandishi wa habari kuzingatia maadili katika utendaji wao wa kazi. Jitihada hizi za ushirikiano tayari zimeanza kuzaa matunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini ya Wizara yangu kuwa juhud hizi za pamoja kati ya Serikali na wadau wote wa habari zitasaidia katika kuimarishe sekta ya habari ili iendelee kutoa mchango mkubwa katika kuharakisha maendeleo na ustawi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana umeendelea kuimarishe ikiwa ni pamoja na kutoa mikopo kwa vijana kupitia *SACCOS*. Mpaka kufikia mwezi Juni 2011, jumla ya *SACCOS* 242 zilikopeshwa Shilingi 1,210,000,000. Aidha, muda wa marejesho ya fedha, amba ni mwaka mmoja tangu *SACCOS* ilipokopeshwa, umekamilika. Mpaka sasa, jumla ya Shilingi 46,350,000 zimerejeshwa na *SACCOS* tisa (9) kutoka Halmashauri za Wilaya ya Muheza, Kilolo, Mbarali, Manispaa ya Lindi na *SACCOS* moja kutoka Manispaa ya Ilala. *SACCOS* zilizorejesha zitakopeshwa tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2010 zimeratibiwa na kukimbizwa katika Mikoa yote 26 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya kaulimbiu "Maliza Malaria, Malaria haikubaliki". Mbio hizo pia zilitumika kuwashamasisha wananchi na hasa vijana kushiriki katika shughuli za maendeleo hususan zile za kiuchumi, kupambana na maambukizi ya virusi vya UKIMWI, dawa za kulevyo, vitendo vya rushwa na ukatili dhidi ya binadamu na kuwashamasisha wananchi kujitokeza kupiga kura kwa amani wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani mwaka 2010. Kupitia mbio za Mwenge wa Uhuru, jumla ya miradi 1,393 yenye thamani ya shilingi 146,464,203,116.29 ilivekewa mawe ya msingi na mingine ilizinduliu wakati wa mbio hizo. Wizara inaendelea kuratibu maandalizi ya mbio za Mwenge kwa mwaka 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana kutoka sehemu mbalimbali za nchi yetu walishiriki katika Wiki ya Vijana, kilele cha mbio za Mwenge wa Uhuru na maonesho ya wajasiriamali na waelimishaji vijana yaliyofanyika katika viwanja vya Mwanga Mjini Kigoma. Jumla ya taasisi 176 za vijana na wadau mbalimbali walishiriki maonesho hayo yaliyoanza tarehe 8 hadi 13 Oktoba, 2010. Wakati wa maonesho ya Wiki ya Vijana wananchi walielimishwa masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na majukumu yanayotekelwa na Serikali na taasisi zake, wadau wa maendeleo na kupewa elimu ya ujasiriamali, afya ya uzazi na VVU/UKIMWI. Pamoja na maonesho hayo, jumla ya watu 936 walijitokeza kupima VVU, kati yao wanaume walikuwa 556 na wanawake walikuwa 380 ambapo watu 15 kati yao wanawake wanane (8) na wanaume saba (7) walikuwa wameambukizwa VVU, sawa na asilimia mbili ya watu walijitokeza kupima VVU.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za kuhakikisha vijana wetu wanapata stadi za maisha na kupambana na changamoto za utandawazi zinazowakabili, ikiwa ni pamoja na kuwapatia elimu sahihi ya afya ya uzazi na kukabiliana na VVU/UKIMWI, Wizara kwa kushirikiana na

Shirika la Idadi ya watu Duniani (*UNFPA*) imechapisha Mwongozo wa Stadi za Maisha kwa vijana kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Mwongozo huo utatumwa na waelimishaji rika, vijana na wadau mbalimbali katika kuwapatia Vijana stadi za maisha. Aidha Mwongozo huo umezinduliwa rasmi tarehe 25 Juni, mwaka 2011. Mafunzo ya awali yametolewa kwa Maofisa Vijana wa Wilaya na Mikoa juu ya matumizi sahihi ya mwongozo huo ili waweze kuutumia katika majukumu yao ya kuwaendeleza vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za Kitaifa na Kimataifa imeendelea kuwahamasisha na kuwahimiza wananchi juu ya umuhimu wa kushiriki katika shughuli za kujitolea. Aidha, siku ya kujitolea duniani imeadhimishwa Kitaifa Mkoani Dar es Salaam tarehe 5 Desemba, 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia, kwa kushirikiana na Taasisi za Vijana, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*) na wadau wa maendeleo ya Vijana, imeadhimisha siku ya Vijana Duniani sambamba na uzinduzi wa mwaka wa Vijana, iliyofanyika tarehe 12 Agosti, 2010 Mkoani Dar es Salaam ambapo vijana wapatao 200 kutoka asasi mbalimbali za vijana, Vyuo Vikuu na Taasisi nyingine za elimu walikutana na kujadili kwa pamoja utekelezaji wa Mpango wa Vijana Duniani uliopitishwa na Umoja wa Mataifa (*World Programme of Action for Youth*) na kuweka maazimio ya pamoja ya utekelezaji wa mpango huo kwa mwaka 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Japan kupitia Ubalozi wake hapa Nchini imeendeleza Mpango wa Vijana wa Meli (*Ship for the World Youth Program*), ambao huwakutanisha vijana kutoka nchi mbalimbali duniani na kujadili masuala mbalimbali ya kiuchumi na kijamii ndani ya Meli inayosafiri kwa takribani miezi mitatu. Katika programu hii, mwaka 2010/2011, vijana 11 kutoka Mikoa ya Morogoro, Manyara, Shinyanga, Kigoma, Dar es Salaam pamoja na Zanzibar waliungana na wenzao kutoka nchi zifuatazo:- Australia, Bahrain, Jamhuri ya Brazil, Chile, Jamhuri ya kisiwa cha Fiji, Japan, Mexico, "Oman", Kisiwa cha Solomon, na Jamhuri ya Vanuata. Shughuli hiyo ilianza mwezi Januari hadi Machi 2011, ambapo jumla ya vijana 274 walishiriki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) iliendelea kuratibu utekelezaji wa shughuli zilizo chini ya Kamisheni ya Afrika zinazolenga kukuza ujasiriamali kwa vijana. Halmashauri za Wilaya 12 za majoribio ya kukuza utamaduni wa ujasiriamali kwa vijana zilitewa. Aidha, vijana 50 wenye Shahada ya Kwanza waliteuliwa na kupewa mafunzo chini ya mpango huu na kupewa jukumu la kusimamia na kuratibu programu hiyo ya ujasiriamali katika Wilaya hizo 12. Wilaya hizo ni Lindi Mjini, Mtwara Vijiji, Bagamoyo, Handeni, Mpanda, Musoma Mjini, Rufiji, Singida Mjini, Manispaa ya Tabora, Unguja Kaskazini A, Micheweni na Urambo. Chini ya mpango huu Mfuko wa Kuwawezesha Vijana Wajasiriamali (*Youth to Youth Fund*) umeanza kazi ambapo vijana wajasiriamali walitangaziwa juu ya kutayarisha Andiko la Miradi (*Business Proposal*) na walioshinda kwa vigezo vilivyoewe kwa na mpango huu walipatiwa fedha za kuendesha shughuli zao za kiuchumi. Mpango huu ultenga shilingi 160,557,821.35 kwa lengo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Watoto Duniani (*UNICEF*) imefuatilia utendaji wa shughuli za maendeleo ya Vijana katika mitandao sita ya vijana walio nje ya shule (*Out of School Youth Network*) inayofadhiliwa na *UNICEF* katika Wilaya sita za mfano ambazo ni Makete, Temeke, Bagamoyo, Hai, Siha na Magu. Lengo ni kuhakikisha kuwa mitandao ya vijana inafanya shughuli zinazolenga maendeleo ya vijana kama ilivyoelekezwa katika Sera ya Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2010/2011, Wizara imeendelea na mchakato wa kufanya Maboresho ya Sera ya Utamaduni ya mwaka 1997 pamoja na Sheria Na.4 ya mwaka 1976 ya Bodi ya Ugaguzi wa Filamu na Michezo ya Jukwaani. Kadhalika imebioresha Sheria Na. 23 ya BASATA ya mwaka 1984 pamoja na kukamilisha Hati ya kuanzisha Mfuko wa Utamaduni Tanzania (*Trust Deed*) ya mwaka 1998. Aidha, Wizara imesimamia na kuendesha Tamasha la 29 la Sanaa na Utamaduni wa Mtanzania la Bagamoyo tarehe 27 Septemba hadi 2 Oktoba, 2010. Tamasha hili liliongozwa na kaulimbiu "Sanaa na Utamaduni

katika kukuza na kuimarisha Demokrasia". Vikundi mbalimbali vya fani za utamaduni vya ndani na nje ya nchi vilishiriki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeandaa na kurusha jumla ya vipindi 50 vya "Lugha ya Taifa", vipindi 49 vya "Kumepambazuka" katika redio na vipindi 52 vya "Ulimwengu wa Kiswahili" katika televisheni ambavyo vimesaidia wananchi kuelewa maana, matumizi na maendeleo ya Kiswahili. Wizara pia, ilianda Mikutano Mkuu wa Sekta ya Utamaduni uliofanyika Jijini Mwanza tarehe 12 hadi 17 Desemba, 2010 ulioshirikisha wadau 300. Mikutano huu uliongozwa na kaulimbiu "Sanaa ni Ajira, Tuithamini". Kadhalika Wizara iliratibu na kusimamia vikundi tisa (9) vya ngoma za asili viliviyoshiriki Maadhimisho ya sherehe za kitaifa pamoja na maadhimisho ya Siku ya Utamaduni Duniani, yaliyofanyika Mkoani Mara tarehe 19 hadi 21 Mei, 2011 ambapo vikundi 13 vilishiriki. Kimoja kilitoka katika kijiji cha Butiama kwa lengo la kumuenzi muasisi wa Taifa letu, hayati Baba wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imesimamia kazi ya ujenzi wa Jumba la Utamaduni eneo la Kiromo Mkoani Pwani na hadi sasa kibali cha kumiliki eneo hilo la ekari 100 kimepatikana, barabara inayounganisha barabara kuu ya Bagamoyo - Dar es Salaam na eneo la mradi imetengenezwa. Kadhalika, eneo la ekari 25 katika eneo la Mabwepande huko Bunju Mkoani Dar es Salaam, ambapo kitajengwa Kituo cha Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika limepatikana. Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika imetambulishwa kwa kufanya Mikutano na wadau watakaowezesha na kusaidia utekelezaji wake. Wadau hao ni viongozi wa ngazi za juu wakiwemo Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu wa Wizara zote za Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Watendaji Wakuu wa Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali za Serikali na zisizo za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wajibu wa Wizara kuimarisha, kukuza na kuendesha lugha yetu ya Kiswahili kwa ajili ya kurahisisha mawasiliano. Wajibu huo ni pamoja na kuratibu na kuhakikisha ustawi na maendeleo ya utumiaji wa Kiswahili kwa kushirkiana na asasi zinazohusika na uendelezaji wa lugha hii hapa nchini. Ili kusimamia na kufuatilia matumizi fasaha na sanifu ya lugha hii hapa nchini, Wizara inao wajibu wa kutoa ithibati ya vitabu vya kiada vinavyotungwa au kufasiriwa kwa Kiswahili kwa mahitaji ya shule na kwa watu binafsi ili kusimamia na kufuatilia matumizi fasaha na sanifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) limeratibu na kutoa huduma ya ukalimani wa Kiswahili kwenye Mikutano ya Umoja wa Afrika (AU) iliyofanyika Kampala, na Addis Ababa, Mikutano ya Bunge la Afrika iliyofanyika Midrand, Afrika Kusini mwezi Oktoba 2010 na Mei 2011. Vilevile lilitoa huduma ya kutafasiri hati mbalimbali zikiwemo hati za bidhaa zinazopitishwa bandarini, vyeti vya shule, ndoa, kuzaliwa na hati za talaka. Hali kadhalika Kitabu cha "Mwongozo kwa Waandishi wa Kiswahili Sanifu" kimefanyiwa marekebisho na kupelekwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu kupatiwa cheti cha ithibati ili kiweze kutumika katika shule za msingi, sekondari na vyuoni kama kitabu cha kiada. Aidha, makala ndefu zikiwemo Hotuba ya Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Kanuni za Uvuvi za Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, baadhi zimefasiriwa kutoka lugha ya Kiswahili kwenda Kiingereza na nytingine kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) liliundwa kwa Sheria ya Bunge Na. 23 ya mwaka 1984. Baraza liliipewa dhamana ya kuhimiza Maendeleo ya Sanaa za Muziki, Sanaa za Maonyesho, Picha Jongefu (filamu) na Sanaa za Ufundu. Pamoja na majukumu hayo Baraza limezindua Programu Maalum ya Jukwaa la Sanaa kwa lengo la kutoa habari za sanaa na utamaduni kwa wananchi. Jumla ya midahalo 41 ilifanyika iliyowashirikisha wasanii, wanahabari na wadau wa Sanaa na Utamaduni wapatao 4353. Kupitia Jukwaa la Sanaa, BASATA imeendesha makongamano yenye lengo la kutoa elimu ya maadili, umuhimu wa usajili, hakimiliki na vyama vya wasanii.

Mheshimiwa Naibu Spika, BASATA imefanya utafiti wa mchango wa sanaa katika kuongeza pato, ajira na kuondoa umaskini, katika Wilaya ya Dodoma, Kilaha, Kinondoni na Morogoro. Taarifa imeshatayarishwa na kukabidhiwa kwa menejimenti ya BASATA. Utafiti umebaini kwamba wasanii hujipatia kipato na ajira kupitia shughuli za sanaa. Baraza pia limetoa mafunzo ya stadi za

uchoraji na utambaji wa hadithi kwa watoto 200 wa shule nne (4) za msingi kutoka mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Michezo ya Kuigiza Jukwaani iliundwa kwa Sheria ya Bunge Na. 4 ya mwaka 1976 kwa lengo la kusimamia maadili katika tasnia ya filamu nchini, utoaji wa vibali vya utengenezaji wa filamu na leseni za kumbi za sinema. Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2010/2011, Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza Jukwaani imesambaza jumla ya nakala 150 za Kanuni na Sheria ya Filamu Na.4 ya mwaka 1976 kwa wadau mbalimbali. Bodi imeendesha semina kwa wasambazaji wa filamu ikishirikiana na Shirikisho la Filamu na Mkuutano Mkuu wa Sekta ya Utamaduni, pia imefahamisha wadau wengine kuhusu Sheria hii. Kazi nyingine zilizofanyika ni pamoja na kukamilisha marekebisho ya Sheria ya Filamu na Michezo ya Jukwaani na kuandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri, na baadaye kupata Sheria itakayolinda maadili ya Taifa kupitia tasnia ya filamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi imeandaa orodha ya filamu zinazotengenezwa nchini kwa lengo la kufahamu idadi ya filamu, maudhui, watengenezaji, wasambazaji na mapato yanayotokana na eneo hili. Kutokana na hatua hiyo, filamu 96 zilitengenezwa, nakala 66,800 zilizlishwa na wastani wa shillingi 1,226,500,000/= zilipatikana. Filamu 50 za *African Magic* ziliuzwa kwa takribani shillingi 57,765,000/= na nyingine kupelekwa Burundi, Kenya, Rwanda, Uganda, Jamhuri ya Demokrasia ya Congo, Zambia, Malawi, Madagascar, Nigeria, Italia, Australia, Marekani na Ufaransa. Bodi imekagua filamu 105 na Miswada ya Filamu 65 na kuiweka katika madaraja. Filamu 5 kati ya hizo zilipewa Daraja la R kwa maana ya kukataza filamu hizo kuoneshwa katika hadhara kwa kuwa zimekiuka maadili ya Kitanzania. Kadhalika imetoa vibali 53 vya utengenezaji wa filamu kwa watengenezaji wa filamu kutoka nje ya nchi. Bodi imeendelea kutoa ushauri kwa wadau wake ili kuinua viwango na kuboresha kazi zao kimaadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSuBa) ilianzishwa tarehe 2 Novemba, 2007 kwa Tangazo la Serikali Na. 220 kwa mujibu wa Sheria ya kuanzishwa kwa Wakala wa Serikali Na. 30 ya mwaka 1997. Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2010/2011, TaSuBa imeendesha mafunzo ya Stashahada kwa washiriki 122 na mafunzo ya muda mfupi kwa wasanii 80 walioko kazini. Aidha imekamilisha mitaala ya Shahada ya Kwanza kwa masomo ya Sanaa za Maonyesho na Sanaa za Ufundu. Pia, imekamilisha kuandaa mtaala wa mafunzo ya Cheti ya Uzalishaji na Usanifu wa Muziki. Mtaala huu utawasilishwa Baraza la Taifa la Mafunzo ya Ufundu ili kupata ithibati na kwamba TaSuBa inatarajia kuanza kutoa mafunzo hayo mwaka wa masomo wa 2011/12.

Mheshimiwa Naibu Spika, TaSuBa imeendeleza ushirikiano na washirika wake, kikiwemo Chuo Kikuu cha Stavanger na Shule ya Utamaduni ya Stavanger ya Norway chini ya mradi wa Norway Tanzania (*NOTA*). Awamu ya pili ya mradi huu ilikwisha mwezi Juni 2011. Hata hivyo, Taasisi imeandaa andiko la mradi wa *NOTA* awamu ya tatu. Andiko hili litawasilishwa kwa Serikali ya Norway ambaa ni wahisani wa mradi huu. Taasisi iliendesha Tamasha la Sanaa la 29 la Bagamoyo, liliofanyika tarehe 27 Septemba, hadi tarehe 2 Oktoba, 2010 na kaulimbiu yake ilikuwa 'Sanaa na Utamaduni katika kukuza na kuimarisha Demokrasia'.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Utamaduni Tanzania ni chombo ambacho kilianzishwa na Serikali ikishirikiana na Wahisani wa nje ili kusaidia vikundi vya wasanii vyenye miradi ya maendeleo. Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2010/2011, Mfuko umeendeleza vituo vya utamaduni na masoko katika Mikoa ya Dodoma na Morogoro kwa kulipia ada za viwanja na kuanza maandalizi ya utengenezaji wa sehemu za kufanya maonyesho wakati wa Maadhisho ya Nane Nane. Kadhalika, Mfuko umeendeleza viwanda vidogovidogo asilia vya nguo katika Mikoa ya Tanga, Singida, Ruvuma na Pemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara kuitia Idara ya Maendeleo ya Michezo imeboresha Uwanja wa Uhuru uliopo Dar es Salaam kwa kuweka viti vya kukaa watazamaji 20,000. Ukarabati huo unaendelea. Kadhalika, Wizara iligharamia ushiriki wa timu za Taifa zenye wachezaji 30 na viongozi 13 wa michezo ya Riadha, Kuogelea, Mpira wa Meza, Ngumi katika Michezo ya Jumuuya ya Madola iliyo fanyika huko India. Aidha, ilishiriki katika mikutano ya kimataifa ya kujenga uwezo na mahusiano ya kimichezo Kimataifa. Washiriki wakuu

wakiwa ni Baraza Kuu la Michezo Barani Afrika, TAFISA CABOS na Jumuiya ya Madola. Pia, Wizara imetoa huduma mbalimbali kwa makocha wageni wa michezo ya Riadha, Ngumi, Netiboli, Judo na Mpira wa Miguu kwa lengo la kuinua viwango vya michezo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imefanya kazi ya kudurusu Katiba za Vyama vya Michezo 55 na kusajili vyama, vituo na vilabu vya michezo 299. Kutoa huduma ya tiba na kinga na upimaji wa wachezaji wa michezo ya mpira wa miguu, ngumi za ridhaa, netiboli, mpira wa mikono na mpira wa kikapu. Kadhalika, imeendelea kutoa huduma ya ushauri kwa wadau kuhusu masuala mbalimbali ya michezo, kujenga bweni la wanafunzi lenye uwezo wa kulala wanafunzi 64 na kuweka umeme wa gridi ya Taifa katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo kilichoko Malya Mkoani Mwanza. Wizara imeendelea kutoa mafunzo ya Stashahada ya ufundishaji Michezo na Stashahada ya Uongozi wa Michezo katika Chuo hiki. Pia imeendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi ya uongozi na utawala katika michezo, ufundishaji na uamuzi katika vituo vya michezo vya Kanda ya Arusha, Songea na Dar es Salaam ambapo jumla ya wataalamu na Walimu wa michezo 230 walipata mafunzo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea na zoezi la kuwapandisha vyeo watumishi wanaostahili kulingana na miundo ya utumishi ya kada zaao na kwa kuzingatia Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya mwaka 1999 na 2008. Katika mwaka wa 2010/2011, watumishi 47 walipandishwa vyeo, watumishi 12 walithibitishwa kazini na watumishi 13 walajiriwa katika nafasi mbalimbali kupitia Sekretarieti ya Ajira. Aidha, Wizara imewezesha kutoa mafunzo kwa Watumishi 49, katika ya hao 39 wamepata mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi na watumishi 10 wanahudhuria mafunzo ya muda mrefu ndani ya nchi. Katika mwaka 2010/2011, Wizara imekamilisha uandaaji wa Miundo ya Utumishi ya Kada za Maofisa Habari, Utamaduni na Michezo. Miundo hii imezingatia matakwa na mahitaji ya watumishi hawa ndani ya Wizara na Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa. Miundo hii tayari imewasilishwa katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ambayo kupitia Baraza Kuu la Utumishi Serikalini itairidhia ili ianze kutumiwa na Mamlaka za Ajira nilizozitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha Utawala Bora na ushirikishwaji wa Wafanyakazi Sehemu za kazi, Wizara imekuwa ikifanya vikao vya Baraza la Wafanyakazi ili kuweza kutatua kero mbalimbali zinazowakabili watumishi wa Wizara. Aidha, Wizara imehakikisha kwamba Watumishi wapya waliojingga na Utumishi wa Umma kwa mara ya kwanza wanapewa mafunzo elekezi ambayo lengo lake ni kuwapa mwelekeo wa utendaji katika Serikali ikiwemo kuwafahamisha matarajio ya mwajiri, taratibu za utumishi na Maadili katika Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha kuwa rasilimali za Wizara zinatumika vizuri na kwa madhumuni yaliyowekwa, Wizara imeendelea kutumia Kamati ya Kuratibu, Kusimamia na Kudhibiti Mapato na Matumizi ya Serikali pamoja na Kamati ya Ukaguzi ya Wizara kuhakikisha kunakuwepo matumizi sahihi ya fedha zilizotengwa kutekeleza shughuli mbalimbali. Aidha, Wizara imeendelea kusimamia kwa ukamilifu utekelezaji wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2001 kama ilivyorekebishwa mwaka 2004 pamoja na Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2001 kwa lengo la kupunguza mianya ya rushwa na kutoa huduma zenye viwango vinavyokubalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Habari, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Wizara itatekeleza yafuatayo:-

- Kukusanya maoni ya wananchi kupitia Tovuti ya Wananchi na kufuatilia ili kuona hoja hizo zinapatiwa majibu stahiki.
- Kuratibu shughuli za Vitengo vya Habari, Elimu na Mawasiliano, kutoa mafunzo ya utoaji habari za Serikali kwa maofisa habari wa vitengo hivyo katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi za Umma, Mashirika ya Umma na Serikali za Mitaa.
- Kuendeleza mipango na mchakato wa kuanzisha mtandao wa kujinda na kuza picha popote duniani kupitia mradi wa "e-commerce". Mtandao huo utawawezesha wadau kupata picha hizi popote walipo kwa gharama nafuu kutoka katika maktaba ya picha lakini pia utalinda picha hizo zisilbiwe.

- Kutafuta na kuanzisha sehemu nyingine rje ya maktaba ya picha ya Dar es Salaam ambapo picha zilizohifadhiwa katika CD zitaweza kuhifadhiwa ili kuepuka uwezekano wa kupoteza kumbukumbu hizo endapo litatokea janga lolote kama moto katika maktaba ya picha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) pamoja na shughuli zake za kawaida limejpanga kuweka mfumo bora zaidi wa kudhibiti matangazo na kununua jenereta la kituo cha Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya utekelezaji ya mwaka 2011/2012, kwa upande wa Kampuni ya Magazeti ya Serikali ni kuimarishta na kuongeza ubora wa magazeti na kupanua usambazaji Mikoani. Kadhalika, kuanzisha Gazeti la Kiswahili la Michezo na kutafuta fedha za ununuzi wa mashine za kuchapa vitabu, kalenda na vipeperushi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya maendeleo ya vijana. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kuratibu Mbio za Mwenge wa Uhuru na Wiki ya Vijana.
- Kufuatilia marejesho ya fedha walizokopeshwa Vijana kuititia *SACCOS* na kuendelea kuwawezesha Vijana kiuchumi kuititia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana chini ya utaratibu wa *SACCOS* za Vijana.
- Kuchapisha na kusambaza mkakati wa ushiriki na ushirikishwaji wa Vijana katika shughuli za maendeleo ya kijamii.
- Kuendeleza ushirikiano baina ya Wizara, Taasisi za Serikali na Jumuiya za Kikanda na zile za Kimataifa, pia kuwesheza vijana na watendaji wa masuala ya vijana kushiriki na kutekeleza mikakati ya Jumuiya za Kimataifa ya maendeleo ya vijana.
- Kuendelea kuwashamasisha vijana kuunda vikundi vyta pamoja vya kuzalisha mali, kuwashauri na kuwaelekeza jinsi ya kusajili taasisi na vikundi vyao na kuzishawishi taasisi za kifedha na mamlaka nyingine kutoa huduma rafiki kwa vijana zinazolenga ustawi wa vijana kiuchumi.
- Kuendelea kuwashimiza vijana na wananchi kwa ujumla kushiriki katika shughuli za kujitolea katika maeneo yao.
- Kuendelea na mpango wa kuwawezesha waelimishaji rika juu ya Mwongozo mpya wa Stadi za Maisha kwa Vijana kwa lengo la kufahamu matumizi yake na kisha kuutumia katika shughuli zao za kila siku za utoaji wa elimu kwa vijana.
- Kuendelea na kazi ya ukarabati wa Vituo vya Vijana vya Ilonga- Kilosa, Sasanda-Mbozi na Marangu- Moshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya maendeleo ya utamaduni. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara itatekeleza yafuatayo:-

- Kuhifadhi na kusambaza matokeo ya utafiti na kuchapisha vijarida vya mila na desturi.
- Kuendesha utafiti wa mila na desturi katika jamii 20.
- Kuandaa na kurusha vipindi 52 vya radio na runinga vya Maadili ya Mtanzania.
- Kuratibu na kuendesha Mpango wa kuibua vipaji kwa watoto wa shule za msingi katika fani mbalimbali.
- Kusimamia na kuratibu vikundi vya ngoma za asili vinavyoshiriki katika Maadhisho ya Sherehe za Kitaifa.

- Kusimamia usambazaji wa machapisho, majarida na vitabu vya Kiswahili katika vituo vya utamaduni vya ofisi za ubalozi wa Tanzania zilizoko nje ya nchi pamoja na kutathmini ufundishaji wa Kiswahili katika vituo hivyo.
- Kufanya utafiti wa lugha za asili katika jamii 12 nchini.
- Kuendesha mafunzo ya lugha ya Kiswahili sanifu kwa Waandishi na Wahariri wa Vyombo vya Habari na kuendesha maonyesho ya machapisho ya lugha ya Kiswahili Kitaifa na Kimataifa.
- Kuratibu na kusimamia maadhisho ya siku ya Utamaduni Duniani.
- Kusimamia na kuendesha Mpango wa Kudumu wa Utamaduni katika kanda sita za Utamaduni.
- Kusimamia na kuendesha Tamasha la 30 la Sanaa na Utamaduni wa Mtanzania litakalofanyika huko Bagamoyo.
- Kusimamia ujenzi wa Jumba la Utamaduni eneo la Kiromo, Mkoa wa Pwani. Kushughulikia umilikishwaji wa eneo kitakapojengwa Kituo cha Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika na kuandaa vikao vya Kamati ya uongozi vitakavyopitia na kujadili utekelezaji wa mchakato wa ujenzi.
- Kukusanya taarifa muhimu zinazohusu Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika kwa kushirikiana na Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) limepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- Kuandaa na kurusha vipindi 52 vya "Lugha ya Taifa", vipindi 52 vya "Kumepambazuka" katika radio na vipindi 52 vya "Ulimwengu wa Kiswahili" katika televisheni.
- Kuendelea kusoma Miswada ya vitabu vya taaluma na kuipatia ithibati ya lugha.
- Kuratibu na kutoa huduma ya tafsiri na ukalmani katika mikutano ya kitaifa na kimataifa na shughuli za Mashirika, makampuni na watu binafsi.
- Kuendelea kuchunguza makosa ya Kiswahili yanayofanywa na vyombo vya habari na watumiaji wengine na kusambaza masahihisho yake.
- Kukarabati na kuboresha baadhi ya majengo ya NIC yaliyopo Kijitonyama, Dar es Salaam, yalyonunuliwa ili yaweze kukidhi mahitaji ya kiofisi ili Balaza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) lihamie katika majengo hayo na kuyatumia kama ofisi zake mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, BASATA imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- Kuratibu midahalo 52 kuitia Jukwaa la Sanaa kwa Wasanii, Waandishi wa Habari na Wadau wa Sanaa 3,600.
- Kuendesha mafunzo ya Sanaa kwa Walimu 100 katika Wilaya mbili za Mkoa wa Morogoro kuhusu utambaji wa hadithi na uchoraji.
- Kuratibu chaguzi za viongozi wa mashirikisho manne ya Sanaa.
- Kuandaa mukutano wa wahisani wa utunishaji Mfuko kwa ajili ya kutekeleza Mpango Mkakati wa Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA) wa mwaka 2011 hadi 2014.

- Kuandaa onyesho moja la sarakasi kwa kushirikisha wasanii wa ndani na nje ya nchi kwa lengo la kutunisha mfuko kwa ajili ya utekelezaji Mpango Mkakati wa BASATA.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 Bodi ya Filamu imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- Kupitia Miswada 240 ya Filamu na kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu maboresho ya filamu na uzingatiaji wa maadili.
- Kukagua filamu 240, kutoa ushauri wa maboresho ya filamu hizo na kuona kama maadili yamezingatiwa, pia kuhakikisha filamu hizo zinakidhi viwango vyta kuingia sokoni na kupanga filamu hizo katika madaraja.
- Kuhakikisha kwamba filamu zinazotengenezwa zinazingatia maadili ya Kitanzania, zinatangaza Taifa na zinazingatia Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza Jukwaani Na. 4 ya mwaka 1976 na Kanuni zake.
- Kutoa vibali 60 vyta kutengeneza filamu kwa watengenezaji wa filamu wa nje na ndani ya nchi.
- Kutoa vibali saba (7) vyta uzinduzi na matamasha ya filamu.
- Kutoa vibali vitano (5) vyta wasanii wa filamu kutoka nje ya nchi wanaokuja kushirikiana na watengeneza filamu wa nchini.
- Kuandaa Tamasha la Filamu za Kitanzania kwa kushirikiana na Shirikisho la Filamu.
- Kutoa leseni za uendeshaji kumbi za maonyesho ya filamu.
- Kuendelea na zoezi la kuandaa orodha ya filamu zinazotengenezwa nchini kwa lengo la kufahamu idadi ya filamu, maudhui, watengenezaji, wasambazaji, mapato na idadi ya filamu zinazouzwa nje ya nchi.
- Kuendelea na ukusanyaji wa takwimu za Tasnia ya Filamu nchini ili kuwajua na kuwatambua watunzi wa filamu, watengenezaji, wasambazaji, waqizaji, wapiga picha, mapromota na vibanda visivyo rasmi ili kudhibiti kuzagaa kwa filamu zinazokiuka maadili ya Kitanzania.
- Kuweka alama kwenye filamu zote zilizokaguliwa.
- Kutoa vitambulisho kwa wasambazaji wa filamu, vitambulisho hivyo vitakuwa vikihuishwa kila mwaka.
- Kusambaza vipeperushi 3,000 na kanuni kwa wadau nchini kote ili kuitangaza Bodi ya Filamu, kutambulisha wajibu wake na kuifahamisha jamii maadili ya Taifa.
- Kukamilisha marekebisho ya Sheria ya Filamu, lengo likiwa ni kupata Sheria itakayoendana na wakati na hivyo kuendelea kulinda maadili ya Taifa katika tasnia ya filamu.
- Kuimarisha Bodi za Wilaya na kutafuta fursa ya kuwapa semina elekezi.
- Kufanya operesheni ya filamu zote zisizokaguliwa mara Kanuni za Sheria ya Filamu zitakapotangazwa katika Gazeti la Serikali.
- Kusimamia mapato yatokanayo na tasnia ya filamu ili kuongeza pato la Taifa, pato la msanii na kuhakikisha mapato yote yanayotokana na filamu yanafika Serikalini.

- Kutoa taarifa katika magazeti kuhusu filamu zote zilizopitishwa, zilizokatazwa na madaraja zilizopatiwa.
- Kuimarisha Sekretarieti ya Bodi kwa kuongeza wataalamu na kutafuta fursa za masomo ya muda mrefu na mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, TaSUBa imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- Kuendesha mafunzo ya Stashahada kwa washiriki 120 na mafunzo ya muda mfupi kwa wasanii 150 walio kazini.
- Kukamilisha Mtaala wa shahada ya kwanza ya Sanaa za Maonyesho na Sanaa za Ufundu.
- Kuendesha Tamasha la 30 la Bagamoyo la Sanaa na Utamaduni.
- Kuimarisha mafunzo ya cheti katika fani ya uzalishaji na usanifu wa muziki kwa washiriki 30.
- Kujenga jengo la utawala ikiwa ni sehemu ya mpango kabambe wa TaSUBa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Mfuko wa Utamaduni umepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- Kuendeleza tasnia ya utamaduni katika utaalamu asilia wa usukaji kwa akina mama waishio vijiji ni katika Mikoa ya Tanga, Iringa na Dodoma.
- Uendelezaji wa Vituo vya Utamaduni na Masoko katika Mikoa ya Dodoma na Morogoro.
- Kuendeleza tasnia ya utamaduni katika utaalamu asilia wa nguo kwenye Mikoa ya Singida na Ruvuma pamoja na Visiwa vya Pemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya maendeleo ya michezo. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara itatekeleza kazi zifuatazo:-

- Kuendelea na jitihada za kutafuta fedha kwa ajili ya uendelezaji wa awamu ya pili ya Ujenzi wa eneo Changamani la Michezo lilitoko Jijini Dar es Salaam.
- Kuanzisha mfumo maalum wa Kitaifa wa kutathmini sifa na kutoa madaraja ya Walimu wa Michezo mbalimbali kwa ushirikiano na Vyama vya Michezo vya Kitaifa na *UK-Sport International*.
- Kuratibu maandalizi na kuwezesha timu za taifa kushiriki katika michezo ya nchi za Afrika itakayofanyika nchini Msumbiji mwezi Septemba, 2011.
- Kuendesha mafunzo ya Stashahada ya Elimu ya ufundishaji michezo, Stashahada ya Uongozi na Utawala wa Michezo kwa wanachuo wa Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya.
- Kutoa mafunzo ya muda mfupi ya fani mbalimbali za michezo kwa washiriki katika vituo vya michezo Kanda ya Kaskazini (Arusha) na Kanda ya Kusini (Songea).
- Kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu miundombinu na vifaa bora vya michezo kwa wamiliki, mameneja wa viwanja na wadau wengine.
- Kuimarisha huduma za Kinga na Tiba kwa wanamichezo kwa kupima afya, kuendesha kliniki za wazi na kuendesha mafunzo ya Kimataifa jijini Dar es Salaam na Arusha.

- Kuhamasisha mamlaka mbalimbali kujenga viwanja vya michezo kama vitega uchumi vya mamlaka hizo na kuboresha viwanja vilivyopo.

- Kuendelea kusajili Vyama na Vilabu vya Michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Baraza la Michezo la Taifa (BMT) litatekeleza kazi zifuatazo :-

- Kushirikiana na Halmashauri za Manispaa, Miji na Wilaya kuhamasisha na kuendesha matamasha ya michezo kwa jamii.
- Kuanzisha na kuendesha mafunzo ya ufundishaji michezo kwa viongozi vijana kwa ushirikiano na vyama vya Michezo vya Taifa na *UK-Sport International*.
- Kuendesha mafunzo ya muda mfupi ya ufundishaji kwa Walimu wa Michezo wapatao 500 katika Wilaya 10 za Tanzania Bara.
- Kuandaa, Kusimamia na kuendesha mafunzo ya Uongozi kwa Vijana kuitia michezo kwa washiriki wapatao 1,200 na pia kuwashirikisha katika mabonanza wanafunzi wapatao 2,000 wa shule za Msingi na Sekondari.
- Kuanzisha mpango maalum wa mafunzo ya Uongozi wa Michezo kwa Wanawake.
- Kuendesha mafunzo ya Utawala Bora, kwa Viongozi wa vyama vya Michezo vya Taifa kwa lengo la kuongeza ufanisi na kuongeza tija katika Sekta ya Michezo.
- Kujenga uwezo wa Wafanyakazi wa Baraza la Michezo la Taifa na vyama vya Michezo vya Taifa kwa kuwaandalia mafunzo ya kulingana na mahitaji yaliyopo.
- Kukamilisha marekebisho ya Sheria Na.12 ya Baraza ya mwaka 1967 na marekebisho yake Na.6 ya mwaka 1971.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Utawala na Rasilimali Watu. Katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Wizara imekusudia kutekeleza yafuatayo:-

- Kufanya mapitio ya mahitaji ya mafunzo kwa watumishi (*Training Needs Assessment*).
- Kuandaa na kutekeleza mpango wa mafunzo utakaojumuisha mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi kwa watumishi wa Wizara.
- Kupandisha vyeo watumishi wa Wizara walio na sifa kwa mujibu wa Nyaraka za Maendeleo ya Utumishi wa Umma.
- Kuelimisha Watumishi kuhusu rushwa na maadili sehemu za kazi na kutoa mafunzo kwa wajumbe wa Kamati ya Maadili ya Wizara.
- Kufanya mafunzo ya mpango wa maendeleo ya rasilimali watu na maandalizi ya mfumo wa taarifa za kiutumishi na mshahara (*Human Capital Management Information system – HCmis*).
- Kuendesha kampeni ya ushauri nasaha na kupima Virus vya UKIMM kwa hiari na kutoa huduma ya lishe na madawa kwa watumishi walioathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Sera na Mipango. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012 Wizara litatekeleza yafuatayo:-

- Kuratibu na kukamilisha mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Michezo ya mwaka 1995 pamoja na Sheria za BAKITA, BASATA, Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza Jukwaani na Baraza la Michezo la Taifa.

- Kufanya tathmini na ufuatilaji wa miradi mbalimbali ya Maendeleo inayotekelizwa Wizarani, na kusimamia utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Miaka Mitatu (2010/2011 – 2012/2013).
- Kuratibu masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yanayohusu sekta za Wizara, pamoja na kubaini fursa za ushirikiano wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, Serikali itaendeleza mafanikio yaliyopatikana katika Sekta zinazosimamiwa na Wizara ili ziweze kuchangia zaidi katika maendeleo ya nchi yetu. Matarajio ya Serikali ni kuona kuwa Sekta za Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo zina nafasi muhimu katika kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Uchangiaji ambaao ni pamoja na kuongeza ajira, kipato, kulinda mazingira, kuleta amani na furaha katika jamii. Katika kutumia fursa hizo bado kuna changamoto ambazo zinahitaji zipatiwe ufumbuzi ili kuzitumia ipasavyo katika kuleta maendeleo ya nchi. Matarajio yangu ni kwamba changamoto zilizopo zitaendelea kupatiwa ufumbuzi hatua kwa hatua hasa kwa kushirikiana na sekta binafsi kupitia mfumo wa "*Public-Private-Partnership*" (PPP) na wadau wengine wa maendeleo. Tukidhamiria inawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani, kwa niaba ya Serikali na kwa niaba yangu, naomba kuwashukuru kwa dhati wale wote walioshirikiana nasi katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2010/2011, katika kutimiza malengo yetu. Mafanikio ya utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara umewezekana kutokana na ushirikiano uliopo mionganoni mwa viongozi na wafanyakazi wa Wizara na wadau wengine walio nje ya Wizara. Shukrani zangu za pekee ziende kwa Mheshimiwa Dkt. Fenella E. Mukangara, (Mb), Naibu Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ambaye amekuwa msaada mkubwa kwangu, Bwana Sethi Kamuhanda, Katibu Mkuu, Bibi Sihaba Nkinga, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Wataalamu na Watumishi wote wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo pamoja na Asasi zilizo chini ya Wizara kwa juhudi walizofanya kuhakikisha kwamba wanatimiza ipasavyo majukumu tuliyokabidhiwa na Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru wale wote walioshiriki katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Aidha, nawashukuru wahisani wote ambaao wametusaidia na naamini kuwa wataendelea kutusaidia. Siyo rahisi kuwataja wote lakini nitaje wachache ambaao wanaendelea kutusaidia wakiwemo Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, Finland, Uingereza, Denmark, Japan, Sweden, Norway na Ujeruman; Pia Mashirika ya kimataifa ya UNESCO na UNICEF. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru vyombo vyote vya habari nchini. Vyombo hivi vimefanya kazi nzuri na fasaha ya kuitangaza nchi yetu. Naamini kuwa vyombo hivyo vitaendelea na kazi ya kuhabarisha, kuburudisha na kuelimisha kwa kuzingatia maadili. Aidha, namshukuru sana Mpiga Chapa wa Serikali kwa kuchapisha hotuba hii kwa wakati, bila kuvisahau vituo vya Televisheni ambavyo kwa namna ya pekee vimerusha hotuba hii hewani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapato, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara imepanga kukusanya jumla ya shilingi 670,009,000 kutoka katika vyano vyake mbalimbali vya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara imetengewa bajeti ya shilingi 14,671,877,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (Matumizi Mengineyo na Mishahara), fedha hizo zinajumuisha:-

- Mishahara ya Idara Shilingi 2,076,869,000.
- Mishahara ya Asasi Shilingi 5,991,270,000.
- Matumizi Mengineyo ya Idara Shilingi 3,806,163,200.
- Matumizi Mengineyo ya Asasi Shilingi 2,797,574,800.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara imetengewa jumla ya shilingi 3,880,851,000 kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya hizo, shilingi 770,611,000 ni fedha za kigeni na shilingi 3,110,240,000 ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Wizara iweze kutekeleza majukumu na malengo yake ya mwaka wa fedha 2011/2012, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe bajeti ya jumla ya shilingi 18,552,728,000 ambapo kati ya hizo, fedha za Matumizi ya Kawaida ni shilingi 14,671,877,000 na fedha za Miradi ya Maendeleo ni shilingi 3,880,851,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitoe tena shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anuani ya [www.hum.go.tz](http://www.hum.go.tz).

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi kwa hotuba yake nzuri sana.

Kabla sijamwita Mwenyekiti wa Kamati kwa ajili ya kuwasaidia Waheshimiwa Wabunge wengine na wananchi wanaotusikiliza ili kuelewana katika mambo ya msingi hapa nilitaka kutoa somo lifuatalo.

Mheshimiwa Mnyika alisimama hapa kusema anataka kutumia Kanuni ya 133 kwa ajili ya kutokuwa na imani na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Natoa somo kwa Wabunge wote. Kutokuwa na imani kwa Waziri Mkuu haimaanishi kutokuwa na imani na Mheshimiwa Pinda. Kutokuwa na imani na Waziri Mkuu maana yake ni kwamba Bunge hili likiungwa mkono halina imani na Serikali nzima. Tafsiri yake ni kwamba hoja hiyo ikipita Serikali hii lazima ivunjwe. Rais atumie utaratibu wa Kikatiba kama ni kuita uchaguzi mwingine au ni kuteua Serikali mpya. Langu mimi ni la utaratibu tu. Kwa hiyo, si jambo dogo la kulibeba tena kunya yuka kila mtu anavyotaka kama tunavyofikiri, lakini unaweza kutokuwa na imani na Waziri Mkuu, kutokuwa na imani na Naibu Spika imo kwenye Kanuni hizihizi. Kutokuwa na imani na Spika imo katika Kanuni hizihizi. Kutokuwa na imani na Mheshimiwa Rais wa Nchi imo katika Kanuni hizihizi lakini ukitaka kufanya jambo hili kubwa lazima uwe umejandaa vizuri, si jambo la kukurupuka.

Kujianaa kwake kukoje, kwa Waziri Mkuu, ni kwamba utatoa taarifa ya maandishi katika Ofisi na kwa hakika tutaipokea kwa sababu ndio utaratibu unaosemwa. Cha pili taarifa hiyo iwekwe saini na kuungwa mkono, ni matakwa ya Kanuni sio ya kwangu, ndio maana kila mmoja lazima asome hivi vitu. Taarifa hiyo iwekwe saini na kuungwa mkono na Wabunge wasiopungua asilimia 20 ya Wabunge wote na ili kukidhi matakwa haya asilimia 20 ya Wabunge wote, Wabunge wote humu ni 357, kwa hiyo asilimia 20 maana yake ni lazima iwe na Wabunge 72 kwenda mbele. Tukishaipokea taarifa hiyo kwa maandishi na ina saini za Wabunge 72 kwenda mbele walioweka saini zao na kuunga mkono kwamba hoja hii sasa iingie humu, itaingia, itajadiliwa, itapigwa kura za siri, sio zile za kuhoji za wote na maamuzi yake yatakuwa ndio maamuzi ya Bunge wala sio ya Naibu Spika au Spika au mtu mwingine yeyote. Nilitaka nieleze hili ili tuelewane, ni vizuri tuendeshe mambo haya katika taratibu ambazo zimebekwa. (Makof)

Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii au aliyedandaliwa kwa ajili hiyo.

**MHE. JUMA S. NKAMIA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Kanuni ya 99(7) na Kanuni ya 114(11) Toleo la Mwaka 2007 nachukua fursa hii kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezai wa Bajeti ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka 2010/2011 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii ilifanya kazi ya kufikiria na kuchambua Bajeti ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo tarehe 02 na 03 Juni,

2011 wakati wa vikao vya Kamati vilivyofanyika Jijini Dar es Salaam. Katika vikao hivyo, Mheshimiwa Dkt. Emmanuel John Nchimbi (Mb), Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo alitoa taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2010/2011. Aidha, Kamati illelezwa kwa kina kuhusu utekelezaji wa mpango wa maendeleo, mapato na matumizi kwa mwaka 2011/2012, makadirio ya mapato na matumizi ya fedha pamoja na kazi zilizopangwa kutekelezwa na Wizara kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

- Kuendeleza mafunzo ya Utawala Bora, mpango wa kazi kwa Viongozi wa Vyama vya Michezo vya Taifa kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi zao katika kuendeleza michezo nchini;
- Kusimamia chaguzi za Vyama vya michezo vya Taifa vitano ili kuimarisha Utawala Bora katika michezo na kuondoa migogoro ndani ya Vyama vya Michezo;
- Uendelezaji wa Vituo vya Utamaduni na Masoko katika Mikoa ya Dodoma na Morogoro;
- Kuendeleza Tasnia ya Utamaduni katika utaalamu asilia wa usukaji kwa akinamama waishio vijiji ni katika Mikoa ya Tanga, Iringa na Dodoma kwa lengo la kuanzisha viwanda vidogo vidogo katika maeneo hayo;
- Baraza la Sanaa la Taifa litaendesha mafunzo ya Sanaa kwa Walimu 100 katika Wilaya mbili za mkoa wa Morogoro kuhusu utambaji wa hadithi na uchoraji;
- Kuhakikisha filamu zinazotengenezwa zinazingatia maadili ya Kitanzania, zinatangaza Taifa na zinazingatia Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza Na. 4 ya Mwaka 1976 na Kanuni zake;
- Kuandaa na kurusha vipindi 52 vya "Lugha ya Taifa" vipindi 52 vya "Kumepambazuka" katika redio na vipindi 52 vya "Ulimwengu wa Kiswahili" katika televisheni;
- Kujenga kituo cha kurushia Matangazo (*FM Trasmitting Station*) huko Zanzibar;
- Kuimarisha vituo tisa vya *FM* vya kurushia matangazo ya *TBC* huko Shinyanga, Manyara, Moshi, Morogoro, Iringa, Mpanda, Newala, Songea na Tunduru; na
- Kuweka mfumo wa kudhibiti matangazo (*TV & Radio Monitoring System of Airtime, sales and billing*).

Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2011/2012. Ili kutekeleza vyema majukumu yaliopangwa kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, inaomba kuidhinishiwa Shilingi bilioni 18.5. Kiasi hiki kimeongezeka ukilinganisha na Bajeti ya Mwaka jana ambapo Wizara ilipewa Shilingi bilioni 18.4. Ongezeko hili bado ni dogo na halikidhi mahitaji ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2011/2012. Kwanza, Shirika la Utangazaji Tanzania (*TBC*). Kamati inalipongeza Shirika kwa kazi nzuri zilizofanyika kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 ikiwa ni pamoja na Mradi wa vituo tisa (9) vya redio FM, mradi wa kuboresha studio ya Mikocheni kuwa ya dijitali, kuonesha matangazo ya kombe la dunia 2010 na kutangaza harakati za uchaguzi mkuu 2010. Pamoja na mafanikio hayo, Shirika la Utangazaji Tanzania linakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo:-

- Ucheleweshwaji wa kupatiwa fedha za maendeleo zilizotengwa mahususi kwa ajili ya miradi ya Shirika. Mwaka wa Fedha 2010/2011 Shirika lilitengewa shilingi 1,200,000,000 na hadi kufikia mei 2011, Shirika lilikuwa limepokea shilingi 600,000,000 tu;

- Ufinyu wa fedha za ruzuku kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Shirika limetengewa kwa mwezi shilingi 100,079,416 ambazo ni pungufu kwa asilimia 44.6 ikilinganishwa na kiwango cha mwaka wa fedha 2010/2011. Hali hii inakwamisha utekelezaji wa shughuli za maendeleo na miradi mbalimbali;
- Kutotekelawa kwa Mkataba wa Utendaji wa mradi wa dijitali ambapo Serikali hajatoa udhamini wa Mkopo unaotolewa na Benki ya Maendeleo ya China yaani *China Development Bank*;
- Ukarabati wa vifaa vya kurushia matangazo (*OB VAN equipments*) vya televisheni bado haujafanyika kutokana na ukosefu wa fedha za mradi kwa wakati;
- Shirika lina upungufu wa watumishi 33 pamoja na vitendea kazi kwa ajili ya vituo vipyta vya FM vilivyoanzishwa; na
- Wizara na Idara nyingi za Serikali hazijalipa madeni yao kwa *TBC* kwa muda mrefu kutokana na huduma za vipindi mbalimbali viliviotangazwa katika Shirika hilo jambo ambalo linakwamisha baadhi ya shughuli za *TBC* kutofanyika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

- Serikali itambue umuhimu wa Shirika hili na kulitengea fedha za kutosha kuijiendesha na Fedha za Maendeleo zitolewe kwa wakati ili kurahisisha utekelezaji wa miradi mbalimbali;
- Kufuatia ukomo wa matumizi ya mitambo ya analogia kwa nchi za Afrika Mashariki ifikapo mwaka 2012, Shirika la *Star Media* lenye ubia na Shirika la Utangazaji *TBC* limeanza kutekeleza mradi wa televisheni wa digitali. Hata hivyo, mradi huo umekuwa mgumu kutekelezeka kwani Serikali hajatekeleza baadhi ya vipengele vya mkataba wa utendaji ikiwemo udhamini wa mkopo unaotolewa na *China Development Bank* ambao unatarajiwa kuwezesha ukamilishaji wa ujenzi wa mitambo hiyo ya dijitali nchi nzima.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawaomba tumsikilize vizuri Mheshimiwa Nkamia kwa sababu usomaji wake ndivyo inavyotakiwa taarifa zisomwe. Sasa wale wote wanaokuja mbele hapa tujifunze, Mheshimiwa Nkamia endelea. (*Kicheko*)

**MHE. JUMA S. NKAMIA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII):** Kamati inashauni Serikali ione umuhimu wa kutoa udhamini wa mkopo haraka kwani ucheleweshaji huu utaathiri mradi kutosambaa nchi nzima kabla ya ukomo wa matumizi ya mitambo ya analogia;

- Serikali iboreshe jengo la *TBC Mikocheni* kwa kukamilisha jengo lililowekewa msingi na Rais mstaafu Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi zaidi ya muongo mmoja uliopita ili *TBC* nzima ihamie eneo la Mikocheni. Hii itasaidia kutoa nafasi ya eneo la Ofisi za Nyerere Road kutumiwa na Wizara ya Habari badala ya kuendelea kutumia fedha nyingi kugharamia kodi ya pango katikati ya mji kama ilivyo sasa; na
- Serikali kuziagiza Taasisi na Idara zake zinazotangaza vipindi vyake mbalimbali kuitia *TBC* kulipa madeni kwa wakati ili kuliwezesha Shirika hili kuijiendesha kikamilifu katika maeneo ambayo halitegemei fedha za Serikali moja kwa moja. Aidha, Shirika lione umuhimu wa kutangaza habari za michezo inayohusisha timu zetu za Taifa zinapokwenda nje ya nchi badala ya kutegemea wafadhili tu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaona kuwa kuna umuhimu wa Serikali kuitisha Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari nchini pamoja na ile ya Haki ya kupata Habari na kushirikiana

na Mfuko wa Vyombo nya Habari na Baraza la Habari Tanzania (*MCT*) ili kuwawezesha Waandishi wa Habari, wamiliki wa vyombo nya habari na vyombo nya habari vyenyewe kufanya kazi zao kwa kuzingatia maadili ya uandishi wa habari makini zenye tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA). Ni dhahiri kuwa lugha ya Kiswahili imezidi kukua na kusambaa duniani ikiwa sasa ni Lugha ya Kimataifa inayotumiwa mathalani kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Afrika. Kutokana na umuhimu wa Kiswahili Katika Taifa letu na kutokana na ukweli kuwa lugha hii ndio kiunganishi kikuu cha mawasiliano kwa Watanzania, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

- Serikali kuwa makini katika kauli zake kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shughuli rasi za Serikali na kusisitiza matumizi ya Kiswahili katika semina, warsha, mabango ya matangazo barabarani, maelekezo ya bidhaa zinazotengenezwa nchini na matangazo ya biashara; na
- Serikali kuona umuhimu wa kulishirikisha Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) katika kuandaa vitabu nya Bajeti za Serikali kwa miaka ijayo kwa Lugha ya Kiswahili ili kuwawezesha wananchi kuelewa muelekeo wa hali ya Uchumi na Mapato ya Serikali pamoja na maeneo yaliyopewa kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA). Kutokana na Upungufu katika Sheria ya Haki Miliki ya Mwaka 1999 na pia kutokuwepo utekelezaji wa Sheria hii kikamilifu, bado unyonyaji wa wasanii unafanya na mawakala, wadhamini, wazalishaji na wasambazaji wa kazi za wasanii. Kamati inaona kuna umuhimu mkubwa wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na Wizara ya Viwanda na Biashara ziharakishe kuleta Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Haki Miliki na Haki Shiriki Na. 7 ya Mwaka 1999 kwani upatikanaji wa Sheria hii utasaidia ukuaji wa pato la wasanii na hata Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kiuchumi wa Sekta ya Muziki uliofanywa na Idara ya Uchumi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kuwasilishwa mbele ya Kamati tarehe 19 Juni 2011, umebaini kuwa mara baada ya marekebisho ya Sheria hii na utekelezaji wake utakapoanza, Taifa litapata chanzo kipywa cha mapato ya Serikali kwani utafiti unaonyesha kuwa:-

- Pato la Taifa linalotokana na Sanaa ya Muziki hapa nchini linakadirwa kuwa shilingi bilioni 71, ikiwa ni karibia asilimia 0.5 ya jumla ya pato lote la Taifa (*GDP*);
- Mapato yanayopatikana kwenye Sekta ya Muziki, yanatoka katika asilimia 12 tu ya kiwango kilichotakiwa kulipiwa kodi ya mapato kwenye sekta hiyo; na
- Hasara inayotokana na ulipaji mdogo wa kodi kwa Taifa (kwenye sekta ya muziki) inakadirwa kuwa asilimia 0.1 ya *GDP* ilitegemewa kuongezeka kwa kiasi cha asilimia 11 katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Sheria ya Haki Miliki na Haki Shiriki ya Mwaka 1999, ikifanyiwa marekebisho na kutekelezwa, faida kwa Wadau wa Sekta ya Sanaa itakuwa kama ifuatavyo:-

- Kipato cha wadau wote wa sekta hii ikiwemo Serikali kitaongezeka;
- Kutakuwa na ongezeko la kipato kwa walioajiriwa katika sanaa ya muziki na filamu na kwa hali hii itavutia ajira mpya katika sanaa hizi; na
- Makadirio ya walioajiriwa (kudumu) katika sekta ya muziki ni asilimia 48 ya wale wote wanaojishughulisha na muziki, asilimia 52 hufanya muziki kama kazi ya ziada hivyo baada ya kufanya marekebisho Sheria hii, kipato kitakuwa zaidi na kitafanya wengi kwenye sekta hii kuithamini kazi ya sanaa na kuifanya ya kudumu kwani itakuwa inawalipa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia faida zilizo orodheshwa hapo juu, Kamati inatoa maoni yafuatayo:-

- Baraza la Sanaa kwa kushirikiana na Bodi ya Filamu Tanzania lihakikishe linadhibiti filamu zinazoiingizwa nchini kiholela na zinazokiuka mila na desturi za Kitanzania ambazo hazina manufaa kwa Taifa letu;
- Taasisi za Serikali, Polisi, Forodha na Mahakama washirikiane na Chama cha Hakimiliki Tanzania (*Copyright Society of Tanzania - COSOTA*) kukomesha uharamia wa kazi za sanaa;
- COSOTA imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Haki Miliki na Haki Shiriki Namba 7 ya Mwaka 1999. Toka COSOTA ianzishwe bado kumekuwa na malalamiko ya wasanii kuhusu haki zao na malipo katika kazi za kisanii. Kamati inashauri Serikali kupitia Wizara husika kufanya mapitio ya Sheria ya COSOTA ili kuzipa hadhi kazi za sanaa kwani nchi nyingi za jirani zimeweza kulinda kazi za sanaa za wasanii wake na kuzifanya kuwa ajira kwa kutumia vyombo vya kisheria vilivyomo katika nchi zao mfano mzuri ni Malawi na Nigeria.
- Kumekuwa na utekelezaji mdogo wa Sheria kwenye ulipaji wa mirabaha na kodi kutoka kwenye sekta ya sanaa ikijumuisha muziki na filamu. Wazalishaji, wasambazaji na watumiaji wa kazi za sanaa hawalipi mirabaha kama inavyostahili kwa mujibu wa Sheria. Kamati inashauri Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) isimamie kuhakikisha mirabaha na kodi zinalipwa kwani Serikali inapoteza mapato mengi ambayo yangesaidia katika kuinua uchumi wa nchi;
- Serikali iboreshe vyuo vilivyokuwepo kwa ajili ya Walimu wa kufundisha sanaa. Kwa mfano Chuo cha Butimba na vingine vilivyopo nchini ili kusaidia kukuza vipaji vya sanaa na kutengeneza ajira kwa vijana na pia kukuza pato la Taifa; na
- Serikali kuona haja ya Jumba la Sanaa Bagamoyo kuwa chini ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo badala ya kuwa chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Vilevile, COSOTA kutoka Wizara ya Viwanda na Blashara na kuwa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Hii itasaldia ufuatiliaji wa karibu na utekelezaji mzuri kwani Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ndio haswa Wizara husika kwa taasisi hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, Baraza la Michezo la Taifa (BMT). Pamoja na ufinyu wa bajeti bado Baraza la Michezo la Taifa (BMT) limekuwa likitekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria iliyoliunda ya mwaka 1967 ikiwa ni pamoja na kuvisimamia vyama 30 vya michezo na kuandaa mafunzo kwa viongozi mbalimbali wa michezo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa Baraza linatekeleza majukumu yake, bado kuna maeneo ambayo Kamati inaona juhudzi zaidi zinahitajika na inatoa ushauri ufuatao:-

- Upo umuhimu wa baraza hili kupewa ofisi katika Uwanja Mpya wa Taifa badala ya kuendelea kutumia majengo ambayo ni mabovu na yanayohatarisha usalama na maisha ya wafanyakazi;
- Wizara iangalie vizuri uwepo wa Baraza la michezo na wakati huo huo kuwa na kurugenzi ya michezo katika Wizara kwani inaonekana kusababisha mwingiliano wa majukumu ya kazi;
- Serikali iteuwe Baraza Jipyaa la Michezo kwani kwa mujibu wa Sheria, Baraza liliopo lilishamaliza muda wake tangu mwaka 2009;

- Serikali itenye fedha za mafunzo kwa wataalamu wa Wizara kwani Sheria za Michezo zinabadilika mara kwa mara;
- Wataalamu wanaoagizwa kutoka nje kuja kufundisha michezo mbalimbali nchini wapewe nafasi ya kutoa mafunzo kwa wataalamu wetu wa ndani ili baada ya mikataba yao kuisha, Taifa libaki na wataalam wa ndani na hivyo kuepuka gherama za kukodisha wataalam wengine kutoka nje;
- Baraza la Michezo lihakikishe linaondoa ama kupunguza uwingi wa Vyama vya Michezo nchini jambo ambalo limekuwa likisababisha vurugu na misuguano isiyio na manufaa kwa maendeleo ya michezo nchini;
- Pamoja na Serikali kuhakikisha kuwa kuna Afisa Maendeleo ya Michezo katika kila Mkoo bado Afisa huyu hajatengewa fungu la maendeleo ya michezo hivyo hutegemea hisani ya Mkuu wa Mkoo ama Katibu Tawala Mkoo (*RAS*), jambo ambalo linamuwia vigumu kutekeleza kazi zake. Vilevile, Halmashauri nyingi za Wilaya nchini hazitengi fedha kwa ajili ya maendeleo ya michezo na hivyo kumfanya Afisa huyu kushindwa kufanya kazi zake ipasavyo; na
- Serikali ianze kutenga bajeti kwa timu zinazowakilisha nchi katika mashindano ya kimataifa kuliko kila mara kutegemea ufadhili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, sekta ya Maendeleo ya Vijana. Takribani nusu ya Watanzania ni vijana na watoto lakini asilimia 60 mpaka 70 ya Watanzania wako katika maeneo ya vijiji ambapo ajira kubwa ni kilimo. Hata hivyo, lipo tatizo kubwa la ukosefu wa ajira nchini ingawa Serikali imejitahidi kusomesha vijana katika sekta mbalimbali. Kamati inashauri kwa kuwa maendeleo ya vijana yanasmamiwa na Wizara hii, ni wakati muafaka sasa Serikali kuboresha sekta ya maendeleo ya vijana ili kukidhi mahitaji yao na hasa katika ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wizara ya kuwaendeleza vijana katika vituo vyake vya Ilionga, Sasanda na Marangu, Kamati inashauri yafuatayo yafanyike ili kuboresha mafunzo katika vyuo hivi:-

- Vituo hivi visajiliwe katika *National Council for Technical Education (NACTE)* ili viweze kutoa mafunzo yenyehadhi ya Cheti, Stashahada na hata Shahada kwa wahitimu;
- Serikali iongeze Wakufunzi katika Fani ya Maendeleo ya Vijana katika Kilimo, Maarifa ya Nyumbani na Ufundii;
- Serikali itenye bajeti kwa ajili ya vituo hivyo badala ya utaratibu wa sasa wa kuendendesha mafunzo kwa mtindo wa zima moto;
- Serikali kuendelea kutoa elimu kwa vijana kuhusu kujikinga na maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) na athari za mimba za utotoni hasa katika Mikoa ambayo inaongoza kwa matatizo hayo;
- Wizara kuandaa programu ya kuwaelimisha vijana namna ambayo wateweza kujiajiri wenye na kuachana na makundi yasiofaa pamoja na kushinda vijiweni; na
- Awamu ya pili ya ujenzi wa uwanja wa Taifa ianze mapema kwani ule uliojengwa utachakaa kabla ya awamu ya pili kujengwa. Hii pia itasaidia katika kuongeza pato la Taifa

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya jumla. Pamoja na maoni yote, Kamati inatoa ushauri wa jumla wa kisekta kama ifuatavyo:-

1. Mfuko wa Uwezeshaji maarufu kama Mfuko wa JK umeonesha kuwasaidia sana Watanzania, hata hivyo vijana wengi vijiji hawakufaidika nao japokuwa ndio wazalishaji wakuu. Serikali itengeneze mpango maalum wa kuwafikishia rasilimali fedha vijana vijiji;
2. Kwa kuwa kumekuwa na mazoea ya kuundwa kwa vigenge vya vijana wasiojishughulisha Mijini na Vijiini, Serikali irejee Sheria ya Nguvu Kazi na kuvigeuza vijiwe au vigenge hivyo vya vijana kuwa vikundi vya ajira na uzalishaji. Vikundi hivyo vipewe nyenzo, mitaji na mafunzo ili pia kutatua tatizo la ajira;
3. Kuanzishwe mfumo wa kutambua kazi rasmi na zisizo rasmi ili kuwaruhusu vijana kujajiri;
4. Vyuo vya VETA virudishwe Wizara ya Kazi na Ajira au Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ili kusimamia vizuri sekta hiyo ya vijana kwani Vyuo hivyo vinalenga maendeleo ya vijana hususan ajira;
5. Kutambua vikwazo vinavyosababisha kutokuwepo kwa maendeleo endelevu ya vijana; na
6. Mikataba yote iliyosainia yenyewe kukuza na kuleta tija kwa vijana na utamaduni wa Taifa itungiwe Sheria haraka ili Taifa linufaike na Mikataba hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani. Kwa niaba ya Kamati, naomba kukushukuru wewe binafsi kwa namna unavyoendesha Vikao vya Bunge kwa umahiri na busara na kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati. Aidha, nawapongeza Wenyevitii wote wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa jinsi wanavyokusaidia kuendesha shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Emmanuel John Nchimbi (Mb) Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Fenella Ephraim Mukangara (Mb), Katibu Mkuu Ndugu Sethi Kamuhanda, Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Sihaba Nkinga na watumishi wote wa Wizara na Mashirika yaliyo chini ya Wizara hii kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia wakati wa kutekeleza kazi za Kamati. Kamati inawashukuru sana na kuwataki mafanikio makubwa zaidi katika kazi za ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa umuhimu wa kipekee, nawashukuru Wajumbe wa Kamati yangu kwa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza kazi za Kamati. Naomba niwatambue wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mwenyekiti na Mheshimiwa Juma Suleiman Nkamia, Makamu Mwenyekiti. (*Makofii*)

Wengine ni Mheshimiwa Capt. John Damian Komba, Mheshimiwa Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare, Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, Mheshimiwa Moza Abedi Saidy, Mheshimiwa Donald Kevin Max, Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi, Mheshimiwa Mhe. Hamad Ali Hamad, Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir, Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, Mheshimiwa Mariam Salum Msabaha, Mheshimiwa Mch. Assumpter Nshunju Mshama, Mheshimiwa Asha Mohamed Omar, Mheshimiwa Ramadhan Haji Salehe, Mheshimiwa Dkt. Seif Seleman Rashid, Mheshimiwa Rebecca Michael Mngodo, Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda, Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee na Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru kwa dhati sana wananchi wa Jimbo la Kondoa Kusini na Kondoa kwa ujumla na familia yangu yote kwa ujumla, lakini pia niwashukuru viongozi wote wa Vyama vya Upinzani katika Wilaya ya Kondoa wanaoshirikiana na mimi sitowataja majina kwa sababu naogopa huenda wakafukuzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashillilah akisaidiwa na Makatibu wa Kamati Ndugu Hosiana John na Ndugu Grace Bidya kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi Taarifa hii kutoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Juma Nkamia kwa hotuba hiyo kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, ukiwa kama Makamu wa Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Tunakushukuru sana kwa mara nyingine kwa usomaji wako amba o umetufundisha namna ya kuweka mambo sawasawa hapa, maana wewe una uzoefu wa kutumia *Mc* hizi kwa miaka mingi.

Waheshimiwa Wabunge, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo wanafanya maonyesho ya shughuli za Wizara hiyo katika eneo letu la maonyesho na kuuza picha za viongozi wa Kitaifa.

Pia kampuni ya *Freedom Electronic* inafanya maonyesho ya vifaa vyta umeme vya aina ya *SAMSUNG*. Wanatoa bei nafuu kwa ajili ya Wabunge wanaokwenda kununua vifaa hivyo na wananchi wengine walio katika maeneo haya.

Waheshimiwa Wabunge, lingine ni kwamba mtaona maoni ya leo ya Kamati pamoja Kambi ya Upinzani hayakuchapwa katika vijitabu vyetu vile vya kawaida ambavyo tumevizoea badala yake yako katika katarasi za A4, ni kwa sababu ile mashine yetu ya kudurusu ina matatizo kidogo, tunaomba tuvumiliane.

Nimepata vikaratasi vingi vikinukuu ile Kanuni ya "Mheshimiwa Mbunge kutotumia lugha ya kuudhi" kutoka kwa Wabunge kadhaa wakisema kwamba Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, alipotangaza kwamba Yanga wamekuwa Mabingwa peke yao bila kuwapongeza sana Simba, kidogo imewakwaza baadhi yao. Naomba niseme Mheshimiwa Waziri hakuwa na nia mbaya. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani, nitoe Mwongozo wa Spika kuhusu suala liliombewa Mwongozo humu Bungeni na Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar jana kama ifuatavyo kwa mujibu wa Kanuni ile ya 68(1) na (7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007.

Waheshimiwa Wabunge, jana wakati wa kipindi cha asubuhi mara baada ya kipindi cha maswali, nilipokea maombi ya Mwongozo wa Spika kutoka kwa Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mwenyekiti alikuwa Mheshimiwa George Simbachawene. Akasema na nanukuu:-

*"Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako, kwa kuwa katika kipindi cha maswali na majibu, Mheshimiwa Esther Matiko alisema Wanajeshi wanapochanganyika na wananchi wanabaka watoto wa shule na Mheshimiwa Waziri hakusita, akamsifia, ahsante sana na akasema kweli. Alivyomjibu kuwa ni kweli na amempongeza muuliza swali, naomba Mwongozo wako, Bunge hilli linapenda kujua kama hii natiyo kauli ya Serikali hapa Bungeni kuwa Wanajeshi wanabaka watoto wa shule?"* Mwisho wa kunukuu kwa aliyoyasema Mheshimiwa Faida Bakar.

Waheshimiwa Wabunge, Mwongozo wangu. Nimepitia Taarifa Rasmi za Majadiliano ya Bunge ili kupata mtiririko wa swali la Mheshimiwa Esther Matiko ambalo aliuliza na mimi nanukuu:-

*"Kwa kuwa uwepo wa Wanajeshi wamechanganyika na wananchi kumepelekea matendo mengine maovu kutendeka kama ubakaji wa wanafunzi wa shule za msingi, je, Serikali haioni hiki kitu ni kibaya sana na kinahitaji uharaka wa aina yake kuwahamisha wananchi hao haraka sana iwezekanavyo?"* Mwisho wa kunukuu swali la Mheshimiwa Matiko.

Waheshimiwa Wabunge, jibu la Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi lilikuwa na mimi nanukuu alivyosema:-

"Kuhusu vitendo vya ubakaji ambavyo nimevisikia, ni kweli. Tunamshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kutuletea taarifa hizo na naamini wenzangu katika Wizara husika suala hili litachunguzwa kwa sababu kwa vyovoyote vile lazima Jeshi litakuwa na majirani. Kwa hiyo, nadhani tatizo hapa siyo kwamba ilko karibu ila ni tabia, kama ni kweli, litashughulikiwa". Mwisho wa kunukuu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuzingatia jibu la Mheshimiwa Waziri, ni dhahiri kwamba Mheshimiwa Waziri hakutamka kwamba Wanajesi wanabaka watoto wa shule, bali alichokisema ni kwamba Serikali ilikuwa imesikia na kumshukuru Mheshimiwa aliyeuiliza swali kwa kutoa taarifa hiyo Serikalini ili iweze kufanyiwa kazi na hatua ziweze kuchukuliwa. (*Makofii*)

Nawaomba Waheshimiwa wote ambao tunajibu maswali au kutoa maelezo humu Bungeni kuendelea kuwa na umakini ambao tumekuwa nao kwa ajili ya kufanya shuguli za Bunge letu kuwa bora zaidi.

Waheshimiwa Wabunge, huu ndiyo Mwongozo wangu kuhusu suala hili. Nawashukuruni kwa kunisikiliza. Tutaendelea kufafanua Miongozo mingine kadri muda utakavyokuwa ukiruhusu. Kwa sababu ya muda, kabra sijamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, naomba sasa nimwite Mheshimiwa Mwenyekiti wa Bunge, Mheshimiwa Mabumba ili aje kuendeleza hili jahazi hapa mbele. Mheshimiwa Mabumba! Inaelekea kuna mawasiliano kidogo, basi nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI - MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI (WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO):** Mheshimiwa Naibu Spika, nina matatizo kidogo ya macho, wakati mwingine unaweza ukaona machozi yanatoka, silii! Ni matatizo kidogo ya macho, nimepata *eye infections*.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai, afya njema na kunipa fursa ya kipekee ya kufanya maajabu yenyepi manufaa kwa taifa langu; kwa baraka zake, niliweza kung'ara kwenye sanaa na kuwa nyota wa muziki wa Bongofleva, ukipenda – *Hip Hop*; kwa uwemo wake leo nimkuwa Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini na kwa mapenzi yake, mimi Msanii wa Bongofleva sasa nimkuwa Waziri Kivuli wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbilinyi, sekunde tu! Sasa, naomba kumkaribisha Mheshimiwa Mabumba ili aweze kuendelea.

*Mwenyekiti (Mheshimiwa Sylvester Massele Mabumba) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, endelea!

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI - MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI (WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Bajeti ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 99 (7) toleo la 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua na kuthamini imani na heshima kubwa niliyopewa na wananchi wa Jimbo la Mbeya Mjini katika Uchaguzi Mkuu uliopita. Licha ya kuletewa mabomu ya machozi, virungu na bado hakuna yeypole kati yetu aliyegogopa. Uwongo haukuweza kufunika ukweli na hata rushwa haikuweza kurubuni akili. Wananchi kwa umoja wao walijitao mhanga kulinda kura zetu bila woga na hatimaye Dunia nzima inajua na imekubali kuwa mimi ndiye SUGU na CHADEMA si chama legelege, bali ni Chama makini na kinachoaminika mbele ya jamii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru na kumpongeza kwa moyo wa dhati kabisa Katibu Mkuu wa Chama changu, Dkt. Wilbrod Peter Slaa na Makamanda wote wa CHADEMA nchi nzima kwa kazi kubwa tulioifanya katika Uchaguzi Mkuu uliopita na kwa harakati nzito tunazoendelea

kuzifanya za kuelimisha jamii juu ya haki zao za msingi. Watapiga kelele sana lakini hatutarudi nyuma, tunasonga mbele mpaka kieleweke. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima, namshukuru Kiongozi Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani na Mwenyekiti wa CHADEMA, Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe kwa kuniamini na kunituea kuwa Waziri Kivuli wa Wizara hii nyeti. Namshukuru pia Naibu Kiongozi Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto (Mbunge) na Mnadhimu Mkuu wa Kambi rasmi ya Upinzani, Mheshimiwa Tundu Lissu, kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya Kibunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii pia kuwashukuru kwa dhati wadau wote wa Sekta ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, kwa kutuamini na kuthamini kazi kubwa ya uwakilishi inayofanywa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, hata kuamua kutupa ushirikiano mkubwa katika maandalizi ya hotuba hii. Naomba niwatambue baadhi ya wadau hao kwa shukrani kama ifuatavyo:- Baraza la Habari Tanzania (*MCT*), Umoja wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (*UTPC*), Baraza la Sanaa la Taifa (*BASATA*), *Rulu Arts Promotions* inayosimamia sanaa na Wasanii wote waliokuja kuunga mkono hotuba hii ya Kambi ya Upinzani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya habari, weledi na maadili ya uandishi wa habari. Vyombo vyaa habari ni taasisi muhimu sana katika ujenzi wa Taifa lenye kufuata misingi ya demokrasia na utawala bora. Vyombo vyaa habari vina dhima kubwa ya kutoa habari na taarifa kwa umma wa Watanzania kuhusu mambo yanayohusu maisha yao na vilevile kutoa elimu na burudani. Vyombo vyaa habari ni kiungo muhimu cha kuunganisha jumuiya mbalimbali, kujenga Utaifa, umoja na kuhimiza maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyombo vyaa habari kwa ujumla wake, ni taasisi yenye nguvu. Ina uwezo mkubwa wa kujenga na vilevile kubomoa ikiwa vitatumwa na kuijendesha vibaya au kuingiliwa uhuru wake. Hivyo basi, wakati vyombo vyaa habari vina wajibu wa kufanya kazi kwa kuzingatia umakini, weledi na maadili ya uandishi wa habari, Serikali nayo ina wajibu mkubwa wa kuhakikisha uhuru na haki za kutafuta na kupata habari vinalindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiotiliwa shaka kuwa baadhi ya vyombo vyaa habari vimikuwa vikiuki kabisa maadili ya uandishi wa habari. Kinachosikitisha zaidi ni pale ambapo baadhi ya Waandishi wa Habari na baadhi ya Vyombo vyaa Habari na ambavyo vimepewaa dhamana kubwa na jamii wanapokubali kutumiwa na baadhi ya watu wenye nguvu ama za kisia au za kifedha ili kuendeleza ajenda zao binafsi. Hili ni jambo lisilopendeza hata kidogo na halina mustakabali mzuri kwa amani na maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachosikitisha zaidi, vyombo vyaa habari vyaa Serikali na hapa nalizungumzia Gazeti la Serikali *Daily News* kuongoza katika ukiukwaji wa maadili ambapo katika kipindi cha mchakato wa Uchaguzi Mkuu uliopita, gazeti hili lilitchapisha tahariri ya uchochezi iliyosema, "Kamwe Dkt. Slaa hatakuwa Rais wa Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania." Maoni haya ya Mhariri yalilenga kuleta uchochezi na kujenga hoja kwamba hata kama Watanzania watamchagua Dkt. Slaa kuwa Rais wao, lakini kamwe hatakabidhiwa jukumu la uongozi, jambo ambalo ni la hatari kwa usalama wa Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la hatari zaidi hapa ni kwamba walioendesha vitendo hivi vyaa uchochezi ni Wahariri wa Gazeti la Serikali ambalo lilitakiwa kuwa mfano wa kuigwa kwa vyombo vingine vyaa habari nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge hili Tukufu imemchukulia hatua gani Kaimu Mhariri Mtendaji wa gazeti hilo ambaye aliidhinisha kuchapishwa kwa tahariri hiyo? Je, Idara ya Habari Maelezo iliwhi kuandika barua kwa Mhariri huyu kumuonya kama ambavyo imikuwa ikifanya hivyo kwa magazeti mengine; hata kabla ya habari hajaandikwa, tayari barua inakuwa imeandaliwa na kinachosubiriwa ni gazeti kuchapishwa na barua hiyo kufika kwa wahusika? Kama Serikali hajamchukulia hatua, Waziri anaweza vipi kuwa na mamlaka ya kuadhibu vyombo vingine vinavyodaiwa kukiuka maadili ya uandishi wa habari

wakati yenyewe imeshindwa kuwajibisha Wahariri wa gazeti lake? Uchochezi huu unapaswa kukemewa na kila Mtanzania kwa nguvu zetu zote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna tabia imezuka ya viongozi wa Serikali kuvitisha vyombo ya habari pale vinapotoa udhaifu wa Watendaji Serikalini, kama ilivyotokea hapa Bungeni hivi karibuni wakati Mheshimiwa Waziri Ofisi ya Rais (Mahusiano) alipotoa vitisho kwa gazeti la Mwananchi. Kambi ya Upinzani inalaani kitendo hicho na kuitaka Serikali iache mara moja vitisho kwa vyombo vya habari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo ambalo wote tunatakiwa tulikemee kwa nguvu zetu zote na kila inapowezekana tuwaumbue na tuwataje wale wote wanaoshiriki katika matendo haya ambayo hayana nia njema sio tu kwa tasnia yenyewe ya habari kwa kuipa jina baya na kuipaka matope, bali pia kwa nchi yetu kwani tuna mifano dhahiri hapa Afrika na kwingineko duniani juu ya athari ambazo zimewahi kutokea vyombo vya habari vilipotumika vibaya. Sote tunakumbuka yaliyofanywa na vyombo vya habari vya Serikali kule Rwanda na maafa yaliyotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Haki ya Kupata Habari. Haki ya kupata habari ni haki ya msingi ya binadamu na inalindwa na Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni haki ambayo inamhusu kila Mtanzania bila ya kujali wadhifa au daraja lake kwenye jamii, umri au jinsia. Mwaka 2006, nataka niamini kwa nia njema kabisa, Serikali ilianzisha mchakato wa kutunga Sheria ya Uhuru wa Habari kwa kutoa Rasimu ya Muswada wa Sheria hiyo. Hata hivyo Rasimu ya Muswada huo ilikataliwa na wadau kwa sababu haikukidhi haja wala viwango vya Sheria kama hiyo vinavyotakikana. Mwaka 2007, Serikali iliitikia wito wa Wadau wa Habari na Haki za Binadamu wa kutaka kuwepo na sheria mbili tofauti na kutenganisha Rasimu yake ya Muswada wa Sheria ya Uhuru wa Habari na kutengeneza Rasimu mbili, moja ya Sheria ya Haki ya Kupata Habari na nyingine ya Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kutenganisha Muswada huo ilikuwa na bado ni muhimu sana kwa sababu Sheria ya Haki ya Kupata Habari ni mtambuka na inahusu haki ya Kikatiba ya Watanzania wote. Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ni ya kisekta na inahusiana zaidi na kutoa mwelekeo wa jinsi vyombo vya habari vitakavyofanya kazi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato huo ulipata mwitiko mzuri kutoka kwa Wadau mbalimbali wa Habari na Wanaharakati wa Haki za Binadamu ambao kwa umoja wao walitembea nchi nzima kukusanya mawazo na mapendekezo ya wananchi kuhusu Sheria ya Haki ya Kupata Habari. Walipeleka mapendekezo yao kwa Serikali ili yaweze kujumuishwa katika mchakato wa utungaji wa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi rasmi ya Upinzani inasilitiza kuwa Sheria hii ni muhimu sana, kwani itaimarisha utawala wa wazi na uwajibikaji. Utawala ulioshamiri katika mila za usiri ndio ulioifikisha Tanzania yetu mahali pabaya. Ndio chanzo cha mikataba mibovu na kushindwa kwa uwajibikaji kwa sababu tu Watendaji wabovu wanaweza kujificha katika kinga ya usiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitoa ahadi mwaka hadi mwaka kuhusu mchakato wa utungaji wa Sheria hii muhimu lakini hadi leo hatujaona Muswada wa Sheria hiyo ukiacha ule ambao wadau wamependekeza. Kambi Rasmi ya Upinzani tunaitaka Serikali kuuleta Bungeni Muswada wa Sheria hiyo ndani ya mwaka huu, ili tuujadili na kupitisha Sheria hiyo bila ya kukawia zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani tunaitahadharisha Serikali kuwa isijaribu kuchakachua hata kidogo maoni hayo ya wadau kwa sababu tumejiridhisha kuwa yana msingi na dhamira ya dhati ya kuboresha tasnia nzima ya habari na uhuru wake. Tunachukua fursa hii kuwataarifu mapema wadau wote wa habari kwamba tutakuwa pamoja nao wakati wote wa harakati za kushinikiza Muswada huo uletwe Bungeni ndani ya mwaka huu. Tunataka Sheria hiyo ipatikane mapema iwezekavyo ikiwa imebeba maoni yote ya wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na umuhimu wa kupata Sheria Mpya ya Vyombo vya Habari, ni muhimu pia kuwapo kwa Sheria inayokidhi mahitaji na inayokubalika kwa jamii yote ya wananchi. Sheria ya Habari katu si mali ya Waandishi wa Habari na wamiliki wa vyombo vya habari pekee yao. Ni Sheria ya Watanzania wote. Hii ni kwa sababu, haki ya kupata na kutoa habari, ni haki ya asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wananchi wanasubiri Sheria mpya ya Habari, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuleta Bungeni Muswada wa kufuta Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976 kwa kuwa Sheria hiyo ni kinyume na Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari. Katika Sera ya Habari na Utangazaji iliyotolewa na Serikali na kuitishwa na Bunge lako Tukufu mwaka 2003, kipengele cha 2.2.2 kinaelekeza kwamba; *"Sheria mbovu za habari ambazo zimekuwa zikkosolewa na kulalamikiwa kwa kuwahaziendani na misingi ya kidemokrasia zitadurusiwa, kurekebishwa au kufutwa."* Hivyo basi, Serikali iliahidi kuwa itatunga Sheria mpya zinazoendana na wakati na kukidhi mahitaji ya kidemokrasia ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasisitiza kuwa mapendekezo ya wadau yanakidhi kwa kiwango kikubwa ahadi hiyo ya Serikali na wadau walizipitia Sheria 27 zinazogusa habari na kupendekeza Sheria 17 miongoni mwa hizo ama zidurusiwe, zirekebishwe au kufutwa. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali isiendelee kususua katika jambo hili na ilete Muswada Bungeni wa Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ndani ya mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa Shirika linalochapisha Magazeti ya Serikali (*Daily News* na Habari Leo) halina Mtendaji Mkuu, toka alipoondolewa Mtendaji aliyekuwepo. Tangazo la kumtafuta Mtendaji mpya mwenye sifa na hadhi ya kuongoza liliondolewa katika mazingira tatanishi. Hivi sasa Shirika hilo limeyumba kiuongozi jambo ambalo limesababisha kushuka kwa uzalishaji. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuanzisha mchakato wa kumpata Mtendaji Mkuu wa Shirika hilo mwenye sifa na hadhi, kabla ya mwaka huu haujamalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya vijana. Benki ya Taifa ya Vijana ianzishwe. Sehemu kubwa ya watu wa Taifa hili ni vijana, tukiendeleza vijana basi tutakuwa tumeendeleza sehemu kubwa ya Taifa. Ni muhimu kama Taifa tuweke vipaumbele vya makusudi vya kibajeti vya kuhakikisha vijana wanapewa kipaumbele cha kutosha na kujengewa mazingira mazuri ya kujikomboa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuanza kujenga mazingira mazuri ya kuchochea ajira nyingi kwa vijana kuititia shughuli za ujasiriamali na shughuli nyininge za kiuchumi, Kambi Rasmi ya Upinzani, inaitaka Serikali ianzishe Benki ya Taifa ya Vijana. Tunapendekeza kuwa mchakato wa kuanzishwa kwa benki hiyo uanze ndani ya mwaka wa fedha wa 2011/2012 na benki hiyo iwe na masharti nafuu kwa manufaa ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wa Baraza la Vijana la Taifa. Kwa mara ya kwanza Serikali iliahidi kuanzisha Baraza la Taifa la Vijana kuititia Sera ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 1996 na tangu wakati huo kila mwaka Serikali imekuwa ikiahidi hivyo hivyo lakini hadi leo hakuna kilichofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani haiko tayari tena kuona Serikali hii ikiwapotezea muda vijana wa nchi hii. Tunamtaka Waziri atoe kauli ya moja kwa moja ya kuhakikisha kuwa mchakato wa kuanzishwa kwa Baraza la Taifa la Vijana unaanza mara moja na Baraza linapatikana ndani ya mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haja ya mabadiliko Idara ya Maendeleo ya Vijana. Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kuwa hali mbaya ya maendeleo ya vijana nchini, pia inachangiwa na uongozi dhaifu usiokuwa na ubunifu wa kutosha wa Idara ya Maendeleo ya Vijana, ambao kwa takribani miaka 10 umekuwa na watu walewale kwenye nyadhifa takribani zote ikiwemo ile ya

Mkurugenzi. Kwa hiyo, tunataka Serikali kuifanyia mabadiliko ya viongozi Idara hii, ili kuleta ari na ubunifu mpya kikazi. Sanjari na hilo, tunapendekeza Idara hii longezewe nguvu na raslimali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Utamaduni. Ni ukweli ulio wazi kuwa sekta ya utamaduni kwa sasa imepoteza mwelekezo kwa sababu mipango mingi ya maendeleo haizingatii umuhimu wa utamaduni wetu kwa tafsiri pana. Maendeleo ya jamii yoyote ile yanategemea utamaduni wa nchi husika, hivyo Kambi ya Upinzani inasisitiza kuwa ni lazima Serikali irudi nyuma na kujitathimini vizuri katika sekta ya Utamaduni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tunaishi katika kipindi muhimu cha mpito wa historia na utamaduni ya tangu kizazi cha uhuru na kile kilichozaaliwa baada ya uhuru, ni muhimu kuhakikisha kuwa historia na utamaduni wetu, unakusanya, unachambuliwa na kuhifadhiwa vizuri kwa ajili ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo. Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kuwa Serikali iunde Kamisheni Maalum ya Rais ya Historia, ambayo pamoja na mambo mengine, iwe na majukumu yafuatayo:-

- (i) Kufanya utafiti wa watu wote waliota mchango mkubwa wa kihistoria katika kupigania Uhuru wa Tanganyika, Mapinduzi ya Zanzibar na Muungano ili waweze kukumbukwa na michango yao kuenziwa.
- (ii) Kutambua maeneo, majengo, na sehemu mbalimbali zenyenye umuhimu mkubwa wa kihistoria.
- (iii) Kupitia matukio muhimu ya historia yetu ili yaweze kuelezewa katika mwanga wa kihistoria. Hii ni pamoja na Uhuru, Mapinduzi, Muungano, Uasi wa Jeshi, Azimio la Arusha, Operesheni Vijijini, Vita ya Kagera, Enzi za Soko Huria na kadhalika.
- (iv) Kukusanya vielelezo mbalimbali vyenye umuhimu mkubwa wa kihistoria kutoka watu binafsi, taasisi binafsi na nje ya nchi ili hatimaye vitu hivyo, viweze kuingizwa katika historia yetu kwa ajili ya kuwa ni urithi wa vizazi vijavyo.
- (v) Kuandika ripoti maalum juu ya historia yetu na matukio mbalimbali ili yaweze kutunzwa kama sehemu ya historia yetu maalum.
- (vi) Kutoa mapendekezo ya jinsi ya kuenzi utamaduni wetu muhimu pamoja na watu mbalimbali ambao walichangia katika matukio mbalimbali kwa namna ya pekee na ambao historia yetu hajjawakumbuka ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Sanaa. Nianze kwa kutangaza maslahi kwenye sekta hii, kuwa mimi ni Msanii wa Muziki wa Kizazi Kipy (Bongofleva) na nimekuwa kwenye fani hii kwa muda mrefu sasa. Kwa uzoefu wangu na kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, nachukua fursa hii kuieleza Serikali kwamba: "Sanaa si mapambo au burudani tu kama ilivyozoleka, bali sanaa ni ajira inayoweza kubadilisha maisha ya Mtanzania ye yeyote anayejihuisha nayo na inaweza kabisa kuwa moja ya vyanzo vikubwa vya mapato ya Bajeti ya Serikali, ikiwa Serikali yenye we itadhamiria kwa dhati kufanya mapinduzi makubwa katika tasnia hii".

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa mbalimbali kutoka nchini Marekani za mwaka 2007 zilionyesha kuwa; "Makampuni yanayotengeneza na kuuza kazi za hatimiliki yataendelea kuwa moja ya nguvu kubwa za uchumi wa Marekani, kwani mapato yatokanayo na filamu, muziki, michezo ya video na mifumo ya kompyuta yanachangia zaidi ya asilimia 6.5 ya Pato la Taifa na kuajiri takribani watu milioni 5.4..." mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kuwa Sekta ya Sanaa ikifanyiwa mapinduzi makubwa inaweza kabisa kuwa moja ya vyanzo vikubwa vya bajeti ya Serikali yetu na kuchangia maendeleo ya Taifa hili. Ikiwa Sanaa inachangia kwa kiasi kikubwa uchumi wa Taifa kubwa kama Marekani, je, Tanzania tuna maendeleo gani ya kujivunia hata tupuuze sanaa? Bado hatujaipa sekta hii umuhimu wake unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasanii pamoja na Serikali bila kujua, wamekuwa wakinyonywa kimapato na wadhamini, wazalishaji na wasambazaji wa kazi za sanaa, hususan kwenye biashara ya kuuza muziki na filamu. Kwa mujibu wa utafiti wa Dkt. Jehovaness Aikaeli ambaye ni Mchumi

wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), alisema sekta ya muziki pekee ikifanyiwa maboresho, inaweza kuingizia Serikali mapato ya kodi ya wastani wa shilingi bilioni 50 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti chache zilizowahi kufanyika, ukiwemo utafiti wa Taasisi ya RULU/BEST – AC, wa mwaka 2007/2008, zimeonyesha kuwa Wasanii na Serikali kwa pamoja, wamekuwa wakipoteza mapato mengi yatokanayo na biashara ya kazi za sanaa, hususan muziki na filamu kama ifuatavyo:-

- (i) Maharamia wameendelea kurudufisha santuri na kanda za muziki, filamu na kazi nyngine za sanaa na kujipatia mapato haramu kwa jasho la Wasanii, lakini hakuna hatua kali zinazochukuliwa kukomesha hali hii.
- (ii) Wasanii wengi wamekuwa wakiingja mikataba isyo na manufaa kwao baina yao na Wadhamini, Wazalishaji, Wasambazaji wa kazi za Sanaa na hivyo kunyonywa kimapato, kwa sababu tu ya kukosa uelewa mzuri wa masuala ya mikataba na kutokuwepo udhibiti wa kutosha wa Serikali.
- (iii) Serikali kwa mwaka 2007 pekee, ilipoteza mapato ya muziki ya jumla ya shilingi bilioni 71.
- (iv) Kodi inayokusanya na Serikali katika Sekta ya Muziki, inapatikana katika asilimia 12 tu ya kiwango cha mapato kinachotakiwa kulipiwa kodi kwenye sekta hiyo.
- (v) Wakati wa utafiti iligundulika kuwa ni asilimia 12.5 tu ya Wafanyabiashara wa kazi za Sanaa, ndio waliokuwa wamelipa mirabaha, asilimia 87.5 hawakuwa wamelipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na wizi na uharamia huu wa kazi za sanaa na kuokoa mapato ya Wasanii na ya Serikali, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, *COSOTA* iwe Mamlaka. Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kuwa Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na.7 ya mwaka 1999 ifanyiwe marekebisho kwa lengo la kuipa meno zaidi ya kulinda haki na kuhakikisha Wasanii wananaufaika na kazi zao. Moja ya mapendekezo ni kulfanya *COSOTA* kuwa chombo chenye nguvu zaidi katika kulinda kazi za Wasanii kuliko ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo katika sehemu ya marekebisho tunayopendekeza, Kambi Rasmi ya Upinzani tunataka Sura Na. 218 ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki, ifanyiwe marekebisho ili kuunda Mamlaka ya Hakimiliki Tanzania (*Copyright Regulatory Authority of Tanzania (CORATA)*) badala ya kuiacha *COSOTA* kama ilivyo hivi sasa. Mamlaka haya yakishaundwa yatakuwa na nguvu zaidi ya kushughulikia mambo mbalimbali ya kazi za wasanii, yawe ndio msimamizi na mratibu wa masuala ya Hakimiliki kwa kushirikiana na Vyama vya Msingi vya Wasanii viliyopo chini ya BASATA, kama vile Chama cha Muziki Wa Dansi Tanzania (CHAMUDATA) na kile cha Wasanii wa Muziki wa Kizazi Kipywa yaani Tanzania *Urban Music Association (T.U.M.A)*, tofauti na sasa ambapo *COSOTA* imebakiwa na kazi ya kusajili kazi za wasanii na kukosa nguvu ya kuzilinda. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa mwenye Hakimiliki ana jukumu la kulinda haki zake kwa kwenda Mahakmani pale anapoona haki yake imepokwa na mtu au kikundi chochote, bado ipo haja ya kuhakikisha kuwa Polisi wetu wa Upelelezi wanahuksika moja kwa moja katika kulinda haki za Wasanii. Mathalani, nchini Marekani hawana Polisi wa kulinda hakimiliki moja kwa moja, lakini Shirika lao la Upelelezi (*FB*), limekuwa likifanya uchunguzi wa mara kwa mara kuhusu hakimiliki za wasanii, kila kunaporipotiwa suala la wizi wa kazi za msanii na limekuwa linahuksika moja kwa moja katika kutoa ushahidi na kusaidia kupatikana kwa haki ya msanii husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kuwa Taasisi za Serikali, Polisi na Forodha washirikiane kwa karibu na Mamlaka ya Hakimiliki na Hakishiriki tunayotaka ianzishwe (*CORATA*), kukomesha uharamia wa kazi za sanaa. Forodha watengeneze utaratibu wa

kutoza kodi kikamilifu kwenye kazi za muziki, filamu na sanaa nyingine zote zinazouzwa nje ya nchi na Mashirika ya Uzalishaji wa Kazi za Muziki –waunde ushirikiano na taratibu zao za kukabiliana na uharamia wa kazi za sanaa kwa mapana yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Februari mwaka huu, wakati akizindua kampeni ya kuzuia malaria ambayo iliwashirikisha baadhi ya wasanii, aliahidi kuundwa Kikosi Kazi (*Task Force*) kitakachowashirikisha COSOTA, Polisi, Tume ya ushindani, *TRA*, *BRELA*, Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na wasanii mbalimbali wanaojihusisha na sanaa ili kutafuta ufumbuzi dhidi ya uharamia na wizi wa kazi za sanaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Wizara kuliarifu Bunge hili, je, Kikosi Kazi hicho kiko wapi mpaka leo? Kama kiliundwa, kiliundwa kwa taratibu zipi na kwa nini suala hilo haliko wazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa *Stickers* kwenye kazi za sanaa. Mbali na marekebisho hayo ya kisheria na kimfumo tuliyopendekeza, Kambi Rasmi ya Upinzani pia tunaitaka Serikali ndani ya mwaka wa fedha wa 2011/2012, itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kuanzisha utaratibu rasmi wa kuwa na *Stickers* kwa ajili ya kazi zote za sanaa, hususan kwenye kanda na Santuri za muziki, filamu na kazi zote za sanaa zinazoshikika na kuuzika. Hapa tunashauri kuwa mamlaka tunayotaka ianzishwe, yaani (*Copyright Regulatory Authority of Tanzania*) ishirikiane kwa karibu na Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) katika kuandaa utaratibu mzima wa kuwa na *Stickers* hizo na jinsi ya kuusimamia na si kuwaachia watu binafsi tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kuwa utaratibu rasmi wa kuwa na *Stickers* ukutumika, sekta ya biashara ya kazi za sanaa inaweza kupata mafanikio ya kuridhisha ndani ya muda mfupi. Mfano mzuri ni *Sticker* yenye nembo ya *TRA* inayowekwa kwenye bidhaa za Konyagi. Faida kubwa ambayo itapatikana kwa kuwa na *Stickers* kwenye kazi za sanaa ni kuwa *Stickers* hizi zitawezesha kubaini kazi halisi (*original*) iliyofanywa na msanii mhusika dhidi ya kazi za bandia zilizorudufishwa au kughushiwa. Sambamba na hilo, mapato ya Wanamuziki, Watunzi wa Filamu na washirika wao pamoja na Serikali yataongezeka na hivyo mchango halisi ya sekta hii kwenye uchumi wa nchi utakuwa wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna taarifa kuwa Wasanii wengi kutoka nje ya nchi wanaofanya maonyesho mbalimbali hapa nchini wamekuwa hawatozwi kodi licha ya kulipwa fedha nyingi. Kwa hiyo, tunaitaka Serikali kuanzia mwaka wa fedha wa 2011/2012, ihakikishe kuwa Wasanii hao wa nje ya nchi ambao wamekuwa wakilipwa dola laki moja hadi dola laki nne kwa onyesho moja hapa nchini, wawe wanatozwa kodi ya kutosha, ili fedha hizo ziongezee bajeti kuu ya Serikali na kuwasaidia Watanzania wengi maskini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaitaka Serikali kwa kushirikiana na vyombo husika, iweke utaratibu wa kuhakikisha kuwa pale Msanii wa ndani anapofanya onyesho au kazi ya pamoja na Msanii kutoka nje, basi kuwe na mgawanyo mzuri na wa haki wa mapato kati ya Msanii huyo wa Nje na Msanii Mzawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha Sekta nzima ya Sanaa nchini na kuhakikisha inaongeza ajira zenye tija na kutoa mchango mkubwa katika ukuaji uchumi, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza hatua zifuatazo zichukuliwe:-

- (i) Serikali ndani ya mwaka wa fedha wa 2011/2012, pamoja na kufanya kazi tafiti zilizokwishafanywa na wadau mbalimbali wa sanaa, ifanye utafiti mahsus na wa kina kuhusu Sekta nzima ya sanaa (*feasibility study*), ili kubaini fursa na vikwazo vyote vilivyopo, na kuainisha njia na mikakati kabambe ya kuboresha na kuisimamia sekta nzima ya sanaa, kwa manufaa ya Wasanii na uchumi wa nchi.
- (ii) Kupitia matokeo ya utafiti huo, Wizara ndani ya mwaka wa fedha 2011/2012, iandae Mpango mahsus wa Maboresho ya Sekta ya Sanaa, ambao pamoja na mambo mengine, ulenge kuziba mianya yote ya upotevu wa mapato ya Sanaa na kuchochaea ajira nyingi na zenye tija kwa vijana.

- (iii) Chuo Kikuu cha Sanaa cha Bagamoyo kipandishwe hadhi na kuwa Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Kawawa cha Bagamoyo (*Kawawa Memorial University – Bagamoyo*). Lengo liwe ni kuhakikisha kuwa Chuo hiki kinatoa mafunzo yote ya hali ya juu ya mambo ya sanaa, michezo na utamaduni kwa vijana wa Kitanzania na wale wanaotoka ng'ambo, huku tukimuenzi Hayati Mzee Rashid Mfaume Kawawa, kwa mchango wake mkubwa katika Taifa hili alioutoa kwenye uongozi na sanaa. (*Makofii*)
- (iv) Serikali ihakikishe kuwa asilimia 90 ya bajeti zote za Wizara, Idara, Taasisi na Wakala wa Serikali zinazotengwa kwa ajili ya kunaksisha ofisi, iwe inatumia kazi za sanaa na samani zinazopatikana hapa Tanzania au zinazotokana na ubunifu wa Watanzania. Hii itachochea ajira katika kazi za Sanaa na kuweka ushindani wa kibashara ambao utainua ubora wa kazi hizo.
- (v) Masomo ya Sanaa yarudishwe katika ngazi zote za elimu katika shule za binafsi na Serikali, ili kuchochchea ubunifu na umahiri wa vijana katika kazi za sanaa na kuinua vipaji vyao mbalimbali.
- (vi) Serikali ihakikishe Mafunzo ya Sanaa yanatolewa kwa vyuo vya elimu ili kuweza kupata Walimu wa kutosha wa sekta hii.
- (vii) Mashindano ya ubunifu wa kazi za Sanaa yaanzishwe yakiwa ni sehemu ya mashindano ya michezo ya UMISHUMTA na UMISETA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kashfa ya Nyumba ya Sanaa. Nyumba ya Sanaa ilianzishwa mnamo 1972 kwa madhumuni ya kutoa mafunzo ya sanaa kwa vijana, wanawake na wasiojiweza pamoja na kutafuta masoko ya sanaa na kazi za mikono. Hata hivyo, kuanzia mwaka 1995 kumekuwepo hali ya kutolewana baina ya Wajumbe wa Bodi ya Wadhamini baada ya kutiliana shaka wenyewe kwa wenyewe, pia kati ya Bodi ya Wadhamini na Wanachama Waanzilishi wa Nyumba ya Sanaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya hali hiyo ni kufunguliwa kwa kesi Mahakamani. Katika kesi hiyo, iliyotolewa hukumu tarehe 24 Februari, 2005, Msajili aliamua kufuta rasmi usajili wa Bodi ya Wadhamini ya Nyumba ya Sanaa akiwataka wakabidhi mali na shughuli za Nyumba kwa asasi mbadala. Uchunguzi uliofanywa na Kambi Rasmi ya Upinzani umebabaini kuwa tangu kutolewa kwa hukumu hiyo, Bodi haijawahi kukasimisha amali na majukumu ya Nyumba ya Sanaa kwa asasi mbadala na badala yake imeendelea kuwepo na kupelekea Nyumba hiyo kuendeshwa kama kampuni binafsi kwa faida ya Wajumbe wachache wa Bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani ina taarifa kuwa Mwenyekiti wa Bodi hiyo iliyofutwa na baadhi ya Wajumbe wake wameleta mwekezaji ambaye wameshaingia naye ubia kimkataba, kwa ajili ya kujenga jengo la ghorofa katika eneo lenye jengo la sasa. Izingatiwe hapa kuwa mwekezaji atapaswa kulivunja au kubadilisha mfumo wa jengo la sasa la Nyumba ya Sanaa, ndipo aweze kujengwa la ghorofa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani, inaitaka Serikali na Bunge lako Tukufu lizingatie yafuatayo:-

- (i) Tujue kuwa Nyumba ya Sanaa hivi sasa inawanufaisha wachache ambao si walengwa waliokusudiwa. Tufahamu kwamba wanufaika hawa hawana rekodi ya uwekezaji katika Nyumba ya Sanaa, hivyo wanavuna matunda yaliyopandwa na wengine hasa kupitia ushirikiano mwema baina ya Serikali ya Tanzania (kupitia Ikulu), Norway (kupitia Shirika la NORAD) na Uhlanzi (kupitia Shirika la NOVIB).
- (ii) Tutambue kuwa Nyumba ya Sanaa ilikuwa ni mlango wa masoko ya sanaa na kazi za mikono, hivyo kutokuwepo kwake kunakwamisha juhudhi za wazalishaji kazi

za sanaa wa Tanzania kuweza kushiriki vyema masoko na hasa soko la pamoja la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuyazingatia yote hayo na kwa manufaa ya wadau wote wa sanaa na Taifa zima kwa ujumla, Kambi rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ichukue hatua zifuatazo kuhusiana na Nyumba ya Sanaa:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, tunataka Nyumba ya Sanaa irudishwe Serikalini kwa Mdhamsini Mkuu wa Serikali ili mchakato wa uanzishwaji wa Bodi huru ya kusimamia malengo yake anuai ufanyike. Uhuishaji wa Nyumba ya Sanaa utachangia sana kuongeza ajira na pato la Taifa, hivyo kupunguza tatizo la uzururaji na kilio cha masoko ya kazi za sanaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tangu kufutwa kwake mnamo mwaka 2005, Nyumba ya Sanaa imeendelea kufanya biashara pamoja na kuingia mikataba ya biashara mpaka sasa, Kambi Rasmi ya Upinzani tunaitaka Serikali ifanye tathmini na ilipwe kodi kutokana na faida ya biashara zilizoendeshwa mara baada ya kusitishwa uendeshaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani tunaitaka Serikali isitishe mara moja uvunjwaji wa jengo lilopo sasa, kwani ni utalii na ni alama ya Taifa inayoonyesha jinsi Serikali za Norway na Tanzania zilivyothamini juhudzi za wasanii na wazalishaji kujikwamua kiuchumi na kuchangia pato la Taifa. (*Makof*)

Tunataka Nyumba ya Sanaa ifufuliwe upya bila kubadili malengo yaliyopelekea kujengwa kwake na badala yake kila kitu kiboreshwe kwa kuheshimu malengo yale yale. Tunaamini Serikali hii inayojita Serikali sikuvi, itaheshimu matakwa ya Watanzania hususan Wasanii ambao pasipo shaka yoyote ile wanataka Nyumba yao irudi kwenye mikono salama kama tulivyopendekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi ya Studio ya Wasanii. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kupitia Bunge Tukufu la Jamhuri ya Muungano alitangaza kuwa amewapa Wasanii Studio ya kufanya kazi zao. Hata hivyo, baadaye wananchi na wadau wengi wa sanaa, nikiwemo mimi binafsi, tulishangaa kusikia Studio hiyo wamepewa *NGO* binafsi ya *Tanzania House of Talent (THT)*! Pia Rais aliahidi kutoa pango ambapo alitoa nyumba ya Serikali kwa Wasanii ambayo ingetumika kuendeshea Studio husika, lakini nyumba hiyo ya Serikali iliyotolewa na Rais sasa iko chini ya *THT* na ndio makao ya *THT*!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji, kwa nini ahadi hizo zitolewe kwa kikundi kimoja tu cha *THT*, tena kilichojikita zaidi katika biashara ya kazi za sanaa, wakati ahadi hizo za Rais zililenga Wasanii wote wa Tanzania? Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua na kuthamini mchango wa *THT* katika Sekta ya Sanaa ya nchi hii, lakini si sahihi kwa Taasisi hiyo binafsi kupewa jukumu la kuhodhi Studio na Nyumba iliyotolewa na Rais kwa ajili ya Wasanii wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala yake, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kuwa Studio na Nyumba hiyo iliyotolewa na Rais ambazo ni za Serikali iwe chini ya Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) kwa manufaa ya Wasanii wote na si *THT* pekee yao kama ilivyo sasa. Tunatahadharisha kuwa hili lisipozingatiwa, jina la Rais na hadhi ya Urais itachafuka kwa kuonekana kufanya kazi kwa maslahi ya watu binafsi (*THT*) badala ya kufanya kazi kwa maslahi ya umma (Wadau wa Sanaa).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Michezo. Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kuwa Michezo ni Afya, Michezo ni Burudani, Michezo ni Ajira na Michezo ni Uchumi. Hata hivyo, mwenendo na hali halisi ya Sekta ya Michezo nchini, vinadhibhirisha kuwa sekta hii imekuwa ikichukuliwa kuwa ni ya burudani pekee. Timu zetu za Taifa zifungwe au zitolewe kwenye michuanoo ya kimataifa, limekuwa ni jambo la kawaida, hakuna hatua zozote kali zinazochukuliwa kuwajibishana wala kuweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha hali ya kufanya vibaya haijurudii tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushahidi kuwa Sekta ya Michezo haijapewa umuhimu unaostahili upo wazi. Taifa letu limeendelea kuwa kichwa cha mwendawazimu, kwa timu zetu za Taifa

kuendelea kufanya vibaya na kuambulia mafanikio kidogo kwenye michuano ya Kimataifa. Kama Taifa tumeshindwa kuzalisha Walimu wa kutosha wa michezo mbalimbali na mbaya zaidi hata Walimu wachache wazalendo hususan wa mpira wa miguu, wenye ujuzi na umahiri wa kuridhisha wamekuwa hawapewi motisha, pindi wanapoteuliwa kufundisha timu za Taifa. Badala yake, Serikali imekuwa ikitumia gharama kubwa kuwapa ajira Walimu wa kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri alieleze Bunge katika kipindi chote timu ya Taifa ya Vijana ilipokuwa chini ya kocha Tinoco toka Brazil, mkataba wake kwa mwezi alilikuwa akilipwa kiasi gani na Kocha wa sasa Jamhuri Kiwelu (Julio) (*Hurio* kwa Spanish) mzawa analipwa kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge ni kwa nini kocha wa netiboli, Simone Mcknnis raia wa Australia aliyetia saini Septemba mwaka jana kwa mkataba wa miaka mitatu kufundisha mchezo huo alikatiza mkataba wake na kuondoka kurudi kwao Australia kwa kile kilichoelezwa kuwa Serikali kushindwa kutimiziwa masharti ya mkataba wake na haswa malipo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa kuagiza makocha kutoka nje, ni sharti uende sambamba na mpango wa kuwapatia ujuzi na uzoefu makocha wetu wa ndani ili pale makocha wa nje wanapoondoka tuweze kuwatumia makocha hao wazalendo kuendeleza michezo nchini. Kambi ya Upinzani, inashauri kuwa pale ambapo makocha wa kigeni wanapoajiriwa nchini kufundisha timu mbalimbali basi wapewe sharti la kuwa na wasaidizi ambao ni wazawa ili mikataba yao itakapomalizika basi wazawa wabakie na ujuzi na kuweza kuendeleza michezo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kambi ya Upinzani inatoa hoja kuwa Bunge hili Tukufu liweze kuutambua mchango mkubwa uliofanywa na makocha wazalendo na ikiwezekana waweze kupata nishani ya Bunge kutohana na mchango mkubwa kwenye sekta ya michezo akiwemo Julio. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka 50 baada ya Uhuru, Tanzania ina uwanja mmoja tu wenye hadhi ya kimataifa amba ni Uwanja wa Taifa wa Dar es Salaam uliojengwa kwa msaada wakati wa Serikali ya Awamu ya Tatu lakini kiwanja hicho sawa na viwanja vingine nchini kimekuwa hakiendeshwi vizuri, hata kulitia alibu Taifa kwa huduma mbovu, ikiwemo ya kukatika kwa umeme kama ilivyotokea hivi karibuni wakati wa fainali za michuano ya Kombe la Kagame ambalo Tanzania ilikuwa mwenyeji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Viwanja vya Michezo ianzishwe. Serikali ianzishe Mamlaka ya Viwanja vya Michezo nchini na kuipa jukumu la kusimamia na kuendesha viwanja vyote vya michezo vilivypopo. Aidha, Mamlaka hiyo kwa kushirikiana na vyombo mbalimbali vya Serikali, ipewe jukumu la kuhakikisha kila mwaka inajenga Vituo vya Kisasa vya Mazoezi na Hosteli kwa ajili ya Wanamichezo, na angalau kiwanja kimoja kikubwa cha michezo chenye hadhi ya kimataifa inayolingana na hadhi ya Uwanja mpya wa Taifa uliopo Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa pendelezo hilo, baada ya miaka tisa, nchi yetu itakuwa na jumla ya viwanja 10 vya kimataifa. Mbali ya kuchochea maendeleo ya michezo nchini na kuajiri Watanzania wengi kutoa huduma mbalimbali, Viwanja hivi pia vitakuza hadhi ya nchi na kuiwezesha nchi kukidhi vigezo vya kuwa Mwenyeji wa michuano mikubwa ya kimataifa kama kuandaa Kombe la Mataifa ya Afrika (CHAN).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sanjari na mpango huo wa Ujenzi wa Viwanja vya Kisasa, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuweka lengo la kuhakikisha Tanzania inakuwa Mwenyeji wa Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ligi za Ndani (CHAN) mwaka 2018 na mwenyeji wa Kombe la Mataifa ya Afrika mwaka 2019. Aidha, Serikali iandae programu na kampeni kabambe ya kuhakikisha timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu (Taifa Stars) inaandaliwa vema na kupatiwa mechii nyingi na ngumu za kujipima nguvu, kwa ajili ya kuhakikisha inafuzu kuingia kwenye michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2014 iliyopangwa kufanyika nchini Brazil.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, viwanja vyote vya michezo, kama Uwanja wa Majimaji Songea, Sheikh Amri Abeid Arusha, Uwanja wa Jamhuri Morogoro, Uwanja wa Jamhuri Dodoma, ule unaoitwa Uwanja wa CCM Kirumba Mwanza na viwanja vingine vyote vilivymilikishwa kwa CCM, virejeshwe Serikalini na viwe chini ya Mamlaka ya Viwanja vya Michezo tunayotaka ianzishwe, ili viboreshwe na kutumika kwa maslahi ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala ya kutegemea tu vituo vya michezo vichache vilivyoanzishwa na sekta binafsi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iandae mpango wa kukuza vipaji vya wanamichezo wadogo kwa kuanzisha Vituo vya Michezo (*Sports Academy*) katika kila Halmashauri kwa kushirikiana na Mamlaka ya Viwanja vya Michezo tuliyopendekeza ianzishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hali mbaya ya sekta ya michezo nchini, bado zipo timu na wapo wachezaji ambao wamekuwa wajitutumua na kufanya vizuri kwenye ushindani wa kimataifa. Kambi Rasmi ya Upinzani inachukua fursa hii kuzipongeza timu za soka za Simba na Yanga kwa kufanikiwa kufika fainali ya Kombe la Kagame baada ya kuzitoa timu nyngine za Afrika Mashariki na Kat. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lugha ya Kiswahili na utamaduni wetu. Kuhusu maendeleo ya Kiswahili, Tanzania inasifika kwa kuongea Kiswahili fasaha, lakini leo ukiingia katika tovuti yeoyote duniani, ukiuliza Kiingereza utaambiwa asili yake ni Uingereza, Kifaransa asili yake Ufaransa, Kijapan asili yake Japan, Kijerumanzi asili yake Ujerumanzi, Kispainola asili yake Hispania, lakini unapoulima Kiswahili, wanasema asili yake ni Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu bora hutolewa kwa lugha ya Taifa inavyosemwa na karibu kila mtu na lugha hiyo hapa kwetu ni lugha ya Kiswahili. Kwa mujibu wa wataalamu na watafiti wa masuala ya lugha na maendeleo (Kwa mfano Prof. Kahigji), ni kwamba hakuna nchi yoyote Duniani ambayo imeendelea kwa lugha ya kukopa. Hivyo basi, Tanzania haiwezi kuendelea kwa kutumia lugha ya Kiingereza tuu katika kutoa elimu kwa vijana wetu kwa hiyo lugha zote mbili zitumike kikamilifu katika kufundishia. Hata hivyo, Kambi ya Upinzani tunapongeza taasisi zote ambazo zimeendelea kukikuza Kiswahili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tumeshindwa hata kulinda huu utamaduni wetu wa asili? Kwa sababu hata juhudi ambazo Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) wanazifanya kuendeleza Kiswahili duniani, zinaishia kutolisaidia Taifa kwa sababu ya mtazamo wa Serikali juu ya lugha ya kufundishia shule za sekondari na vyuo vya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa hotuba yako nzuri. Waheshimiwa Wabunge sasa tunaingia katika majadiliano, naomba niwataje watakaoanza asubuhi hii, tutaanza na Mheshimiwa Esther Bulaya, Mheshimiwa Abdallah Ameir, Mheshimiwa Mohamed Seif Khatib ajilandaye.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia ikizingatiwa mimi ni mdau muhimu, *by Profession* ni Mwandishi wa Habari lakini pia ni Mbunge wa Vijana, kwa hiyo Wizara hii inanihu vili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuwapongeza Waandishi wenzangu Tanzania nzima kwa kufanya kazi katika mazingira magumu, lakini bado warmeweza kutoa mchango wa kutoa elimu kwa wananchi wa Tanzania. Pia napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza vijana wote Tanzania kwa kuendelea kujitutumua kupigana na kukabiliana na ukata wa maisha unaowakabili kutokana na tatizo kubwa la ajira inayowakabili vijana wetu ambao ni asilimia sitini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza wajumbe wenzangu wa Kamati ya Utekelezaji wa Umoja wa Vijana Taifa kwa kuumiza kichwa na kufikiria ni kitu gani ambacho wanaweza kukianzisha kuleta suluhu ya matatizo yanayowakabili vijana wenzetu na kuamua kuanzisha Benki ya Vijana ambayo wenzetu wa Kambi ya Upinzani walikuwa wanaomba

Serikali, sasa sisi tayari Umoja wa Vijana tumeshaanzisha benki hiyo. Tunaomba tushirikiane ili vijana wote bila kujali itikadi yao ya vyama waweze kupata fursa ya kupata mikopo kwa bei nafuu. Hongera sana Kamati ya Utekelezaji ya Umoja wa Vijana na Baraza Kuu la Umoja wa Vijana Taifa. Naamini kabisa pia fursa hiyo ya mikopo watapata hata vijana wenzetu wa Igunga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa napenda kuanza kuchangia. Nianze kwa kumukuu Mheshimiwa Mbunge mwenzangu Zainab Kawawa wakati akichangia katika Hotuba ya Wizara ya Kazi alisema vijana ni bomu lingine ambalo linakuja. Ni kweli kabisa wakati Serikali inafikiri kushughulikia tatizo la migogoro ya wafanyakazi lakini vijana ni bomu kubwa linalokuja mbele. Vijana wengi hawana ajira na hii si kwa Tanzania peke yake ni kwa Afrika nzima na ndio maana Umoja wa Nchi za Afrika waliliona hilo na kuweka mikakati ya miaka 10 kuanzia mwaka 2009 mpaka 2019 kwamba ajenda ya vijana ni agenda muhimu na wengi sasa hivi wanaelekea kukata tamaa na ndio maana wanashiriki katika mageuzi kwenye nchi zao. Mlimi naomba Serikali iwe makini katika hili tusifike huko, tuwasikilize vijana tuweze kutatua matatizo yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali ya Tanzania kuwa ya tatu Afrika katika kuzalisha dhahabu lakini nasikitika kwamba sekta hii ya madini haijatoa mchango mkubwa wala haijatoa ufumbuzi wa kumaliza tatizo la umaskini kwa vijana. Mbali na vijana wachache ambao wananaufaika na sekta ya madini labda kwa kuwa na ma-Godfather kwenye migodi lakini bado vijana wengi wanaofanya kazi kwenye migodi wanafanya kazi kama vibarua, hawajui hatma yao ya kesho ikoje lakini pia hata hawa wachimbaji wadogo hawajawezeshwa vya kutosha ambao wengi wao ni vijana kuweza kumudu gharama za vifaa vya uchimbaji wala kumiliki migodi ya nchi yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya madini, vijana wenzetu wamekuwa watazamaji wa kuona tu madini yanachukuliwa na kwenda nchi zingine. Sasa angalizo langu kwa Serikali kwa sababu tayari sekta ya madini imeshindwa kutoa mchango mkubwa wa kumaliza umaskini kwa vijana na kutatuta tatizo la ajira, sekta muhimu ambayo itamaliza tatizo hili ni kilimo. Naomba pia vijana wasije wakawa manamba katika ardhi yao. Asilimia 80 ya Watanzania wanapata ajira katika sekta ya kilimo. Sasa Wizara hii ya Vijana imejipanga vipi kuhakikisha vijana wananaufaika na sekta ya kilimo? Wakati Waziri wa Fedha anawasilisha bajeti yake alielezea mikakati mbalimbali ya Tanzania kuwa na mageuzi ya kilimo na kuwezesha kulisha dunia, *fine*, sina tatizo nalo lakini je, Wizara hii ambayo naamini ndio *coordinator* ya Wizara mbalimbali katika *issue* zinazowahusu vijana imejipanga vipi kuhakikisha vijana wenzetu watanufaika katika sekta ya kilimo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napitia vitabu mbalimbali kuna hekta milioni 25 ambazo zinatafaa katika kilimo cha umwagiliaji, je, Wizara imejipanga vipi kuhakikisha vijana wenzetu watawezeshe ili na wenye kwenye sekta ya kilimo. Waziri Mkullo hapa alishatuambia kwamba tutafanya Mapinduzi ya kilimo na watashirikiana na wawekezaji mbalimbali kwa kugharimu mabilioni ya dola. Tayari tumeshashuhudia kuna baadhi ya maeneo yameshaanza kutengwa kwa ajili ya kuwekeza kwenye sekta ya kilimo. Tunaomba na hili nalo vijana wasiwe watazamaji kuangalia ardhi yao tu inaondoka na hawafaidiki nayo. Namwombwa Mheshimiwa Waziri awe *coordinator* mzuri kwa *issues* zinazowahusu vijana katika Wizara zote. Kilimo sasa hivi ndio itakuwa mkombozi wa vijana wasiwe wanaimba tu kauli ya Kilimo Kwanza halafu hawanufaiki nayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa vijana asilimia 60 ndio wanaotengeneza asilimia 14.4 ya watu wasiokuwa na ajira Tanzania, naomba sana tuwasaidie vijana wenzetu wasikate tamaa,

wasije kupoteza matumizi kabisa na Serikali yao kwamba haiwajali. Wamekosa fursa katika sekta ya ya madini, wapate fursa katika sekta ya kilimo, waweze kujajiri wenyewe ili waweze kuondoa umaskini unaowakabili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nzungumzie *profession* yangu ya habari. Tumekuwa tukiwategemea sana Waandishi wa Habari katika mambo yetu mbalimbali. Nashukuru hapa leo nasema wazi hizi pande mbili zote zinamiliki *media*. Upande wa *Opposition* na Serikali lakini bado wanashindwa kuboresha maslahi ya Waandishi wa Habari. Inasikitisha na inatia aibu humu ndani tunakuwa tunajidai kupigania haki za watu lakini watu tunaowaajiri, Waandishi wa Habari tunawanyonya kwa sababu wao wenyewe hawawezi kujitetea. Si vizuri tukawa tunajinafikisha humu ndani wakati Waandishi kwenye vyombo vyetu hatuwalipi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha eti Mwandishi analipwa shilingi 1000 kwa *story*. Asilimia 80 ya Waandishi waliokuwepo kwenye vyombo vyetu habari ni *corresponded*, wanalipwa kutokana habari. Labda kwa wiki akijitahidi ataandika habari 100 lakini zitatoka mbili, kwa hiyo, kwa wiki ana shilingi 2000 tunakwenda wapi, halafu baadaye tunasema wawe wazalendo wawe wazalendo hata maslahi yao hatuwaboreshei? Naomba Mheshimiwa Waziri alichukue hilo na sisi tuliomo humu ndani tunaomiliki vyombo vyetu habari tuache unafiki, tuwalipe vizuri Waandishi wa Habari. Tuache kuwatumia kwa maslahi yetu binafsi, tuwalipe vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwaomba Waandishi wa Habari wenzangu, tupo kwenye Mfumo wa Vyama Vingi na tunajua kila mtu ana mapenzi ya Chama chake lakini tutende *fair*. Tutumie *ethics* zetu zinavyosema, tuandike habari zilizo sahihi bila kujali itikadi zetu na zitakazotoa elimu kwa umma hata kama wewe haikufurahishi, lakini tulitendee haki Taifa hili tuwe wazalendo, tutende haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuzungumzia Timu ya Taifa ya Wanawake, imesahaaulika. Hapa sasa ndipo tunapoona unyanyasaji wa Kijinsia, Timu ya Twiga Stars. Hii timu haipewi hadhi kama Timu ya Taifa, haipewi hadhi kama jinsi inavyopewa hadhi Timu ya Mpira wa Miguu (*Taifa Stars*). Timu ya *Taifa Stars* imekuwa ikelelewa kama yai, *Twiga Stars* inalelewa kama jiwe, siyo haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Timu ya *Twiga Stars* mbali na matatizo yote waliyokuwa nayo, wamekuwa wakifanya mazoezi kwenye mazingira magumu *sometimes* wanakosa hata maji mazoezi eti timu ya Taifa ya Wanawake na wanajitahidi. Tumeona mwaka jana wameshiriki Michuano ya Mpira wa Miguu ya Wanawake Afrika lakini mwaka huu wameshiriki COSAFA na pia walishika nafasi ya tatu na wamepata fursa kushiriki Michuano ya *All African Game* ambayo itaraja kuanzia mwezi Septemba lakini maandalizi duni, timu hii inafanya mazoezi katika mazingira magumu. Hapa hata tukiuliza maandalizi yake yakoje hatujui lakini watoto wa watu wana-struggle kwa ajili ya Taifa hili. Wanafanya mazoezi katika mazingira magumu mpaka kuna Mmarekani mmoja ameandaa *DVD*, anaitwa Nishal Legal ameellezea *the way Twiga Stars* inavyofanya mazoezi katika mazingira magumu mbali ya kuipa heshima Taifa letu. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, atupie macho Timu hii ya Taifa ya Wanawake hata kama *TF* wanamuongopea, namshauri afanye *research*, naamini ana uwezo huo wa kupata taarifa sahihi ili tuisaidie timu hii tusi-base kwa *Taifa Stars* ambayo *sometimes* inaboronga, tuisaidie Timu ya *Twiga Stars*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kujua wana mikakati gani ya kuibua soko la wanawake. Tunaona tu Kopa Cocacola lakini je, kwa upande wa timu ya wanawake kuibua wachezaji wa mpira wa miguu wa kike ukoje? Kule kwetu Tarime kuna timu nzuri tu ya wanawake lakini sijasikia mikakati yoyote ya Serikali ya kuendeleza soko la wanawake Tanzania. Namwomba Mheshimiwa Waziri waache kuwanyanyapaa wanawake na unyanyapaa huu umeanza kwenye Timu ya Twiga Stars.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia kwenye Hotuba, mbele yake kuna Timu ya Taifa ya *Taifa Stars*, nilitegemea hata huku upande wa nyuma ingekuwepo Timu ya *Twiga Stars*. Mheshimiwa Waziri Waziri nakuomba, dada yangu Mheshimiwa Naibu Waziri timu hii ya Twiga

iangaliwe. Tena nashukuru hii Wizara yote ime-*balance gender*. Kwa hiyo, naomba sana muisaidie Timu ya Taifa ya Wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *issue* ya wasanii imezungumzwa sana na hawa ni vijana wenzetu na nashukuru Kambi ya Upinzani kwa wazo lake la shughuli ya kusimamia kazi za wasanii zihamie Wizara ya Habari na mimi hilo naliafiki kabisa. Wasanii wetu wamechoka, wanatumia muda mwangi kutunga nyimbo lakini hawathaminiwi. Fedha wanazopipata haziendani kabisa na kazi zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja lakini niliyosema naomba yazingatiwe. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Kabla sijamwita mse maji anayefuata, naomba Idara ya *Hansard*, Hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani muichukue kama ilivyokuwa kwa sababu hakuweza kuimaliza. (*Makofii*)

**MHE. ABDALLAH SHARIA AMEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona na kunipa nafasi kuzungumza katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mara ya kwanza kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia mimi kuwa Mbunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Jimbo la Dimani kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitaongelea zaidi katika suala zima la mchezo wa mpira wa miguu kwa sababu kama mnavyofahamu mimi ni mdau mkubwa wa mchezo wa mpira wa miguu. Kule Zanzibar nilikuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mpira wa Miguu kwa miaka 12 na zaidi. Kwa maana hiyo, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kutoa hotuba yake nzuri ambayo inaweza kutekelezeka ndani ya miaka mitano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpira ni fedha na bila ya fedha huwezi kuwa na mpira. Tukiangalia juzi hapa tulikuwa tuna Mashindano ya Kagame, kwa kweli tukiangalia kwa undani fedha zilitumika zaidi hasa kwa timu zote za Tanzania ambazo ziliweza kuingia katika hatua ya fainali na hatimaye timu yetu ya Yanga ya Dar es Salaam kuwa Mabingwa wa Kombe la Kagera lakini nasema fedha zilitumika, Yanga imesajili wachezaji wengi hasa Asamoo kutoka Ghana. Kwa hiyo, nachotaka kusema, Serikali naiomba sana ipange bajeti madhubuti kabisa ambayo itasimamia mpira huu wa miguu wa Tanzania ili tuweze kuondokana na aibu ambayo tulipata juzi, timu yetu ya Taifa imeshindwa kwenda Sudan na yote hii inatokana na ukosefu wa fedha. Sasa nadhani Serikali itakapokuwa ina bajeti nzuri, ina uhusiano na mambo ya michezo basi tutawenza kufanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ifanye mambo haya yafuatayo ili kuweza kuinua mpira wetu wa miguu Tanzania. Kwanza, Wizara ya Michezo ishirikiane na Wizara ambayo inahusika na mambo ya viwanja tuhakikisha kwamba kila sehemu ambayo inatolewa viwanja kwa ajili ya makazi ya wanadamu basi kuwe na viwanja vyta michezo. Viwanja hivi vyta michezo si kwamba viwepo tu na Serikali iweze kuvisimamia ipasavyo. Kwa sababu kama vitakuwa vimetengenezwa viwanja lakini havikusimamiwa vizuri na Serikali watatokea wajanja wachache kuweza kuvitumia na kufanya mambo yao ambayo wanayahitaji. Mfano mzuri ni Uwanja wa Jangwani, kuna eneo ambalo limezingirwa sasa hivi watu wanataka kulitumia kwa manufaa yao ambalo ni eneo kwa ajili ya michezo lakini kwa makusudi watu kwa ubinagsi wao wanataka kulitumia kwa manufaa yao. Kwa hiyo, naomba Serikali ianzishe viwanja vyta michezo kila sehemu zilizopimwa na isimamie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, kipindi cha nyuma Zanzibar kulikuwa kuna maduka ya michezo ambayo yanahudumiwa na Serikali yenye. Sasa naiomba sana Wizara wetu ianzishe Mfuko Maalum wa kuanzisha maduka ya michezo na yasambazwe katika kila Wilaya ili kuhakikisha kuwe na unafuu wa vifaa vyta michezo na upatikanaji wake uwe katika kila Wilaya na waweze kuvimudu kwa bei rahisi zaidi. Kwa hiyo, naiomba Serikali kupitia Wizara yetu basi ianzishe

maduka ya vifaa vya michezo katika kila Wilaya kwa ajili ya kupata vifaa vya michezo vya mpira wa miguu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ambalo nataka kulichangia katika kuendeleza mpira wetu wa miguu Tanzania, mashulenii ndio chimbuko letu la michezo. Kama ni chimbuko letu na tunaamini kwamba mashulenii tunatoa vipaji vizuri vya wanamichezo basi kuanzishwe somo maalum la michezo katika shule na wapatikane Walimu ambaa wanaweza kufundisha masomo ya michezo katika shule zetu ili kuweza kuibua vipaji ambavyo vitawezza kusaidia kukuza mchezo wetu wa mpira wa miguu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niondoke hapo niende kwenye *TFF*, Chama chetu cha Mpira Tanzania kifanyi haya yafuatayo. Moja, kuanzisha *academy* na *academy* hizi ziwe zinasimamiwa na Chama chenyewe cha michezo siyo kuanzishwe *academy* halafu baadaye ziachiwe huru. Ndani ya *academy* basi kuwe na Sheria ndogondogo ambazo zitawezza kuwabana wale ambaa wanawatamani wachezaji wadogo wawe na utaratibu maalum wa kuweza kuwachukua na kuweza kuwatumia ili faida ziweze kusatikana katika sehemu zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo naliomba kwa *TFF*, makocha kama walivyosema Kambi ya Upinzani, tuna makocha wazuri wa Tanzania ambaa wanaweza kufundisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatumia hela nyingi zaidi kuwachukua makocha wa nje ambaa wazalendo wako hapa ambaa wanaweza kutumia hela ndogo tu na wakaweza kufanya kazi vizuri kama alivyotoa ndugu yangu hapa, akina Julio ni kocha mzuri na amefanya kazi nzuri sana ya kuweza kuitangaza Tanzania katika mashindano mbalimbali. Kwa hiyo, hawa ni makocha ambaa tunawahitaji tuwaenzi, tuwaenzi kabisa waweze kuendeleza vipaji vya watoto wetu. (*Makofii*)

Kama walivyosema wenzangu kwamba ni lazima makocha watakaokuja kutoka nje, basi ni vizuri zaidi wale tukawatumia kuwafundisha makocha wetu wa Tanzania. Halafu baadaye watakapoondoka, basi wanaacha hazina siyo wanaondoka na utamu wao, hapana. Wanaondoka, lakini wanatuachia hekima ambayo tunaweza tukaitumia siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niondoke hapo, niende katika *TFF* na *ZFA*. Kwa kweli nashukuru sana uhusiano uliokuwepo kati ya *TFF* na *ZFA* Zanzibar katika muda mrefu na ushirikiano ambaa umetoka katika kuhakikisha kwamba Zanzibar nayo inakuwa mwanachama wa *FIFA*. Lakini bila ya Zanzibar, hakuna Tanzania. Zanzibar ndiyo inayofanya kuwe na Tanzania. Lakini muda wote ambaa nilikuwa nimeweza kufanya kazi ndani ya *ZFA* Zanzibar, sijaona ruzuku hata moja ambayo imetokea *TFF* kwenda *ZFA* katika kuisaidia. Ile ruzuku inayotoka *FIFA* ni ruzuku ya Tanzania na kama ni ruzuku ya Tanzania na Zanzibar nayo wanayo haki waweze kuipata. (*Makofii*)

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja, atuelezee: Je, anaelewa nini? *TFF* inapata ruzuku gani kutoka *FIFA*? Je, *ZFA* inakuwa inagawiwa katika mfumo gani kama ipo haki ya kuweza kugawiwa? Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja, hili naomba atuelezee ili tuweze kufahamu: Je, *ZFA* inakuwa ina haki ya kuweza kupata fungu kutoka *FIFA* ambayo imepitia *TFF* au fungu lolote liko ndani ya *TFF* peke yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda sana kuwapongeza sana wananchi wangu wa Dimani kwa kunichagua mimi kuwa Mbunge na ninawaahidi kwamba sitawaangusha katika kipindi cha miaka mitano. Baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Asante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Abdallah Sharia. Naomba kumwita sasa Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Mheshimiwa Alhaj Mohamed Missanga ajiandae na Mheshimiwa Mariam Kasembe atafuatia. Mheshimiwa Mohammed.

**MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa heshima hii na mimi kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama tangu uchaguzi mkuu kumalizika, ningeomba nichukue nafasi hii kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Uzini Zanzibar kwa

kunichagua kuwa Mbunge wao kwa mara nyingine tena kwa kura za kishindo. Mimi naahidi kwamba nitajitahidi kuwasaidia na kuwapa matumaini yao katika muda ujao. (*Makofi*)

Pili, ningependa niwashukuru sana Madaktari wa hapa Dodoma, madaktari wa Muhimbili na madaktari wa Hydrabadi kule India kwa kunisaidia pale nilipokuwa na matatizo ya kiafya. Nimerejea mzima na salama kabisa. Nawaambia ndugu zangu wa Uzini bado mzima na naweza kuwatumikia kwa nguvu zangu zote kabisa. Nawashukuru sana. Mwisko, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Nchimbi kwa hotuba yake nzuri na nimefarijika kuona kwamba wakati mimi Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana mwaka 1977/1988 yeche aliwa chipukizi. Baadaye akaja kuchukua nafasi yangu ya Uenyekiti. Nilipokuwa Waziri wake wa Wizara ya Habari na Utamaduni akawa Naibu wangu. Sasa ni Waziri wa Habari. Hongera sana kwa kunifuata nyuma. Endelea sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni ishara kwamba vijana wa Tanzania wale ambao wanalelewa na chama wana nafasi nzuri katika uongozi katika nchi hii na Nchimbi naona ni mfano nzuri. Kwa hiyo vijana, endeleeni kukitumia chama chenu. Asanteni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazungumzo yangu yatakuwa katika maeneo matatu. Suala la Uandishi, michezo na suala la lugha ya Taifa. Uandishi wa habari ni taaluma. Ni lazima mtu asomee, hata kama una kalamu yako nzuri ya *Perker* lazima uende chuoni ukasome. Uandishi wa habari siyo kazi ya wale ambayo wamekosa kazi, ndio waende kwenye habari. Maana yake kuna mazoea kwamba kama umekosa kwenda shulenii basi, kachukue uandishi wa habari. Maana unapata makanjanja huko! Kwa sababu watu wanakwenda kule bila kukusudia kwa sababu hawana kazi nyingine.

Ni vyema wafuate maadili ya uandishi. Uandishi wa habari pia ni maadili. Kuna maadili ya uandishi wenye na maadili ya Taifa. Kwa hiyo, nashauri waandishi wa habari wafuate maadili ya uandishi wa habari, maadili ya Taifa na pia uzalendo. Mimi naangalia televisheni mara nyingi sana, na suaona hata siku moja maiti wa maaskari wa Marekani, siyo kama hawafi, wanakufa, Iraq, Pakistan, lakini hawaonyeshi. Lakini hapa utaona waandishi wetu wapiga picha, wanaonyesha maiti, watu hali zao mbaya kabisa. Sidhani kama ni uzalendo ule. Lazima tujizie, mambo mengine hayafai kuonyesha katika hadhara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uandishi wa habari siyo umbeya wala uzushi. Kwa hiyo, siyo fahari kwamba wewe hodari kuandika umbeya na uzushi. Kila mtu ana haki ya faragha zake. Kwa hiyo, naomba waandishi wa habari fuateni maadili, andikeni habari, msiandike umbeya na uzushi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa uchaguzi hapa Tanzania, waandishi wa habari huwa wanununiliwa na wanasiasa na kuwa vibaraka wao ili wawasemee wao. Hii siyo uandishi wa habari mzuri. Mimi nashauri Serikali iwe na mpango kwamba kila wakati wa uchaguzi vyombo vya habari vijisajili vyenyewe kwamba mimi kipindi hiki nitasaidia chama cha *CHADEMA* ili tuwajue. Mimi *CUF* ni kadhalika. Ndivyo wanavyofanya Marekani. Marekani unajua kabisa kwamba gazeti fulani linaunga mkono chama kadhaa. Tufanye hivyo ili kupunguza unaafiki ulioko katika baadhi ya waandishi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasema kwamba hili ni muhimu sana kwa waandishi wa habari kwamba wajitambulise wao kwamba wanafanya nini. Nilikuwa namsikiliza Msemaji wa Upinzani, rafiki yangu, akizungumza kuhusu gazeti la *Daily News*. Mimi nafikiri lile ni gazeti moja ambalo linifuata maadili ya uandishi ni *Daily News*. Nina heshima kubwa sana hapa nchini na nje ya nchi yetu. (*Makofi*)

Yule mhariri alisema kwamba Dkt. Slaa hatashinda, ametabiri tu na utabiri siyo vibaya kutabiri. Mtu kama kasema hivyo, kama safari hii Dkt. Slaa hatashinda, katabiri. Pia siyo vibaya kwa mwandishi wa habari kutabiri. Pili, niende kwenye michezo. Michezo, ni sehemu nyingine ambayo inazungumzia kwamba michezo ni furaha. Hakuna mtu ambaye hana michezo aupendao, kuna wa faragha na dhahiri. Kuna kukaa kitako na kusimama na kukimbia, kila mmoja ana michezo wake. Kwa hiyo, michezo ni furaha kwa kila mtu na michezo ni afya na afya maana

yake, unapunguza gharama ya kwenda hospitali. Afya maana yake unafanya kazi vizuri kazini kwako. Michezo pia ni ajira. Michezo ni itifaki na michezo pia inaleta amani na umoja na utulivu. Kwa hiyo, michezo ni muhimu sana kwamba ipate nafasi katika nchi yetu tuendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michezo katika Tanzania, nafikiri kuna haja ya Serikali kuiendeleza kwa kuwekeza. Bila kuwekeza michezo haiwezi kuendelea. Lazima tu-invest kwenye michezo ili tuendelee. Bila hivyo, hatuwezi kuendelea. Kuwekeza wapi? Tutaanza kwenye maeneo mbalimbali. Kwa mfano, kuwekeza katika viwanja vya michezo, na siyo kwenye kiwanja cha Taifa tu, lakini viwanja vyote vya Mikoa viwekezwe ili michezo ipate kuendelea zaidi. Pia michezo usiwe mmoja tu katika riadha na kadhalika. Tuwekeze katika kutafuta walimu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa namsikia Mheshimiwa Mbunge mwenzangu hapa, nafikiri siyo busara kwa sababu ni Mswahili tu, basi anakuwa kocha wa Taifa, hapana. Michezo ni sayansi. Lazima awe na ujuzi. Tusidhanie kwamba lazima awe ni Mswahili, hata Wazungu wanachukua kila mahali.

Kwa hiyo, nasema michezo ni sayansi, lazima tuwapate wataalamu wenyewe kujua michezo, siyo kwa sababu alicheza mpira zamani na kadhalika. Wakati wao walicheza mpira kulikuwa na *formation* ya mpira ikiitwa *WM*. Sasa kuna *four to four*, haiwezekani kabisa. Kucheza mpira wa miguu chini, sasa watu wanacheza na viatu. Kwa hiyo, wakati umebadilika kabisa, kuna sayansi, kuna televisheni na kadhalika. Kwa hiyo, ni lazima tutafute waalimu wanaofanana na wakati huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea kuhusu michezo pia vifaa. Bila vifaa hatuwezi kucheza. Lazima Serikali isaidie kwa vifaa vya bei rahisi ili wanamichezo wawe na vifaa. Kuwe na mipango bora vya wanamichezo. Mimi nilikuwa Waziri pale na Bwana Nchimbi anakumbuka na Bendera. Hali mbaya sana kwenye vyama vya michezo ni mbaya sana, sijui mpaka leo ni vipi. Kwa hiyo, lazima viongozi wa michezo wapate taaluma, wajifunze kazi kwa ufanisi mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria za Michezo lazima zifundishwe. Chimbuko bora la wachezaji bora lazima tuwe na mahali ambapo pana chemchemi ya kupata wachezaji bora. Mnipata wapi? Nashauri, moja ni majeshi. Majeshi ni sehemu kubwa ya kuwapata wachezaji bora. Wachezaji bora wa zamani walikuwa wakikimbia mbio katika majeshi. Kwa hiyo, lazima tuzungumze nao tuwasaidie, tuwape vifaa ili watutolee wachezaji bora katika Taifa letu.

Eneo la pili, ni viwanda. Zamani tulikuwa na viwanda na makampuni kama *TPC*, Bandari na kadhalika. Sasa hakuna. Humu tulipata wachezaji bora zaidi. Eneo la tatu, ni Shule za *Primary, Secondary* na *Vyuo na Vyuo Vikuu*. Sasa tunafanya michezo, lakini siyo kama zamani, hata kidogo. Kuna haja ya kuona njia zaidi kutafuta vijana katika Shule za *Msingi* na Shule za *Sekondari*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni vilabu. Vilabu vikubwa vinabaki kutafuta wachezaji bora tu, lakini hawaandai wenywewe. Lazima Sheria ile ya *TFF* zamani kwamba lazima kila klubu iwe na timu yake ya vijana iwe ni lazima, bila hivyo wasiingizwe katika mashindano. Bila hivyo watapata wapi wachezaji? Kwa hiyo, sasa pengine ni vilabu vyenyewe vijitahiji kufanya hivyo. Lakini pia kuwe na shule za michezo *academy*. Mimi siamini kwamba *TFF* wanawenza kufanya hivyo. Lakini vilabu wafanye hivyo. Watu binafsi wafanye hivyo ili tuwe na mtandao mkubwa wa wachezaji kutoka sehemu mbalimbali, bila hivyo hatushindi. Nchi zote za *West Africa* zinafanikiwa kwa sababu wanazo *academy*. Mimi nilikwenda kule na ninajua.

Pia *TFF* iunde chombo maalum cha kuendesha mashindano ya vijana ya miaka 15, 17, 19 na 21. Bila hivyo, bila na mashindano ya vijana Watanzania, itakuwa kichwa cha mwenda wazimu kila siku. Vilabu navyo pia lazima vipewe nafasi hiyo. Riadha ni michezo ambaa hauna gharama kubwa sana, kwa sababu wanakimbia mmoja mmoja tu. Kwenye mpira wa miguu wako 11. Lakini mbio ni mtu mmoja tu basi. Rahisi kuicheza michezo huo. Ningemshauri Mheshimiwa Nchimbi, mimi nilikuwa pale, Waziri wako nilitaka kwenda Kenya na Ethiopia kujifunza, kwa nini wanatushinda watu hawa? Kwa nini? Mimi ningeshauri kwamba tafuta timu yako uende Kenya na Ethiopia ukaone kwa nini wanatupita watu hawa jirani zetu kwenye riadha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpira wa miguu mwaka 2005 kiwango cha *FIFA* tulikuwa 175. Mwaka 2007 tulipanda mpaka kufika 89. Leo nafikiri tuko 128. Kwa nini? Kwa nini tunaporomoka? Tunaporoka kwa nini? Tujitahidi kwa sababu hii ni heshima kubwa sana. Hatukuwahi hata mara moja kufika fainali la Kombe la Afrika toka mwaka elfu moja na thelathini mpaka leo hatukuwahi kuingia katika Kombe la Dunia. Kwa nini? Tujilize. Tuache ushabiki huu wa Usimba na Uyanga hapa! Twende mbele! Mpira sijui Simba na Yanga tu! Lazima tujitahidi tutoke hapa tulipo. Mimi nafikiri kuna tatizo kubwa sana. Lazima Serikali ije na mpango kabambe kuona ni namna gani tunaweza kuuendeleza mpira wa miguu ambao unapendwa na watu wengi sana duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kombe la Dunia linaangaliwa na watu zaidi ya bilioni 26. Wananchi wengi wanapenda mpira wa miguu, tunawakera Watanzania. Tunawaudhi Watanzania kwa sababu hatuuendelezi mpira wa miguu. Ningeshauri Serikali kuchukua hatua ya kufanya hivyo. Bado nina dakika tano.

**MWENYEKITI:** Ni ya pili hiyo. Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB:** Aaah, Basi bwana.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Naomba kumwita sasa Alhaj Mohamed Missanga na Mheshimiwa Mariam Kasembe ajiandae.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukushukuru sana kwa kunipa nafasi mapema tu kuchangia katika hoja hii muhimu. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Nchimbi pamoja Naibu wake, Katibu Mkuu na wote wanaoshiriki katika Wizara hii kwa maandalizi mazuri ya hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya habari, mimi sitaki kujikita sana kwa sababu wako wenyewe na bahati nzuri Mheshimiwa Mohammed Seif yeche ni mtaalam, amesema mambo ya vijana wako, Mheshimiwa Esther kazungumza vizuri. Mambo ya sanaa wako wenyewe, akina Mr. Sugu. Kwa hiyo, mimi sitaki kuingia sana huko. Mimi naomba nijikite kwenye michezo. Nikipata nafasi, nitazungumza mambo ya Netiboli na *football* na riadha. Naomba nianze na netiboli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu katika netiboli kulikuwa na utulivu na amani, michezo ambao uliendeshwa vizuri bila migogoro, bila matatizo yoyote kwa muda mrefu sana. Lakini hivi karibuni kumezuka tatizo katika netiboli. Umezuka mgogoro ambao umesabisha Katibu Mkuu wa Chama hiki Ana Kibira kusimamishwa kuwa Katibu Mkuu toka mwezi Agosti, 2009. Nilipofuutilia sababu za msingi ambazo zimemfanya Ana au Katibu Mkuu huyu asimamishwe, kwa kweli mimi nimeona ni mambo ya hovyo hovyo tu, wala hakuna jambo la msingi. Kwa sababu, naambiwa msingi wa kumsimamisha ni kwa sababu eti ame-side na *CHANEZA* au wenzetu wa netiboli wa upande wa Zanzibar katika kudumisha mashirikiano na mahusiano mazuri kati ya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani juu ya kuendeleza michezo wa netiboli, jambo ambalo siku zote hapa tunasisitiza habari ya kuimarisha Muungano na hivi ni vyombo vya kuendeleza Muungano.

Sasa mwenzetu huyu ambaye anatekeleza azma ya kudumisha Muungano kwa utaratibu huu kwenye *CHANETA* na kujaribu kushirikiana na viongozi wetu wa Zanzibar wa *CHANEZA* aonekane kuwa ni mtovu wa nidhamu, kwa nini ame-side na Wanzibar? Au kwa nini anataka kushirikiana vizuri na Wazanzibar? Kwa nini anakuwa karibu na *CHANEZA*? Mimi nasikitika sana.

Kama kweli sababu ni hiyo na siku zote hapa tunazungumzia habari ya kudumisha Muungano, mimi nadhani bibi huyu hakutendewa haki. Kinachonisikitisha zaidi kwamba toka mwaka huo wa 2009 Baraza la Michezo lipo, limeshindwa kutatua, Wizara yenyewe ipo, imeshindwa kutatua. Kweli Baraza limeshindwa kutatua mgogoro huu mpaka sasa ni miaka takribani miwili, huyu binti wa watu kasimamishwa kwa sababu ambazo hazina msingi wowote. Hili linasikitisha, ningependa maelezo ya Mheshimiwa Waziri atakapokuwa ana-sum up. Lakini kwa sababu Baraza wameshindwa na Wizara imeshindwa, nimwombe Mheshimiwa Mwenyekiti Jenista Mhagama na ndugu yangu Juma Nkamia kama Makamu Mwenyekiti, wachukie hili, waunde

Kamati, watafute kwa nini hili tatizo lipo na wafanye jitihada ili limalizike na huyu Katibu Mkuu arudishwe kwenye nafasi yake. (*Makof*)

Wacha sisi tulichukue Kibunge, maana Wizara wameshindwa na Baraza wameshindwa. Wacha sisi katika nafasi yetu kwa kutumia Kamati yetu, na Mheshimiwa Nkamia waifanye hiyo kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *football* nina kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Tenga kwa kazi nzuri ambayo anaifanya toka ameingia kwenye uongozi wa *TFF*, amefanya mambo mengi sana. Najua changamoto zipo. Najua mapungufu yapo, lakini ukweli nasema amefanya kazi nzuri na yako mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma, mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Utendaji wa *FAT Taifa*, kwa hiyo, nayafahamu. Sisi tulipokuwa pale, ukilinganisha na sasa yako mafanikio mengi tu. Kwa mfano, ratiba na kalenda ya *football* sasa hivi unakwenda sambamba na *FIFA* kiulimwengu mzima. Mashindano ya kirafiki, haya mashindano rasmi ya klubu, *friendly matches*, yote haya sasa hivi tunakwenda *in line* na wenzetu wa *FIFA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini toka ameingia Tenga, moja ya *problem* ambayo ilikuwepo ni kwamba, kulikuwa hakuna imani kwa Chama cha Mpira kutoka kwa Wafadhili na Wahisani, na matokeo yake tulikuwa hatupati ufadhili wala uhisani kwenye Chama cha Mpira. Leo wewe ni shahidi Mheshimiwa Mwenyekiti kwamba, *TFF* wamejenga imani kwa wafadhili kiasi kwamba, *TFF* wanapata ufadhili mzuri sana kutoka katika vyombo mbalimbali.

*NMB* wanafadhili, *TBL* wanafadhili, *Vodacom* wanafadhili, hawa wasingejuja kama wangekuwa na wasiwasi kwamba, fedha zao hizi wanazotoa, basi zinapunjwa hivi. Ni kazi ambayo imefanywa na Mheshimiwa Tenga na Kamati yake ya Utendaji. Naomba nipongeze sana kwa mafanikio haya ambayo wameyapata na ninaomba uniruhusu vilevile niwapongeze sana *TBL*, niwapongeze sana *Vodacom* na niwapongeze sana *NMB* kwa kuthubutu kufadhili masuala ya mpira ambayo hata kama unavyoona kwenye *Kagame Cup* iliyopita, basi ufadhili wao ndio umesababisha Tanzania tukaweza kushiriki na alhamdulillah, Yanga wakawa mabingwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile huko nyuma kulikuwa na migogoro mingi katika *TFF* au katika *FAT*. Leo wewe mwenyewe unaona, hata magazeti siku hizi hayaandiki tena mambo hayo. Ni kazi nzuri ambayo imefanywa na Mheshimiwa Tenga. Lakini kama alivyosema Mheshimiwa Mohamed Seif, tulifika namba ya 89 mwaka 2009 kama nipo sawasawa, ye ye amesema mwaka 2007, lakini nipo tayari kuwa *corrected* kati ya mwaka 2007 na 2009 tulifika namba mbili (*two digits*), namba ya 89 katika ubora katika ulimwengu, 89 sio kazi ndogo hiyo, chini ya kazi nzuri ambayo imefanywa na wenzetu hawa. Sasa tumeoporomoka tuko 123, 127, 129, vyovoyote itakavyokuwa lakini tumeshuka chini, lakini awali tulifika mahali pazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasema kwa *TFF* mimi naomba niwapongeze, lakini niwaombe changamoto zilizopo waziangalie. Moja ya changamoto waliyonayo, kwa kweli wazungumze na waamuzi. Yako malalmiko mengi sana kwa timu zetu za mpira wakilalamika. Timu A, timu B, timu C, mimi sitaki kuwataja, lakini kimsingi yako malalamiko mengi ya waamuzi, ningeomba sana *TFF* waliangalie hili kwa sababu linaweza likaharibu sifa nzuri hii ambayo ninajaribu kuieleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mohamed Seif, amezungumza vizuri. Changamoto waliyonayo ni kukazania timu za vijana, klubu zetu hizi ziwe na timu za viajana. Haya mambo ya kusajili sijui kutoka wapi, kutoka wapi, mambo ya kuanza kushutumiana siyo mazuri. Lakini kama wana timu nzuri za vijana, kama ambavyo ilikuwa miaka ya nyuma ile miaka ya 1960 na 1970 akina Kocha Victor Stansilaus alivyokuja hapa kutoka Romania na Simba wenzetu walimleta mwingine, mambo yalikuwa mazuri. Kwa hiyo, tuimarishe timu zetu za vijana, *Footbal Academy* zetu tuzifungue na tuziimarishe. Hapa naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza la Michezo - Mheshimiwa Kipingu, ni mfano mzuri kwa kusimamia soka la vijana, amekuwa

na *Academy* yake, huyu ndiye mtu wa kuungwa mkono ili kusudi vijana wetu waweze kufanya vizuri. Huko ndiko ambako kutawenza kutusaidia sisi tuweze kupata matokeo mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako malalamiko kuhusu makato ya 20% ya Uwanja wa Taifa. Vilabu vinalalamika sana, unatangaza pale umepata shilingi milioni 400 lakini klubo inaondoka na Shilingi milioni 100 na kadhalika. Kwa hiyo, yako malalamiko mengi. Nadhani ni vizuri kuliangalia hilo ili kusudi kusaidia vilabu vyetu hivi viweze kupata chochote kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usalama Uwanja wa Taifa, hali sio nzuri. Pale *VIP* ngazi ya kuteremka ni moja, *lift* ile haifanyi kazi. Ikitokea dharura kama iliyotokea juzi, jamaa walipigwa bao, wamekasirika wamezima taa, basi inakuwa ni vurugu tu! Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, uliangalie hili kwamba, ni lazima kwa kweli ile *lift* ifanye kazi na kama kuna njia nyingine, au *control* ya wale walioingilia milango mingine wasilazimike kuja pale kwenye ule mlango wa *VIP* ambaao kidogo unakuwa na matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa riadha, tarehe 13 July, niliuliza swali hapa na nikasema yale ambayo Mheshimiwa Mohamed Seif amesema, twende Kenya tukajifunze wenzetu wanafanya nini kwa sababu, mazingira yetu yako sawasawa. Napenda niseme Mheshimiwa Waziri, jibu lako halikuwa safi, sikuridhika nalo. Ninalo hapa na bahati nzuri Mheshimiwa Mohamed Seif, ambaye alikuwepo pale amelizungumza vizuri.

Kwanza, unasema aah, acha kwanza tujiangalie tufanye kongamano. Kuna ubaya gani kwenda Kenya? Kuna ubaya gani kwenda Ethiopia? Kwenda kujifunza wenzetu hawa wanafanya nini mpaka wanafanikiwa na sisi hatufanikiwi! Kwanza Kenya, hapa Nairobi unakwenda kwa gari tu, huna habari ya ndege, labda kwa Ethiopia, lakini ni karibu pale. Sikwambii uende China wala sikwambii uende wapi. Mimi bado nasema sikuridhika na jibu lako na bahati nzuri Mheshimiwa Mohamed Seif, amelizungumza hili. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, nendeni Kenya, nendeni Ethiopia mkajifunze wenzetu wanafanya nini mpaka wanafanikiwa katika mashindano ya riadha. Sisi tuna matatizo gani kiasi kwamba hatufanikiwi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alizungumzia akasema turudishe mashindano ya *Primary School* na *Secondary School*, nashukuru sana. Mmefanya hivyo na kweli mashindano yamerudishwa, tunawapata wale vijana. Sasa tukishawapata wale vijana wa *Primary* na *Secondary* waliofanya vizuri, *what next?* Unawapata tu, basi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima kuwe na kitu pale ambacho kinawenza kusaidia kuwaendeleza hawa vijana. Wenzetu katika nchi nyingine wana kitu wanaita *High Performance Training Centre*, ambayo hii *Training Centre* ndiyo inawachukua wale ambaao wameshinda kwenye *UMISETA*, sijui kwenye nini kule, wanawekwa pamoja pale wanapigwa msasa kama ni miezi miwilli, miezi mitatu, wanaendelezwa pale na baadaye wanarudi tena. Sisi hii hatuna. Hebu basi kama hatuna, naomba Mheshimiwa Waziri, tuwe na *High Performance Training Centre*, ili iweze kusaidia kuendeleza vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi kama hivyo ndivyo, naunga mkono hoja, lakini suala la *netball* lishughulikiwe haraka.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Lakini vilevile nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara hii kwa kutuandalia bajeti ambayo imetupa fursa kusimama hivi sasa kuweza kutoa michango yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafsi hii kwa makusudi mazima kumpongeza Waziri Mkuu – Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda kwa kazi nzuri anayoifanya ya kutuongoza hapa Bungeni. Mheshimiwa Pinda amekuwa msikivu, amekuwa akishaurika, tumekuwa tukimshauri mambo mbalimbali yanayojitokeza ndani ya Bunge na amekuwa akiyatrafutia majibu ya kuleta ufanisi wa kazi katika Bunge letu na kwa manufaa ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia hivi majuzi, tumekuwa tukilumbana humu ndani katika masuala ya mafuta. Lakini tulipolipeleka kwa Waziri Mkuu, amechukua hatua za makusudi na hivi leo watu wanaanza kupata huduma. Lakini siyo hilo tu, tunatarajia hoja ya Waziri wa Nishati na Madini, kwa kuwa tulirejesha, natumaini Mheshimiwa Waziri Mkuu atakuja na majibu mazuri itakapofikia siku ya siku. Kwa hiyo, ninamwomba Waziri Mkuu, tumhakikishie kwamba, sisi Wabunge tuko nyuma yake, tutaendelea kumshauri na tunaomba aendelee kutusikiliza. Akaze buti, asihofu jambo lolote ili kuifliska nchi yetu mahali panapokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani zangu za tatu, naomba niwapongeze wasichana wangu kutoka kwenye Jimbo langu la Masasi, wasichana kutoka Kijiji cha Ndanda, pale Njenga, ambao walishiriki ligi ya *Netball* ngazi ya Mkoa na kushika nafasi ya pili kwa kujitegemea wao wenyewe bila msaada wowote. Nawapongeza sana. Nasema nipo nyuma yao na hayo ndiyo matunda niliyokuwa ninawahamasisha wakati napita kushukuru. Nawashukuru sana kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuchangia kuhusu uhuru wa vyombo vya habari. Vyombo vya habari ni vyombo ambavyo vinatusaidia sana katika kutoa elimu na wananchi wanaelimika kuititia vyombo vya habari na wananchi wamekuwa wadau wakubwa katika vyombo hivi vya habari. Lakini niseme kwa masikitiko makubwa kwamba wapo wadau mbalimbali wanashindwa kuvitumia vyombo vyetu hivi vya habari kwa kutoa taarifa ambazo zinaweza zikasaidia katika nchi yetu na kupeleka taarifa kwenye vyombo vya habari zinazopotosha umma zisizokuwa na maslahi, zisizofundisha wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mfano. Kuna matangazo mbalimbali ambayo tumekuwa tukishuhudia katika *television*, masuala kwa mfano ya Haki Elimu, tumekuwa tukiangalia jinsi wanavyoonyesha shule zetu zilivyo mbovu huko vijijini. Tumekeuwa tukishuhudia matangazo mbalimbali yanayotangaza jinsi akina mama tunavyolundikana kwenye kitanda kimoja pengine watu sita na wakati wa kujifungua kupata matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi ninaomba niwe tofauti na matangazo haya. Niwe tofauti na wadau wanaopeleka matangazo haya kwa sababu, kwa fikira zangu mara nyingi nimekuwa nikifikiria kwamba, mwananchi au mwanadamu anaweza akajifunza jambo zuri kwa yale mazuri ambayo yanatendwa na mtu mwengine. Nilichokuwa ninakitarajia, kama kuna hawa wadau wanapeleka haya matangazo, wanatumia pesa nyingi sana katika kufanya utafiti huko kwenye vijiji vyetu, kwa sababu, matangazo haya ninaamini yanalipiwa. Wanatumia pesa nyingi sana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafikiri hawa wadau kama wangkuwa wanaona kwamba Watanzania walio wengi hawana shule bora, tunapata shida ya maji, badala ya kutumia pesa nyingi kwa utafiti huu, fedha hizo zote wanazozitumia wangkuwa wanapeleka pale mahali ambapo pana tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mfano. Sisi Waheshimiwa Wabunge, tutakuwa mashahidi, yupo ndugu yetu mmoja anaitwa Mustapha Sabodo. Yule baba ana huruma sana na ana uzalendo wa nchi yetu. Ametambua matatizo mengi yaliyopo katika nchi yetu, ameona jinsi watu wanavyopata shida ya maji, ameona jinsi madarasa yetu huko vijijini yaliyopo mabovu, lakini ye ye badala ya kutumia pesa zake kupeleka matangazo kwenye vyombo vya habari na kutoa matangazo haya, amekuwa akitumia pesa zake kwa ajili ya kusaidia kuondoa kero mbalimbali zilizopo katika nchi yetu. Nampongeza sana mdau huyu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ninawaomba sasa wale wadau wengine ambao wanatumia muda mwangi na pesa nyingi kupeleka mambo mabaya katika vyombo vya habari, waige mfano wa Mustapha Sabodo. Hizo pesa kama wanazo, basi wanisaidie hata mimi Mama Kasembe kupeleka kwenye Jimbo langu ziende zikajenge shule, niende nikachimbiwe visima, kwa sababu yale matangazo wasije wakafikiria kwamba, wananchi yanawafurahisha na hayaleti tija yoyote wala hayaleti manufaa yoyote. Naomba vyombo vya habari mnaonisikiliza, leo hii naomba mtoe kwamba, Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Masasi, anawaomba wadau wote ambao wanaleta

matangazo ya kudhalilisha nchi yetu, pesa hizo watupelekee Majimboni. Wabunge tuna matatizo makubwa Majimboni kwetu. Hongera sana ndugu yangu Mustapha Sabodo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleee kuzungumzia suala la michezo. Suala la michezo, mimi nafikiri katika nchi yetu bado hatujatilia mkazo. Lakini vile vile suala la michezo ukiangalia kwa undani, kwa sehemu kubwa tumekuwa tukiachiwa wanasiasa. Sisi Wabunge, Madiwani, kwenye maeneo yetu kama hatuhamasishi michezo, basi ujue huko Mikoani michezo imekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii nimkumbushe Mheshimiwa Waziri, tulipoanza Bunge hili, nilifanya makusudi mazima ya kumpatia mpango uliopo kwenye Jimbo langu la Masasi kwa ajili ya kuwasaidia vijana ambaao wao wenyewe wameamua kuondokana na kukaa katika vijiwe na kuunda vikundi nya kiuchumi, lakini jioni wanashiriki michezo. Nilikuletea na ninafikiri umeisoma, umeipitia, sidhani kama kuna Mbunge amefanya hivyo. Ninachokitaraja Mheshimiwa Waziri, hawa vijana walikuwa wanakaa vijiweni, wao wenyewe ndio wameamua kusajili vilabu ambavyo ndani yake kuna vikundi nya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa ninavyozungumza, Jimbo la Masasi, kuna vikundi vilivyosajiliwa 85, vikundi nya utamaduni vinne vimesajiliwa, lakini hawa wote ndani ya klubu zao wameanzisha vikundi nya kiuchumi. Asubuhi wanafanya kazi za kiuchumi kuzalisha mali, jioni wanakwenda kushiriki michezo. Naomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuwa anafanya majumuisho, anipe jibu la ile ombi langu. Naomba nisaidiwe, tusiwavunje moyo hawa vijana ambaao kwa kweli sasa hivi wameamua kuachana na mambo yote waliyokuwa wanayafanya maovu na kurudi katika mstari kama Serikali inavyoshauri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho, naomba nichukue nafasi hii kuzungumzia suala la utamaduni. Suala la utamaduni katika nchi yetu tumekuwa na tofauti makabila kwa makabila. Kila kabile lina utamaduni wake, lakini hivi sasa utamaduni mkubwa uliopo ndani ya makabila yetu umekuwa ukipotea. Naomba nichukue nafasi hii kupongeza kabile moja bila hiyana ya aina yoyote, naomba niwapongeze wamasai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu Wamasai ukiangalia katika nchi yetu ndiyo bado wanaendeleta tamaduni zao. Lakini pamoja na kuwapongeza na wao naomba niwaambie, kwa sababu, ninavyoona, hata wao utamaduni wao utapotea kwa sababu, sasa hivi wameenea nchi nzima, wamekuwa wamachinga wa kuuza dawa. Sasa nina wasiwasi, wale Wwamasai wangu waliopo Mtwara, kama bado wanaendeleta mila na utamaduni waliokuwa wanauendeleta walipokuwa huko Arusha, nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mfano wa kuigwa na ninasema sisi wengine tullobakia tuangalie mila tulizonazo katika makabila yetu. Zile mila na desturi ambazo kwa kweli zinaweza zikatujengea heshima katika nchi yetu, hebu tuziangalie tuzirejeshe tena kwa manufaa ya kizazi kijacho. Iko hatari kabisa, kizazi kijacho hakitajua utamaduni wetu ulikuwa ni upi? Kwa sababu sasa hivi watoto wetu wamekuwa wakiangalia luninga. Kwa hiyo, watoto wanafikiria kwamba, tamaduni ni yale mambo wanayoyaona katika TV zetu. Kwa hiyo, ninaomba sana tushirikiane, Serikali pamoja na sisi viongozi na wazee kule vijijini wanaonisikiliza, kurudisha heshima ya nchi yetu hii kuititia suala la utamaduni wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye suala hilo hilo la michezo, mwaka huu hatukufanya vizuri katika kuwandaa vijana wetu wa Shule za Msingi pamoja na Sekondari. Kazi ilikuwa kama ni ya Zimamoto. Dakika za mwisho, Serikali ndiyo inaagiza kwenye Halmashauri zetu kwamba, Halmashauri zisaidie Shule za Msingi katika kuendesha haya mashindano. Kama tutakuwa tunakwenda kwa utaratibu huu, hatutapata vijana ambaao wana vipaji na huko vijijini wamejaa vijana ambaao wana vipaji nya aina mbalimbali. Kama tukiwasaidia, ninaamini kabisa tutakuwa na vijana wa fani mbalimbali wa michezo ya aina mbalimbali kwenye Taifa letu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile tuangalie suala la viwanja. Hata tukiangalia kwenye sekondari zetu za Kata tunazojenga, viwanja tunavyovikuta, sana sana ni viwanja nya mpira wa miguu. Sekondari chache utakazozikuta ambazo zina viwanja nya mpira wa miguu, *netball*, labda *basket ball*, hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo tunahimiza kwamba, vijana wetu mashulen i washiriki mashindano ya aina mbalimbali. Bila kuwa na viwanja, hili suala halitafanikiwa. Lakini tunapozungumzia michezo, tuszungumzie suala la *netball* pamoja na mpira wa miguu tu. Iko michezo mingi, zamani nilikuwa naona, kwa mfano, masuala ya riadha, kupochezana vijiti, watu walikuwa wanakimbia kwa magunia. Ile pia ilikuwa inaleta changamoto kwa sababu, ipo michezo ambayo mnaweza mkashiriki watu wa rika zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kwa mfano tukikazania mashindano, kwa mfano, yale ya kukimbiza mbuzi, atakayempata wa kwake, unawasadida hata wazee wetu na wao washiriki katika suala la michezo. Kuna mchangaji mmoja hapa amesema michezo ni afya. Unapofanya michezo na wewe unapunguza gharama za kwenda hospitali kupata matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba nitoe hamasa kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba na sisi tusiwe wasemaji tu, tushiriki katika michezo, tunapokuwa hapa Bungeni na tunaporudi majumbani kwetu. Kwa sababu, sisi tukishiriki suala la michezo, nafikiri hata jamii inayotuzunguka na wao wataiga mfano wetu, tutajikuta jamii yote inashiriki katika michezo. Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, hapa Bungeni tuna timu zetu, tuna klabu yetu...

*(Hapa kengele iligonga kuashiria muda wa  
mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru, Mheshimiwa.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, nakushukuru. Sasa badala ya Mheshimiwa Moza Abeid Said, namwita Mheshimiwa Kombo Hamisi Kombo.

**MHE. KOMBO HAMISI KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafsi hii ya kuchangia Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Nianze na Sekta ya Habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Habari ni chombo muhimu katika jamii yoyote na katika nchi yoyote. Sekta ya Habari ni sekta ambayo inaweza ikaliletea Taifa maendeleo. Lakini sekta hii ya habari ina uwezo mkubwa wa kuweza kulilitea janga Taifa lolote. Hali iendako, vyombo vya habari vitatumiwa vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba, kweli Tanzania tunao utaalam wa vyombo vya habari, lakini wengi wao wanavitumia vyombo vya habari kinyume na maadili ya vyombo vya habari vinavyotakiwa vitumike. Tuangalie miaka ya nyuma wenzetu wa Burundi kulikuwa na redio moja iliyokuwa ikiitwa Redio Intarahamwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa redio hii ilitumika vibaya katika nchi ya Burundi, iliweza kuwalettea Warundi maafa makubwa mno, sasa na Tanzania upeo wetu wa kutumia vyombo vya habari tunautumia vibaya. Inawezekana kwamba baadhi ya waandishi wa habari wanachukua hongo kutoka kwa watu fulani, ili waweze kuandika habari zao vile ambavyo wanataka wao. Sasa haya, siyo maadili mema ya uandishi wa habari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari ni elimu, na endapo itatumika vizuri kama inavyotakiwa, basi wananchi wetu wataweza kuzifuatilia habari zetu. Lakini nataka nikuhakikishie kwamba, kuna baadhi ya magazeti hivi sasa, baadhi ya wananchi wengi hawayatumii kwa sababu maneno yaliyomo mle, hayaleti changamoto yoyote ya maendeleo isipokuwa ni kupigana vijembe, kulumbana baina ya viongozi na kiongozi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niseme kwamba waandishi wetu tuiswatumie vibaya. Kama tuna chochote cha kuwasaidia waandishi, kama alivyosema Mheshimiwa Bulaya, basi tuwasaidie waandishi, lakini isiwe ni kichocheo cha rushwa cha kutaka tuandikiwe habari zetu vile tunavyotaka sisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni utamaduni. Tukitaka tusitake, utamaduni wa Mtanzania umeanza kuathirika kwa kiasi kikubwa mno kwa kufuata tamaduni za wageni. Siyo tamaduni ya Watanzania kuva rasta hata siku moja, wala siyo utamaduni wa Mtanzania kuva nguo nusu uchi. Siyo utamaduni wetu! Siyo heshima zetu! Siyo silika zetu! (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo tumeefikia hatua ya kwamba Watanzania hatuthamini hata miili yetu au ngozi yetu ambayo tumejaliwa kupewa na Mwenyezi Mungu, kuna Watanzania ambao wanadiriki kula vidonge, eti wabadijishe ngozi za miili yao. Sasa hii, ni kuchuma maradhi ya makusudi kwa sababu rangi hiyo unayoipata ambayo siyo majaliwa yako, rangi yako ulijojalilwa na Mwenyezi Mungu, ndiyo hiyo hiyo, basi rangi hiyo unayoipata haikusaidii chochote. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la sanaa, nakubali kwamba wasanii Tanzania hawajapewa umuhimu unaostahiki, na ni jukumu la Serikali kupitia Wizara husika kuhakikisha kwamba imewaandaa wasanii wa Kitanzania ili waweze kuliletea Taifa hili maendeleo ya kweli. Lakini sanaa nazo zina mipaka yake, sanaa nyngine zinakiuka maadili na silika za Watanzania. Kuna baadhi ya michezo ambayo inachezwa na baadhi ya wasanii wanaonyesha mambo ya siri za ndani za baba na mama mbele ya watoto jambo ambalo siyo somo la kuweza kumpa mtoto wa Tanzania, linakiuka maadili na silika za Watanzania. Ni aibu, kashifa, baadhi ya CD au kanda zinazoonyeshwa kwa hadhara ya vijana wetu wadogo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie kusema kwamba siyo utamaduni wa Mtanzania mwanamke kuweza kuva nguo za kiume na hakuna dini yoyote inayoruhusu kufanya hivyo kuweza kuva nguo za kiume na hakuna dini yoyote inayoruhusu kufanya hivyo. Hakuna dini inayomtaka mwanamke atembee nusu uchi. Haya yanatendeka. Leo tunakaa tunawasema vijana kwamba vijana wetu wanakuwa ni wakorofi, wakati sisi wazazi ndiyo source wa matatizo yale. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika suala la michezo. Nakubaliana na wenzangu waliosema kwamba michezo ni sehemu ya ajira. Hivyo, kwanini kama kweli Tanzania tunataka tuonekane katika medani ya kimataifa kwamba na sisi tunaweza, tusiweze kuwatoa vijana wetu kuwapeleka popote nchini, lakini wakaenda wakasoma sekta hii ya michezo wakaja hapa wakalitumikia Taifa lao na kulipatia faida Taifa lao? (*Makof!*)

Tunachukua mtu kutoka nje kwa ajili ya kuja kusomesha hapa, lakini unapochukua kundi la vijana ukawapeleka nje kwa ajili ya kwenda kusoma, aidha, iwe mpira wa miguu au mpira mwingine wowote, basi wanapoingia hapa, wao watakuwa ni walimu bora wa kuwasomesha, wengine na Taifa hili halitakuwa tena na uchache wa wanamichezo utakaoweza kuwafundisha wengine. (*Makof!*)

Sasa niseme kama Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo imetengewa Shilingi bilioni 18.5 na hiki ndicho walichoomba na wao wamesema kwamba kumeongezeka point moja. Hatufiki popote katika Sekta ya Michezo. Bado tutaendelea kurudi chini, bado tutakuwa hatuendelei kimichezo na bado tutatafuta walimu wa kuja hapa kuchukua riziki zao ambazo hazitawasaidia Watanzania halafu warudi kwao, ni matajiri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pendekezo kwamba kuna haja ya kujenga kiwanja kila Mkoa ambacho kitashirikisha michezo yote, lakini vilevile kuwe na viwanja angalau vinne, iwe ni Kanda ya Ziwa kiwanja kimoja, Kusini kiwanja kimoja, Kati kiwanja kimoja na Kaskazini kiwanja kimoja. Hivi viwe ni viwanja ambavyo vitatambuliwa kuwa ni viwanja vya kimataifa vilivyopo Tanzania, na Zanzibar kuwe na kiwanja kimoja. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani siyo Watanzania wengi ambao hawapendi michezo. Mimi mwenyewe ni mwana sanaa, na tayari nimeshatunga kitabu changu, rasimu ipo hapa, nimeieleza wakati nilipotakiwa nikijaza fomu, nilifikiria angalau nitaitwa nihojiwe juu ya rasimu hii na vipi inaweza ikatoa mchango kwa Taifa? Lakini sijaulizwa mpaka leo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, ahsante sana. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, nakushuru Mheshimiwa kwa vile muda umeshatuishia, naomba niwataje ambao watachangia tukirudi saa kumi tutaanza na Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Vicky Kamata, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Murtaza Mangungu, wakajiandae, tukirejea hapa wataanza kuchangia.

Nina tangazo moja. Mheshimiwa Pindi Chana - Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala anawatangazia wanasheria Wabunge wote, kesho tarehe 12 kutakuwa na Mkutano wa Tanganyika *Law Society*, ambao utafanyika Chuo Kikuu cha *Dodoma, College of Humanities* kuanzia saa tatu asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya tangazo hili, naomba kusitisha shughuli za Bunge hadi saa 10.00 Alasiri.

(*Saa 7.14 mchana Bunge lilitfungwa mpaka Saa 10.00 jioni*)

(*Saa 10.00 jioni Bunge lilitrudia*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Kama niliviotangaza mchana, tunaanza na Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo na Mheshimiwa Vick Paschal Kamata na Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa ajiandae.

Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo inaonekana hajaingia, basi naomba nimwite Mheshimiwa Vick P. Kamata.

**MHE. VICK P. KAMATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu. Lakini kabla ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya njema iliyoniwezesha niwe mahali hapa sasa hivi na kuchangia bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda sana kuvipongeza vyombo vyahabari na kuwapongeza waandishi wa habari kwa kazi nzuri na kubwa ambayo wanaifanya na kazi ambayo inatambulika na kuheshimika. Kwa kweli nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijawapongeza zaidi na zaidi, ningependa pia ku-*declare interest* kwamba na mimi ni mwandishi wa habari, nimesoma Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustine, ninajua ugumu, changamoto, mazuri na kila kila kitu ndani ya vyombo vyahabari japo sitazungumza kwa kirefu sana kutokana na muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu Wamarekani wanasema katika ile mihimili mitatu kama kungekuwa na wa nne, basi ingekuwa ni vyombo vyahabari, nami naungana nao na ninakubaliana nao kwa kuamini na kutambua mchango mkubwa wa Vyombo vyahabari. Vyombo vyahabari vikiamaa kujenga, vinajenga kweli na vikikorofishwa vikaamua kuharibu, vinaweza kuharibu kweli. Hivyo, tunatakiwa tuvithamini na kuviheshimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema *Journalist is a watchdog of the society*. Kazi ya mbwa ni nini? Kazi ya mbwa ni kubweka pale anapoona kuna mambo hayaendi sawa na kazi ya mbwa ni kubweka pale anapoona kuna kitu kinatia mashaka. Hivyo, waandishi wa habari wakibweka au wakiandika kitu, tunatakiwa tushirikiane nao. Ina maana wanakuwa wameona kuna tatizo mahali fulani, au kuna kitu kina utata mahali fulani. Hivyo, sisi kama Serikali tunatakiwa kuungana na kushirikiana nao ili tuweze kulisukuma gurudumu tunakotaka liflike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina tatizo kidogo na sielewi kwa nini Serikali inachelewa sana kufanya maamuzi kwenye baadhi ya vitu muhimu. Kwenye vyombo vyahabari kuna Wakurugenzi ambao wame-*act* muda mrefu, kwa mfano, Habari, Maelezo na *Daily News* wana-*act* zaidi ya miaka mitatu sasa. Kwa hali ya kawaida, binadamu ye yote ukiwekwa mahali unakaa kama vile kwa muda, hujiamini kwamba wewe uko pale, huwezi kutoa ubunifu wako sawasawa kwamba mimi niko hapa, ngoja ni-*deliver* au ngoja nifanye kazi watu waone au ngoja nifanye kazi ambayo ninaiamini na kujua vizuri. Hata kama anataka kuanzisha kitu fulani atasita kwamba ah! pengine nikikianzisha kabla hakijafika popote, ataletwa mtu mwengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ni zaidi ya miaka mitatu kama sikosei hawa watu wana-*act* kama Watendaji wazuri. Kwa huu muda mrefu, wameshajulikana kama hawa watu wanaweza, basi wawekwe wawe *full directors*, wafanye kazi kwa kujiamini kwamba wako kazini kweli na kama basi hamwaoni kama wanafanya kazi vizuri, basi wateuliwe wale ambao mnadhani watafanya kazi. Wakati mwininge tunatakiwa sisi kama Serikali tushirikiane na hivi vyombo nya habari ili tufanye kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingependa kuongea sana kwenye eneo hili, lakini pia kabla sijatoka kwenye eneo hili la vyombo nya habari, kuna Sheria ambayo ilikuwa inazungumzwa Bunge lillolipa, sikuwepo, lakini nilikuwa nafuatilia. Kuna Sheria ya vyombo nya habari, ninaamini kabisa Sheria hii ndiyo itakayoweza kuleta tija kwa waandishi wa habari na kwa vyombo nya habari kwa ujumla. Ninaomba basi Serikali ilete hii Sheria hapa ili tuweze kujadili. Ninaamini kabisa Sheria hii ndiyo itakayoleta tija kama nilivyosema pale mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii inasisitiza na ni lazima iangalie maslahi ya waandishi wa habari. Naomba Sheria hii iangalie maslahi pia ya vyombo nya habari ili tuweze kufanya kazi kwa pamoa kama mhimili wa nne japo haujawa rasmi. Nimesema Wamarekani wamesema kama kungekuwa na mhimili mwininge, vyombo nya habari vingekuwa ni muhimili wa nne. Basi na mimi naamini na wote mnaamini vyombo nya habari vingekuwa vikifanya kazi kubwa, tushirikiane navyo ili tuweze kufika kule tunakotaka kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia randama ya Wizara, nimeangalia katika mipango ya maendeleo, nimeona kuna mpango wa kuibua fursa ya ajira kwa vijana. Mpango huo umelenga kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana, mpango huo umeandaliwa na Serikali ikishirikiana na Shirika la Kazi Duniani, kitu ambacho ni kizuri, nafurahi sana. Lakini ninapenda tu kujua ni vijana wangapi kutoka Mkoa wa Geita watanufaika na mpango huu?

Mwisho wa siku, nitapenda kuuliza kama tutajaaliwa mwakani njue ni vijana wangapi wamenufaika na mradi huu mzuri, maana kama unatoa mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana, basi vijana walio wengi maeneo mbalimbali wakipata hii elimu itawasaidia kujkwamua na ugumu wa maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika hii bajeti, nimeona kuna mradi wa kinga dhidi ya UKIMWI. Mradi huu lengo lake kubwa ni kuhamasisha vijana kubadili tabia ili kupunguza maambukizi ya UKIMWI, mimba zisizotarajiwa, na watoto wa mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Wizara hii kama ambavyo vyombo mbalimbali vimejitokeza kuwaibua wanaovuta madawa ya kulevyo, wametambulika na wakasaidiwa na wengine wamepatiwa elimu, sasa wamerudi kuwa katika hali nzuri ya kawaida. Kuna kundi dogo la vijana nadhani limesahaulika kidogo, ni kundi la hawa mabinti ambao wanajuza usiku, yaani machangudoa. Nina imani kabisa kuititia Wizara hii kama litawekwa dirisha na ukawekwa utaratibu wa kuwapata hawa mabinti nina uhakika siyo wote ambao wanapenda kufanya hii biashara haramu na mbaya, ninaamini wanafanya biashara hii pengine kutokana na mazingira, ugumu wa maisha na wengine pengine ni kukosa elimu.

Hivyo dirisha hilo kama litakuwepo litawasaidia hata hawa mabinti ambao hawapendi kufanya hii biashara, pengine wanafanya kwa sababu ya kukosa elimu na kukosa misaada muhimu, hii inaweza ikawasaidia wakabadilika na kubadilisha tabia. Kwa sababu fungu lipo kwa ajili ya kuwasaidia na kuwashamasisha waweze kubadili tabia. Ninaomba sana Serikali izingatie hilo na iwasaide, maana hilo ni kundi la vijana ambalo limetengewa hili fungu, itakuwa ni vizuri pia na wao wakanufaika nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye Idara ya Utamaduni ambayo ndiyo inabeba hasa jina la Wizara, moja ya jukumu la Idara ya hii ni kuimarisha na kuwezesha sekta ya utamaduni iweze kushiriki kikamilifu katika kuinua pato la mwananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Geita na maeneo mengine, sisi Wabunge wote ni mashahidi, tunapokwenda katika majimbo na Mikoa yetu tunaona makundi mbalimbali ya ngoma za asili. Hawa watu wanafanya kazi nzuri, wanadumisha utamaduni wetu, wanaimba nyimbo nzuri, wanaelimisha jamii na wakati huo huo wanatuburudisha. Lakini sioni kama mchango wao unatambulika sana na Serikali. Kuna hawa Maafisa Utamaduni, hivi kweli wanajua nini wajibu wao? Hivi kweli Serikali inawajengea uwezo ili waweze kujua majukumu yao kule waliko?

Mimi nina imani kabisa kama Maafisa Utamaduni watapatiwa elimu ya kutosha, wakaelekezwa majukumu yao, wakashirikiana na wanakijji wakaweka *program* ya kushindanisha vikundi na kikundi na kinachofanya vizuri kinapatiwa motisha fulani. Kama wakishindana kutoka Tarafa na Tarafa au Kata na Kata mpaka kufikia Wilaya na wanaofanya vizuri labda wanapewa Trekta. Hii itawaongeza motisha na kuipenda sanaa na kufanya kazi kwa kujituma ili iweze kuwaongeza pato, maana hata hii ni ajira na kama Serikali itaitambua itakuwa ni ajira nzuri kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali ikishirikiana na Maafisa Utamaduni ambao wanalipwa mishahara kwa ajili ya kazi hizo, basi watoe elimu, wahamasishe hivi vikundi ili vijitume, vitunge nyimbo nzuri, viburudishe na wakati huo huo waone wanaburudisha, lakini wanapata faida ya burudani wanayoitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, nina tatizo kidogo ambalo limenisumbua akilini mwangu. Nimekuwa nikizungumza na wasanii wa *Bongo Movie* na wakati huo huo nimezungumza na wasanii wa *TAF* ambao ndiyo shirkisho la wasanii nchini. Kuna mgogoro mkubwa, ninaamini kabisa Waziri au Serikali inaweza ikawa na taarifa na mgogoro huu. Hivyo, ninaomba basi, Serikali ijaribu kuwaita hawa watu wakae pamoja wazungumze na kujua tatizo lao ni nini. Maana mimi baada ya kuwasikiliza nimeona kila upande una mazito.

Naomba sana Serikali mara baada ya mimi kuzungumza hapa, Waziri azungumze na hawa watu ili kila mtu aeleze ni nini tatizo na wajue ni jinsi gani watalitatua, kwani lengo ni kufanya kazi kwa kushirikiana tuijenge nchi yetu, kwani wasanii ni kioo cha jamii.

Sasa hivi ukiangalia kutokana na huu mgogoro, kila siku tunaangalia kwenye magazeti, utaona msanii kaandikwa vibaya, kumbe kundi hili limechochea maneno, limepeleka *story* kwenye gazeti, wakati mwininge *story* haina ukweli, tayari huyo mtu ameshachafuliwa. Hii inasababisha watu waone fani ya sanaa hapa nchini haina maana. Kwa hiyo, tunaomba Serikali isaidie kuwaweka sawa hawa watu ili mgogoro uishe ili tuungane tufanye kazi kwa pamoja, tushirikiane na tuweze kufika mahali ambako tunataka kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona muda unanitupa mkono, lakini naomba nimzungumzie mtu mmoja anaitwa Msama ambaye amejitahidi sana. Kwanza naomba nimpongeze. Amejitahidi sana kuhakikisha anatetea wasanii waliokuwa wanaibiwa kazi zao. Mtu huyu amefanya kazi kubwa na inayotisha. Ameshakamata kazi ambazo zinazidi shilingi milioni 150 mpaka sasa, hata maisha yake pia yako hatarini kwa sababu mtu anaye-produce hizo *CD* umemkamata na kumpeleka Mahakmani. Anaona kabisa sasa umeshamzibia mwanya wake wa kuiba, kufaidi na kuishi kama alivyokuwa anataka kuishi. Huyu mtu yuko hatarini, hivyo tunaomba Serikali ishirikiane naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona pia Polisi hawana uelewa mkubwa wa jinsi ya kuwakamata hawa watu wanaoiba kazi zetu sisi wasanii. Hivyo, iwape elimu kubwa ya kutosha ili vita hii tuweze kushinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache, naunga mkono hoja. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, nakushukuru. Sasa namwita Mheshimiwa Victor Mwambalaswa.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja hii iliyo mbele yetu. Pamoja na kukushukuru wewe, lakini

namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa zawadi ya uhai na nguvu mpaka nimesimama kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyezekiti, hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Vijana ni nzuri sana, lakini nitaanza kuongelea vijana. Vijana ni Taifa la leo, vijana ni Taifa la kesho na vijana ni Taifa la kesho kutwa. Taifa la Tanzania linaitwa Kisiwa cha Upendo, Uvumilifu, Umoja na Mshikamano kwa sababu sisi vijana wa zamani tulifundwa na kulelewa na waasisi wetu na wazazi wetu. Pia tulifundwa na kuwekwa unyago tukawa na moyo wa upendo, wa kushirikiana na kuheshimu watu dunia nzima. Ndiyo maana nchi yetu inaheshimika duniani kote. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyezekiti, lakini vijana wetu sasa hivi kuna hatari ya kumomonyoka kwa upendo na uvumilifu na uchapa kazi, inabidi vijana hawa tuwapeleke jandoni, inabidi tuwafunde.

Mheshimiwa Mwenyezekiti, kuna jando ya aina mbili. Jando ya mila ambayo unawekwa kambini, unafunzwa mambo ya maisha, unafunzwa kuheshimu na kuwatii wakubwa, kupenda kazi, ndoa na kila kitu. Lakini lipo jando la pili ambalo ni la hospitali. Hilo wanashughulika tu huko hospitali, basi. Sasa ukimwona kijana leo anamwambia mtu mzima ambaye umri wake ni sawasawa na baba yake kwamba wewe muongo, ujue hii ni matokeo ya jando la hospitali. Mjomba wangu ananiona pale anacheaka. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyezekiti, naomba Wizara ifanye ubia na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga, Jeshi la JKT kwa vijana, lirudi na usimamie wewe. Mimi nimekwenda JKT, ukifika JKT kitu cha kwanza unapewa kitanda, godoro, *mess tin*, nguo zote unabeba kichwani. Kitanda unabeba kichwani ndiyo unakwenda kutafutiwa chumba. Utakaa huko miezi sita au mwaka, utadhani unapata mateso sana ya kufanya kazi na kupiga kwata lakini mwisho wa siku ukitoka JKT utakuwa na moyo wa uzalendo, upendo, uvumilifu, kupenda kazi na utaifa, unakuwa umevipata kutoka JKT. Jambo la muhimu sana ni utaifa na kupenda kazi na kutokupenda dezo unafundishwa JKT.

Mheshimiwa Mwenyezekiti, kwa hiyo, naomba sana Wizara hii ifanye ubia na Wizara ya Jeshi la Kujenga kusimamia vijana, waanze mara moja kupelekwa jandoni JKT ili tuwe na Watanzania wazuri wa kesho kutwa.

Mheshimiwa Mwenyezekiti, miaka ya 1960 na 1970 ukichukua mchezo wa mpira wa miguu tu, Tanzania ilikuwa katika Afrika Mashariki na Kati kila anayekuja hapa anachukua mbaao. Aje Zambia anachukua mbaao, akija Malawi mnahesabia mbaao, Kenya, Ethiopia, Rwanda na Burundi ndiyo usiseme, lakini sasa kila tukienda huko tunachukua mbaao sisi, yaani Tanzania inachukua mbaao. Nadhani kuna kitu kimepotea hapo katikati.

Mheshimiwa Mwenyezekiti, nakuomba sana, Wizara hii ianze kusimamia michezo yote kuanzia kwenye shule za msingi. Kwenye shule za msingi kuwe na viwanja vya kutosha, vifaa vya michezo vya kutosha, yaani Halmashauri itoe, kuwe na Walimu wa michezo wa kutosha. Shule za Sekondari kuwe na viwanja vya kutosha. Sasa hivi kuna watu wengi wanajenga Shule za Sekondari binafsi, wanajenga majengo tu na maghorofa, lakini hawaweki viwanja vya michezo, kwa hiyo, watoto wanakwenda kusoma tu na kwenda mjini. Viwanja vya michezo viwepo na Wizara yako ishirikiane na Wizara ya Elimu, kila panapoengwa Shule, Wizara ihakikishe kwamba pale pana viwanja vya michezo, vifaa vya michezo na pana walimu wa michezo.

Mheshimiwa Mwenyezekiti, mimi nimekwenda kwenye Chuo Kikuu ambacho Serikali yetu ya awamu ya nne imefanya jambo kubwa na zuri sana. Ni Chuo Kikuu cha Dodoma, yaani *UDOM*. Ndiyo! Pana viwanja viwili au vitatu vya michezo. Wanafunzi 20,000, viwanja viwili havitoshi, ndiyo maana vijana wetu wa sasa hivi *spear time* yao ni tofauti na sisi. Sisi zamani ilikuwa *spear time* wakati tunasoma unaitumia kwa michezo au kujisomea. Lakini wao sasa hivi *spear time* yao wanaitumia kwenda kuzurura mjini. Nakuomba sana Wizara yako ishirikiane na Wizara ya Elimu ya Juu ili kuhakikisha Vyuo Vikuu vyetu vyote vina viwanja vya michezo, vina Walimu wa michezo kama Mwalimu Zambia wa zamani, wa kutosha ili Taifa letu liache kuwa kichwa cha mwendawazimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba Wizara ishirikiane na Wizara ya Ardhi. Nchi nyingi ukiona kwenye miji wanaweka *open spaces*, siyo za kupumzikia tu, bali hata michezo, vijana wanacheza michezo pale. Sasa Dar es Salaam imevamiwa, nashukuru Wizara ya Ardhi imeanza kulishughulikia suala hili na hata Dodoma imeanza kuvamiwa sasa hivi. *Open spaces* zote wanajenga watu. Kwa hiyo, vijana wetu wanakuwa hawana pa kucheza, ndio maana muda wa *spare* wanakwenda kuzurura mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, Wizara yake ishirikiane na Wizara ya Ardhi ili kuhakikisha kwamba *open spaces* zinatumwa kwa mambo ya kupumzika na pia vijana kucheza michezo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yanayofuata natataka ufanuzi na maelezo kidogo kwa Mheshimiwa Waziri. Jambo la kwanza niongelee uwanja wa Taifa wa Mpila. Serikali ya Awamu ya Tatu imefanya jambo zuri sana, tumejengewa uwanja wa michezo mkubwa sana na wa kisasa na uwanja huo ni mzuri sana katika Afrika mashariki, kwani unachukua watu wengi. Nia ya Serikali ni kuinua viwango vya michezo vya vijana wetu.

Sasa uwanja wa Taifa, viti vyote vilivyopo kule ndani vimewekewa namba. Maana ya namba zile ni kwamba, utakapokuwa unanunua tiketi, namba ya kiti chako inakuwa kwenye tiketi. Ili nunue tiketi ambayo ina namba yako, zipo mashine ambazo zinatumika kuingiza watu kwenye viwanja vya michezo, *cinema halls*, kwenye *stations* za treni ambayo inakuwa na namba yako. Hiyo inasaidia kuhesabu watu na kuhesabu kiasi cha fedha. Hizi mashine zinaitwa *turnstile machines*. Zipo za *electronic* na zipo nyingine ambazo ni *manual* ambazo zinafanya kazi hata kama umeme umezimika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka maelezo ya Mheshimiwa Waziri, kwanini wanaohusika hawaweki mashine hizi Uwanja wa Taifa? Wanataka tuvaelewe vipi? Serikali kwa nia nzuri inataka kuinua michezo na ndio maana Mheshimiwa Rais ameamua kumlipa mshahara kocha wa timu ya Taifa ya mpila wa Miguu. Sasa badala ya kufanya juhudhi mpate mapato ya kutosha uwanjani pale, mumlipe wenyewe huyo kocha. Mmeufanya kuwa ni mradi wenu wa kutunisha matumbo yenu. Nataka maelezo kwa kina ni kwanini hawaweki mashine hizo pale uwanjani? Hilo la kwanza! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nitataka maelezo. Shirila letu la Utangazaji, *TBC* miaka ya karibuni hapa wallingia ubia na Serikali ya Japani, wakapewa fedha nyingi, wakajengewa mtambo wa kisasa wa masafa mafupi kule Mabibo ili waweze kurusha vipindi vya shule kwa Shule za Msingi ili kuweza kuziba pengo liliopo la walimu ili wanafunzi wanaingia darasani, wanaikuta redio iko pale, wanamsikiliza mtu ambaye yuko *studio* Dar es Salaam, anawafundisha. Lakini cha ajabu ni kwamba *TBC* mradi huo wameuzima, wanachangamkia mambo mengine. Huu mradi uko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Kila wakati tunapiga kelele kwamba, walimu hawatoshi katika Shule za Msingi. Serikali ya Japani imetusaidia tuwafundishe watoto wetu kwa kutumia vipindi vya redio, *TBC* wamepeleka wapi mradi huo? Nitataka maelezo ya kutosha kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kumezuka mtindo sasa hivi wa vituo vya *television cables* vya Mikoani, huko Dodoma, Iringa, Mwanza, wanarussha matangazo ya *TV* wao wenyewe bila ya kuitisha kwa *authority*, bila kuitisha kwa *Tanzania Communication Regulatory Authority (TCRA)*. Ipo imezuka sana, hiyo ya *cable TVs*. Nataka maelezo ni kwanini Wizara imeacha hizi *television cables* zinarusha matangazo kienyeji huko Mikoani? Hao ndio wanaopotosha hata maadili, wanarussha vipindi vingine vya ajabu ajabu hata vya ngono. Wizara inachukua hatua gani kuweza kushughulikia suala hili? Nitataka maelezo ya kutosha kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nataka nizungumze juu ya mengine ambayo ni mazuri zaidi kwa *TBC*. *TBC* wanaporusha matangazo yetu haya kama ninavyoongea sasa hivi inabidi walipwe na Bunge, hivi ninavyoongea, wanalipwa na Bunge. Mwaka jana *TBC* wamedai fedha zao muda mrefu sana, mpaka Mheshimiwa Waziri Mkuu alipoingilia kati ndipo wakalipwa na

Bunge. Mheshimiwa Waziri Mkuu alipoingilia kati, ndiyo wakalipwa na Bunge shilingi milioni 700. Kwanini Hazina isiwalipe *TBC* moja kwa moja? Kwanini wanatoa cheki huku, halafu tena cheki itoke huku iende kule? Nitataka maelezo ya kina kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba *TBC* pia wana kituo chao Mikocheni ambapo wanajenga studio ya kisasa, na Serikali iliwaahidi kwamba itawapa fedha za kutosha ili waweze kujenga kituo hicho kwa gharama ya shilingi bilioni 1.2. Toka mwaka 2009, huu ni mwaka 2011 Serikali imetoa shilingi milioni 600 tu na Mkandarasi ambaye wamemweka kule anatishia kuwapeleka *TBC* Mahakamani. Naomba Serikali ifanye kila njia iipe *TBC* hizo shilingi milioni 600 zilizobaki ili aweze kumlipa huyu mkandarasi na kujengewa kituo chake cha kisasa huko Mikocheni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama niliyosema, Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, mimi ni mjomba wake na unajua mjomba ni mama. Kwa hiyo, sivezi kusema kwamba sitaunga mkono hoja ya mjomba ambaye mimi ni mama yake, lakini nitaunga mkono hoja hii baada ya kunieleza na kunifafanulia mambo haya matatu, manne ambayo nimemwuliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, nakushukuru sana. Namwita Mheshimiwa Moza Abedi Saidi, kama hayupo, naomba nimwite Mheshimiwa AnnaMaryStella John Mallac. Mheshimiwa Magreth Mkanga ajandae, pia Mheshimiwa Murtaza Mangungu atamfuatia.

**MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Aidha, kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipatia afya na uzima wa kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wizara hii ya leo, naona nitaongelea zaidi upande wa vijana. Tunapoongelea vijana, tunaongelea nguvu kazi ya Taifa ambayo ikitetereka tu Taifa lote linatetereka pia. Kijamii, tunapoongelea sura ya umasikini, huonekana pia kupitia katika vijana hasa wanapokosa ajira, elimu, afya na kipato kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo tulilonalo sasa katika nchi yetu ni sera na mipango isiyotekelezaka, kwani vijana hawa hawa tunaowazungumzia ndiyo hao hao amba Serikali kwa namna moja ama nyininge imewasahau sana. Serikali haitoi fursa sawa kwa vijana wote, imekuwa zaidi inatenga Mikoa hasa nikiangalia wenzetu wa Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na miji mingine iliyoendelea. Lakini kwa sisi wa Mikoa ya Rukwa na Katavi, tumesahaulika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wetu wa Mikoa ya Rukwa na Katavi kwa kweli wananyanyasika na kuhangaika sana. Serikali ilisema kwamba, vijana waji-group waunde vikundi na kuanzisha miradi, baada ya hapo Serikali itawa-support. Lakini nikiangalia mfano wa vijana wa Mikoa wa Katavi naona hata aibu kuongea. Vijana wamekuwa na moyo wa kuitikia mwito wa Serikali, wameunda vikundi vyao, wameanzisha ajira mbalimbali kama vile ufyatuaji wa matofali, kilimo cha bustani kwa maana ya mboga na matunda, kilimo, lakini badala yake wale Maafisa Maendeleo ya vijana katika Halmashauri wamekuwa hawako karibu nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wanapajaribu kutaka kuona ni jinsi gani watapata mikopo, ile mikopo kwa kweli hawapati, wanaishia kuhangaika, hata kale kadogo walikokuwa wameanzisha wanajikuta kanateketetea na wanakosa mwelekeo na ndiyo mwanzo wa vijana kukaa vikundi badala ya kuji-group wazalishe mtando wa kufanya kazi, lakini badala yake wanakaa sasa vijiweni kupoteza muda na kuanza kushawishiana kushiriki katika mambo potofu ya tabia za ajabu kama uvutaji wa bangi na kutukana watu. Hawana kazi ya kufanya, sasa wafanye nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iwaangalie hawa vijana kwa macho mawili. Vijana ndio nguzo ya Taifa, hasa ukizingatia kwamba wao ndio wengi, kwani ni asilimia 60. Kwa hiyo, Serikali ingewaangalia sana vijana, jamani tunakokwenda ni kugumu sana kwa sababu hawa ndio tegemeo letu katika Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya vijana, kundi linalofuatia ni akina mama. Ukimwelimisha au ukimpa (*support*) nguvu mama mmoja, basi umeokoa familia na Taifa lote kwa ujumla. Hata hivyo, akina mama wamekuwa wakijaribu na kujihangaikia wenyewe katika kutafuta namna ya kuzalisha mali, mikopo wanaisikia tu lakini hawajui watafanyaje waipate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna huu mfuko wa hizi fedha za Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. Hizo kwa kweli akina mama au vijana wamezitegemea kwamba zingewasaidia. Lakini kwa vijana na akina mama wa Mpanda tuliihia kufukuza inzi tu, hatujui tufanye nini. Mikopo tunaisikia tu hiyoo, inaruka, inapita, inatuacha Katavi tumetulia. Naomba kwa kweli Serikali iangalie, iwawezeshe akina mama na vijana kupata mikopo ili tuweze kwa kweli kuwaokoa vijana hawa, warudi katika maadili mema. Maana yake tutaishia kuwalaumu tu, lakini tunawaona. Vijana, wafanye nini sasa? (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hapo nimemaliza, sasa naomba niende kwenye suala la utamaduni. Katika suala la utamaduni, kwa kweli maadili yameporomoka sana. Utamaduni wa Mtanzania sasa unatukimbia, japokuwa bado utamaduni upo, lakini maadili yameanza kupotea. Labda naweza kuwasifu wenzetu wa kabile la Wamasai kwamba, kidogo ndio bado wanana kwenye utamaduni wao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wa makabila mengine, naona kwa kweli tumpoteza mwelekeo na hii yote nailaumu Serikali kwa sababu ndio imekuwa ikikumbatia mambo mengi katika vyombo vya habari. Vyombo vya habari vimakuwa vikitangaza mambo mengine ambayo kwa kweli ni kinyume cha maadili. Lakini Serikali inaangalia tu na macho. Mimi naiona Serikali kuwa ni sawa na mama ambaye analea familia, watoto wote wanamwangalia mama atasema nini, kiasi kwamba kama mtoto akipotea kimaadili labda amepita akiwa amevaa mavazi yasiyofaa. Mama anatakiwa kung'aka ili mtoto aelewe yuko katika upande gani au afuate msimamo gani. Lakini Serikali yetu imekuwa ikiangalia na macho na haitangazi kipi kibaya na kipi ni kizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika suala la ushindani huu wa ma-*miss*, kwa kweli hawa ma-*miss* wanapokuwa katika ushindani, watoto wetu naona kama wanadhalilishwa sana. Sijui ni biashara za kimataifa au ni nini? Nashindwa kuelewa. Kwani nikijuliza, sipati jibu. Yaani hata kama baba amekaa anaangalia mtoto wake, amekwenda kugombea u-*miss* kule, kama baba ana wageni wamemfikia pale, sidhani kama atamtambulisha yule mgeni kwamba haloo, mwone mwanangu yule anagombea u-*miss*. Sidhani! Ni aibu! (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wetu wanadhalilishwa, wanavishwa vichupi, wanavaa vinguo ambavyo havina heshima. Sasa sijui tunashindania nini? Hivi Serikali imeshindwa kutafuta kigezo kingine cha kumtambua mshindi kwa kumpima mtoto labda uwezo! Eeh! mpaka tupitie hatua ya kucaa nguo za kuonyesha nusu uchi! Jamani, naomba turudi katika maadili. Serikali ijithadi kurudi katika maadili ili kusudi tupate Taifa la kesho lililo bora na vizazi vijavyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia upande wa utamaduni huo, watu tunaiga mambo ya nje, hatujui tunakokwenda, ni wapi na vizazi vinavyokuja tunavipeleka wapi? Wengine tumefikia hata hatua ya kukataa vyakula ambavyo ni asili yetu. Mtu hawesi kula kiasi kilichochemshwa kwa maganda, anataka mikate, anataka jam, vitu kutoka nje, wakati sisi wenyewe Watanzania tuna uwezo wa kuzalisha vitu vizuri na vyakula vizuri kama hivyo tena vya asili, ambavyo vina faida sana katika miili yetu. Lakini tunaiga iga, tunapata vitu ambavyo wakati mwingine havina faida na sisi na kwa vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naiomba Serikali iwjali sana hawa wacheza ngoma za asili kwani wamesahaulika sana. Serikali haiwijali, inawahitahi tu labda unapopita Mwenge, ndio inawaona kama wana thamani. Mwenge ukipita ndio tunaagiza sasa ngoma za asili wakahangaike juani na hakuna Serikali inachowalipa zaidi ya wao kuhangaika na kupewa labda

pombe tu, wanaishia kunywa pombe, basi. Lakini wacheza ngoma za asili ni muhimu sana katika Taifa letu.

Naomba Serikali ingewakumbuka sana kwa sababu hawa ndio watarudisha utamaduni wa nchi yetu kupitia vizazi vinavyokuja. Hiyo ni kumbukumbu tosha. Lakini hata Mawaziri wanapotembelea labda mashule, ni aibu sana wanaimbiwa nyimbo za Bongo Fleva na wanafunzi; wapi na wapi jamani! Ngoma za asili ndiyo utambulisho wa nchi yetu na makabila yetu. Naomba Serikali iliangalile hilo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ingefanya michezo ni lazima, siyo hiyari. Michezo irudishwe mashulenii tena kuanzia Shule ya Msingi ikiwezekana ianzie katika Shule za Chekechea kabisa. Pia kuwe na ushindani, hata katika baadhi ya sikukuu za kitaifa, tuwe tunashuhudia mechii ya Shule za Chekechea. Miaka 12 wanaanza na wenyeewe kuandaliwa mashindano na hapo ndiyo tunatafuta watoto wabunifu na wachezaji wazuri wa baadaye badala ya kusubiri mpaka wamemaliza Darasa la Saba ndipo tuanze kutafuta watoto wa kucheza mpira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kupata wachezaji wazuri kama tutaanza kuwatafuta watoto wa kucheza mpira wakiwa labda na miaka 20, hatuwezi kumpata mchezaji mzuri. Mchezaji mzuri ni kuanzia utotoni. Tunaomba Serikali irudishe michezo kuanzia Shule za Msingi au Chekechea kabisa. Kipaji cha mtoto tunaanza kukiona akiwa mdogo. Kwa hiyo, michezo irudishwe, iwe ni lazima na siyo hiari. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani kulikuwa na michezo sana. Katika masomo kulikuwa na kipindi kimetengwa kwa ajili ya michezo. Naomba sasa hivi vipindi vya michezo virudishwe mashulenii. Kuwe na kipindi kabisa cha michezo, baada ya masomo mengine inafuata michezo. Kama ilivyokuwa enzi zetu, kulikuwa na michezo mingi. Riadha, *netball, football, high jump, long jump*, michezo kama kukimbilia kwenye magunia, eeh! Ni afya tosha kwa vijana wetu kwa sababu michezo ni afya, ni ajira na ni burudani. Leo katika vizazi vyetu hivi ukimwona kijana wa sasa ni kama bamia. Jamani! Eeh, kwa sababu hawana kabisa nafasi ya kushiriki katika michezo. Hawapati michezo shulenii, wanaipata kwa muda kama pale tunapoandaa mashindano ya UMITASHUMTA au UMISETA. Hapo ndiyo mazoezi yanaanza. Wapi na wapi! (*Makofî*)

(*Hapa kengele ya pili iligonga kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. ANNAMARRYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuni pa wasaa ili nami niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza, niwapongeze Waziri, Naibu Waziri na wote kabisa waliohusika katika kuandaajabu au hotuba hii. Hotuba imeeleweka vizuri tu sana, inatia matumaini, lakini kuwa na hotuba ya matumaini ni kitu kingine na kuweza kuitekeleza ni suala lingine. Tunawaomba tu kwamba pamoja na pesa ndogo waliyopata, basi ndani ya mpangilio waendelee kupangilia kipaumbele zaidi cha haya yaliyomo, vinginevyo, yote yanaweza yakashindikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naanza kwanza kujikita kwenye masuala ya michezo. Nilivyo sio mchezaji, najua tu karata, lakini nadhani nawajibika kwa vile mengine naya fahamu, hivyo nizungumzie mawili, matatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeisoma hii hotuba kwa makini kidogo, lakini imenipa majonzi ya kutosha tu, kwa sababu sikuona kinachonifurahisha kuhusu michezo ya watu wenye ulemavu. Kumekuwepo na kuto kuwezesha kikamilifu sehemu hii ya michezo ya jamii hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyofahamu mimi, watoto wenye ulemavu, wakubwa zao, mababu zao wanashiriki kwenye michezo inayoweza kuchezwa na wao. Kwa mfano, ile michezo

ya ya kutupa vifaa vizito, *basketball* ya kutumia baiskeli, riadha, *football*, wanacheza hawa. Katika kucheza kwao, wameshawahi kutuwakilisha huko kwenye Mataifa ya mbali. Kila mara timu hizi zinapajaribu kwenda nje, mara zote wamerudi na medali tofauti na michezo inayochezwa na watu wenye macho, miguu na masikio wakati mwingine wanarudi bila kitu (zero). Hawa wanarudi na medali, na medali hizi ni sifa ya Taifa hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mpaka kufikia hatua ya nchi yetu kufahamika nje kutokana na walemavu hawa kufanya juhudhi, wenye ulemavu hawa hawasaidiwi kikamilifu wakati wa maandalizi ya hayo mashindano. Kuna walioleta medali 11 mwezi wa Sita tu, kama Vyombo vya Habari navyo tunavisikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuvishukuru kabisa vyombo vya habari, kwamba vinathhubutu kabisa kutoa taarifa ya mambo haya. Wale walikuwa watu wenye ulemavu wa akili chini ya Olimpiki maalum, walikwenda kushindana kimataifa, wakarudi na Medali 11 mwezi wa sita, nchini hapa. Lakini maandalizi yao pale walipoweka Kambi *salvation army* Dar es Salaam yalikuwa yanasicitisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kwa sababu hata huduma muhimu za maana zile zilikosekana na mjue kwamba, kwa watu wenye ulemavu kama ni elimu yao, kama ni kazi zao zinagharimu zaidi kuliko michezo ya wazima. Kwa hiyo, hata kuangaliwa wanahitajika waangaliwe zaidi kwa sababu wana mahitaji maalum ya ziada ili kuweza kufanikisha chochote kile ambacho mtu mwenye ulemavu anapaswa kukitekeleza au kukifanikisha nchini. Hata chakula kilikuwa tatizo, wasaidizi waliwekewa wachache tu.

Kwa mfano, kwa upande wa ulemavu wa akili mtoto mmoja anahitaji kuwa na wasaidizi hata wawili. Mwingine anacheka hovyo, mwingine anafanya hivi, wanapaswa kusaidiwa wale, lakini wasaidizi walikuwa wachache. Makocha walikuwa wawili tu wa kuwaelekeza hiyo michezo yote ambayo walikwenda kushiriki huko mbele ya safari. Hivi Serikali hawakulijua hili? Kwanini tunaachia tu chama kinachohusika? Kama vyama vikubwa vinasaidiwa sijui na *TFF*, sijui na wadhamini gani, sembuse vyama vya michezo vya watu wenye ulemavu?

Hamjui kwamba havina fedha wala uwezo ni moyo tu wa kwenda kuwakilisha nchi za nje, hawakusaidiwa. Kama ni msaada unakuwa sijui wa tiketi ile ya kwenda kule, lakini hii tiketi utampeleka huko kwa kushinda kitu gani kama huku nyumbani hujamsaidia kumtayarisha huyu mtu. Matayarisho ya wanamichezo wetu tena hapa sio tu kwamba wenye ulemavu, matayarisho ya wanamichezo wetu katika michezo mbalimbali wanapokwenda nje, jamani inakuwa sio mizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nimesikiliza kwenye vyombo vya habari wanariadha wanaokwenda sijui Mozambique wanalamika, *netball Taifa Stars* sijui timu gani ile Twiga wanalamika, inakuwaje hatuwezi kushinda kama maandalizi huku nyumbani hatuyavalii njuga, halafu tunasema tunarudi watu wendawazimu. Sasa kama huku nyumbani kwenyewe ndio tunakaribisha uendawazimu, kule watakwenda kuponyeka na uendawazimu si watarudi tu hivyo hivyo. Kwa hiyo, hili limenisikitisha pamoja na kwamba watoto hawa wamerudi na medali lakini hawakusaidiwa. Sasa kinachofurahisha ni kwamba tunafurahia tu ushindi, lakini maandalizi hatuyakamilishi. Mimi ninaomba sana michezo ya kundi hili ithaminiwe wasaidiwe kuandaliwa kwa sababu mara zote wamerudi na ushindi. Kila mwaka wanaposhiriki wanarudi na ushindi sasa kwa nini tusiendelee kuwapa moyo? Kwa nini tusiwathamini na wao wanatuletea kinachofaa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho ningependa kukizungumzia ni juu ya vyombo vya habari. Vyombo vya habari navishukuru kwa ujumla wake televesheni, magazeti pamoja na kwamba wakati mwingine ndio hivyo tunawalamikia kwamba aah, wanaandika andika wanatuonyesha vitu ambavyo havisaidii, nadhani wameshasikia itabidi wajirekebishe. Lakini kwa upande wangu nashukuru vyombo vya habari vinapoenda kwa masuala ya watu wenye ulemavu kwa kweli hawaoni kuvitoa vile vitu hadharani. Kwa mfano mwenye ulemavu anapohitaji kitu, juzi tu hapa kama mme-note *TBC* Dodoma ilimsaili kijana mmoja ambae ametoka Kondoa na baiskeli iliyotengenezwa na mbao, sijui wenzangu mliiona? Kokocho kokocho amejieleza *TBC* wamemuonyesha. (*Makofii*)

Nishukuru wafadhili na hasa *TBC* basi iliyo *disclose* hiyo *scenery* yule kijana jana tu amepata balskeli na mfadhilli amekataa kumuelewa ni nani lakini mimi kama mwakilishi wao imebidi nimshukuru sana yule baba, naishukuru sana *TBC* kama chombo kimojawapo cha habari na vingine vyote vimeshawahi kufanya hivyo, watu wanasaidiwa watu wanaelewa kwamba ni kitu gani kinachoeleweka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa *TBC* hapo hapo naomba niilize Serikali. Ni muhimu sana utamaduni wetu tuenzi na tuuhifadhi. Hivi kwa nini kiashiria cha Taarifa ya Habari ndani ya *TBC* mmeweka sasa mviringo tu nje nje nje nje!!! Yule aliyekuwa anapiga tarumbeta juu ya Mlima wa Kilimanjaro kwa nini mlimtoa? Mbona yule alikuwa anaonyesha utamaduni na alikuwa anaonyesha fahari ya Tanzania ule mlima. Sasa hivi utasikia *so so so so!!!*

Mimi hata sivielewi vitu vile vinaelimisha nini? Vile vinaelimisha nini, utamaduni tunauenzi pipi? Kwa taarifa ile mimi nadhani wengine walitaka kuona aah!! Hii Kilimanjaro ndivyo ilivyo hata hao walipo nje. Sasa yametolewa yale, sijui ndio uzungu, sijui ndio utamaduni tunausahau mimi hata hakinifurahishi. Akinifurahishi Mheshimiwa Mwenyekiti na nilishauliza swali hapa, nilivyojibwa jibowi basi hivyo hivyo. Nililiza kwa ajili ya kuumia sioni maana utamaduni ule urudishwe. Kama hatumrudishi Mzee Nyunyusa yule wa ngoma 12 kwamba ni *old fashion* lakini hata huyu mbona bado ilikuwa inaleta ile *essence* ya Utaifa jamani. Nadhani mmenielewa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo nizungumzie Mfuko wa Maendeleo wa Vijana. Naipongeza Serikali kwamba mwaka hadi mwaka inasema inaimarisha Mfuko huu kwa kuongeza fedha ili kwa kupitia *SACCOS* vijana kukopeshwa. Lakini hapa tu naomba nitoe ushauri fedha hizi za Mifuko ya Vijana hasa kwa kupitia Halmashauri kule, vijana wenye ulemavu katika maeneo mengi walikuwa hawapati. Naipongeza Shinyanga tu waliweza kufanya kitu kama hicho, lakini kwingine kote hawaangaliwi hawa. Kwanza hawajui, kwa hilo la msingi hapa Maafisa Maendeleo wa Vijana kwenye Halmashauri zetu basi *wa-take effort* kuvalimisha hawa ndugu zangu kwamba mnapaswa kujunga ndipo iwe hivyo, vinginevyo ni haki ambayo inapotea tu kwa sababu hawaijui na wala hawashirikishwi.

Kwa hiyo, ninaomba pawe na maelekezo maalum kwa Maafisa wanaohusika kuweza *ku-mobilise* hawa watu ili waweze kufaidika kama vijana wenzao wanavyofaidika pamoja na kwamba msemaji aliyejita anasema hata huko kwao hawafaidiki. Kwa kweli huu Mfuko una matatizo kweli kweli. Sijui sasa hivi kwa sababu mnaupitishia kwenye ma-*SACCOS*, vinginevyo ilikuwa ni shughuli nzito. Afadhal hata ule Mfuko wa Maendeleo wa akinamama kwa sababu mimi nilikuwa ni mmojawapo wa kukadiria kwamba kikundi hiki kinafaa, kikundi hiki kinafaa, huu Mfuko nao uweze kuangaliwa kikamilifu. Kwa hiyo, ninaomba sana ndugu zangu hawa waweze kufaidika na mabadiliko haya na wao ndio maskini wa maskini katika maisha. Kama kijana wa kawaida mnasema ni maskini ana hali ngumu hawa vijana wenye ulemavu ndio tatizo kupita kiasi. Ndio hao mtawaona mabarabarani wanaendelea kuomba na wanaonekana kuwa ni mzigo wa Taifa kwa sababu tumewasahau mno kuliko hata wao wengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya naunga mkono hoja, lakini naomba haya niliyoyashauri timu za michezo za watoto wenye ulemavu zipate *support* na Serikali wanatuletea faida. Mfuko huu wa wenye ulemavu nao wafaidike na *TBC* mrudisheni yule baba wa kipenga juu ya Mlima wa Kilimanjaro. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, namwita sasa Mheshimiwa Murtaza Mangungu pia Mheshimiwa Donald Max ajiandae, Mheshimiwa Martha Mlata ajiandae na Mheshimiwa Susan Lyimo ajiandae. (*Makofii*)

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hotuba ya Makadirio ya Wizara husika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijachangia ningependa ku-*declare interest* kwamba kwa mujibu wa Kanuni 61 ya Bunge. Mimi ni Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa *TFF* kwa maana kwamba kule tukienda tunalipwa posho, kwa hiyo, kuna mengine naweza nikasema yana maslahi ya kifedha na mimi. (*Makofii*)

Mchango wangu utasimama katika mambo matatu, kwanza kabisa nitakuwa na lawama, pili nitakuwa na ushauri, lakini pia nitakuwa na pongezi. Lakini kwa kuwa fikra za mwanadamu zimejengeka zaidi katika mambo mazuri kwa hiyo naomba Mwenyekiti nianze kwa pongezi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi za kwanza nawapongeza Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi pamoja na Naibu wake kwa hali ya moyo wa kujitolea katika kusimamia na kuendeleza michezo na utamaduni katika nchi yetu. Pongezi za pili napenda nkipongeze Chama cha Waandishi wa Habari wa Michezo chini ya Mwenyekiti wake Bwana Juma Pinto kwa tukio la kihistoria kabisa ambalo wamelianzisha kutoa zawadi kwa wanamichezo wanaofanya vizuri lakini zaidi kwa kumtunukia tuzo maalum Rais wa Awamu ya Tatu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa katika tuzo hilo zilizofanyika mwezi uliopita kwa jitihada zake za kukuza michezo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nimpongeze Rais wa *TFF* Leodgar Tenga kwa kuteuliwa kwake kuwa Mjumbe wa Kamati ya Utendaji wa Shirikisho la Soka Barani Afrika (*CAF*). Lakini pia nampongeza Naibu wake Athumanu Nyamrani kwa kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Bodi ya Rufaa katika Shirikisho hilo la Soka la Afrika. Napenda pia kuzipongeza timu za Azam na Mtibwa kwa jitihada zake za makusudi kwa mshikamano wake wa dhati kabisa katika kuendeleza soka la Tanzania, huu ni mfano wa kuigwa na wanastahili kupata pongezi za kutosha kabisa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, makocha wazawa ninao wachache amba o nitawatamka hapa lakini ni wengi amba o wanastahili pongezi. Jamhuri Kiwelu, Silvester Mashi, Salum Mayanga na Ramadhani Aluko wamefanya kazi kubwa sana ya kuibua vipaji katika nchi yetu. Michezo mara zote inahitaji ioneshwe na isikike.

Lakini wapo waandishi amba o wamekuwa wanaandika makala ya aina mbalimbali kusaidia kuinua michezo na kusaidia kuelimisha michezo. Nampongeza sana Keny Mwaisabula, Kambi Mbwana, Abdurahman Kipenga na Edo Kumwembe kwa makala ambayo wanatoa katika vyombo mbalimbali vya habari, lakini siwezi kumsahau Shafii Dauda na Alex Luambano kwa uchambuzi wao makini wa michezo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa michezo, nikifuata kitabu hiki cha hotuba nasema kabisa sitowenza kuchangia kama vile ambavyo mwenyeze mtazamo wangu unavyoona na hali halisi iliyyo. Mchango wangu wa maandishi nimeuwasilisha hapo kwa Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo, utawiana zaidi na kitabu hiki cha hotuba ambacho wametugawia. (*Makof!*)

Mimi ni mkweli na dua yangu kwa Mwenyezi Mungu kila siku naomba anieu nikiwa nasema ukweli. Sasa hivi timu yetu ya Taifa imepoteza mwelekeo na haina dira, ni ukweli usiofichika kocha hatufai. Kocha wa Timu ya Taifa hakuna jambo hata moja ambalo ameweza kutufanya mpaka hii leo tuisubiri mpaka tuzidi kuharibikiwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la michezo mapendekezo niliyoyatao hapo kwa Serikali kuititia Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wetu wa Awamu ya Nne ametoa fedha nyinyi sana ukiangalia wastani zaidi ya dola 30,000 zinapotea kila mwezi kuwalipa makocha wa kigeni. Malazi yao na usafiri wao makocha hawa hawana msaada wowote, kwa nini fedha hizi tusijielekeze kuwasaidia vijana wetu hapo Watanzania wenzetu wakaenda Ulaya kwenda kujifunza au kwenye nchi zilizoendelea wakaja kufundisha mpira hapo? Ni jambo ambalo linastajaabisha sana unawezaje kutengeneza timu ya Taifa bila ya kutengeneza msingi? Walimu wa shule za msingi amba o wanakuza vijana hawana elimu ya michezo, makocha amba o wanafundisha timu za daraja la pili, la tatu, timu za mikoa, wilaya hawana ujuzi. Sasa kwa nini tunaelekeza fedha hizi zote kuwanufaisha watu wawili tu wakati tungeweza kuwanufaisha watu wengi zaidi? Hili nasema mliangalie vizuri na mliangalie kwa makini. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hapo tunazungumza na Serikali, tunaishauri Serikali kama Katiba inavyotamka Bunge kazi yake mojawapo ni kuisimamia Serikali, naishauri Serikali ifute

ushuru kwenye vifaa vya michezo. Vifaa vya michezo vinakuwa ni ghali sana kutohana na bei kuwa juu na ushuru kuwa mkubwa. (*Makofi*)

Kwa kuwa kengele ya kwanza imelia mengine itabidi niyaruke, lakini nataka nizungumzie suala la wasanii pia. Wasaidiwe kwa namna ya kipekee, wameonyesha wanawenza. Wasanii hawa siku zote wamekuwa wanalamika ni jambo la kustaa jabiswa kwamba kazi zao zinaibiwa, kazi zao zinaibiwa na hakuna hatua zinazochukuliwa. Imekuwa ni hoja hapa hata *mastering studio* kwa nini tusianzishe kwa umoja walionao? Tuwagawie japo *mastering studio* moja wakawa wanahifadhi kazi zao na wanajizalishia wenyewe kuliko kuhanganya na hawa watu ambao wanawanyonya kila siku. Lakini pamoja na hayo kuitia Bunge hili naomba niwashauri wasanii nao vilevile wajiheshimu. Tumechoka kusoma kashfa katika magazeti na vyombo vya habari zinazowahu wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa asubuhi kulikuwa na hoja kwamba vyombo vya habari vinapotisha ukweli, inawezekana ikawa ni kweli, lakini Serikali nayo ivunje ukimya iwe inatoa taarifa za kweli wasisubiri mpaka vyombo vya habari vipotoshe, tusiwakemee tu. Mimi ni Mjumbe katika Bunge hili kwenye Kamati ya Mahesabu ya Mashirika ya Umma, namshukuru Mzee Mwambalaswa hapa amezungumza, lakini ninachosema kwamba vyombo vya Serikali vya *TBC/TSN* visaidiwe kulipa madeni yake. Tumepitia hesabu zao wanadai karibu shilingi bilioni 4.5. Mnataka wajideshe wapanue huduma, watajiendeshaje na Serikali yenyewe na Mawizara hayalipi fedha katika vyombo hivi? Sasa tusifanye hadithi za kuwashimiza kuwafanya wafanye kazi bora wakati sisi wenyewe hatupo tayari kuwasaidia kwa kuwalipa kazi ambazo wanazifanya kuitia vyombo hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa nitaomba hili nipaatiwe maelezo na Waziri wa Michezo hali iliyokuwepo kwa wanamichezo wanaokwenda kwenye *All Africa Games Mozambique* ni mbaya. Malalamiko hayaishi kila siku vyombo vya habari, wanariadha wanalia, wana ngumi wanalamika kila aina ya michezo. Hivi kweli kama Serikali kutoka hapa kwenda Mozambique tumeshindwa kupeleka wanamichezo wengi tunapeleka wanamichezo 60 kati yao karibu 20 ni viongozi.

Mimi nimeongea na Mheshimiwa Shabiby hapa alikuwa yupo tayari kutoa mabasi yake kupeleka mpaka Mozambique. Serikali kweli haina uwezo wa kukodi mabasi mawili kuwapeleka wanamichezo zaidi ya 100. Kuna maboti, Mozambique tunaweza kwenda kila namna hata majahazi yapo. Kwa sababu kama tungenesema kwamba tuchukue waogegeleaji wasingeogopa kusafiri kwenda Mozambique kwa kutumia majahazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo ambalo namwomba Mheshimiwa Waziri sio kwa kusubiri mpaka tupate adha kwa kusubiri mpaka jambo lingine lolote. Nataka litolewe tamko kwamba wanamichezo wanaongezeka kwa sababu hatutokuwa na nafasi nyingine zaidi ya kuwapeleka wanamichezo wengi katika mashindano ya *All Africa Game*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Namwita sasa Mheshimiwa Donald Max, Mheshimiwa Martha Mlata ajiandae na Mheshimiwa Sabreena Sungura ajiandae. (*Makofi*)

**MHE. DONALD K. MAX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote naomba nimpongeze Waziri wa Wizara hii Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi, kwa sababu mimi ni Mjumbe kwenye Wizara hii. Nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Fenella Mukangara, nimpongeze sana Mheshimiwa Jenista Mhagama ambaye ndiye Mwenyekiti wetu. Lakini pongezi zaidi ziende kwa Msemaji Mkuu aliyezungumza leo, mdogo wangu ambaye ametoa hotuba nzuri sana na kutukumbusha alikotoka ndugu yetu Juma Nkamia, nimpongeze sana. Hotuba imesikika vizuri, simu tumepokea nyingi kwa hiyo, tunaomba awe na moyo wa kuendelea kutuelimisha kwenye hilo. Naomba tufike mahali sasa haya masuala ya makabasha yaanze kupungua. Tunaweka mikakati, tunatoa fedha utekelezaji unashindikana. Marehemu Baba wa Taifa alipofanya makosa aliandika vitabu na tunavisoma kwamba ingekuwa nianze upya miaka 25 mingine makosa haya nisingefanya. Hapa tulipo tunaendelea na makosa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mzee Mkapa, Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu amezungumzia sana umangimeza, ubinafs i kwenye Wizara zetu. Huu ni mzigo mzito kwa sababu bahati nzuri Waziri Mkuu yuko hapa labda wengine wanaogopa kusema lakini ukweli ndio huo. Mawaziri na Naibu Mawaziri sio wenye mzigo mle ndani ya Wizara, matatizo yako kwenye utendaji. Washauri hawapo, utakuta Wizara ina Msemaji wa Wizara, utakuta ina Wanasheria, lakini wanashindwa kuwashauri, kwa sababu mtu kama Waziri anabeba Taifa, habebi jimbo anaangalia mikoa 24, Wilaya 100 na kitu yeye ana mzigo mzito kuliko mimi mwenye Jijimbo lenye kata 19, vijiji 136. (*Makofii*)

Kwa hiyo, anapofanya kazi yake anaangalia Taifa kama Taifa, haangalii Jimbo lake haangalii Mkoa wake. Sasa kama hawasaidiwi maendeleo yatakuwa magumu sana. Kwa kiliingereza tunasema *charity begins at home*. Hapa nyumbani tunashindwa hata Mheshimiwa Rais mnashindwa kumshauri. Nimshukuru Mheshimiwa Mwambalaswa, Mheshimiwa Mangungu wamezungumza vizuri. Tunatumia *five billion* kumweka Maximo hapa nchini for ten years. Hiyo *five billion* sasa hivi tungejigawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni mia moja wangekwenda kwa sababu na sisi tulisomeshwa na Serikali zilikuwa zinakuja *scholarship* mia moja tunasoma nje tunarudi kutumikia Taifa. Kule wenzetu kila mmoja ana utalaam wake. Mimi kama mimi ukinipa watu mia moja, watu 25 nitawapeleka *Latin America*, kama Brazil au Argentina, wengine 25 nitawapeleka *Seria A*, 25 nikawapeleka pale Uingereza wallobaki nitawapaleka hata kama ni Ujerumanu au wapi ili kusudi Mikoa yetu 24 inaweza kuwa na makocha wa Kimataifa kila baada ya miaka mitano tuktoa makocha hata 20 au 30 nchi hii itakwenda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema kuihamasisha michezo ni kama kwenye kilimo tupo pale pale. Wewe unaniambia Kilimo Kwanza leo nakulimia hekari 1,000 sijui nyanya nikilima naipeleka wapi kutengeneza *Tomato Sauce* na kwenye michezo ni hivyo hivyo. Tumehamasisha ndugu zetu vijijini kila mahali. Mpango wa MMEM tumejamishwa na Mpango wa MMES. Leo tunazungumzia michezo, sijasikia Serikali inasema kwamba tujlandae vipi na michezo. Tumelipigia kelele na mpaka leo linaendelea. Unapojandaa kwa michezo watu wenye taaluma wapo wengi nchi hii. Tupo milioni arobaini na kitu na wakati nachangia kwenye Wizara ya Uchukuzi nilisema wataalam wengi wamo humu ndani ya Bunge. Lakini nashangaa Wizara hazitaki kuwatumia wala Serikali haiwahitaji kutoa michango yao. Siamini kama Serikali itashindwa kutoa *exemption* kuleta hata kontena 20 za mipira na jezi tukaanza mashulenii, hilo siliamini. Kwa sababu kama tunesema vifaa vya michezo watoto wetu hawana pesa, Serikali itoe *exemption*, makontena yaingle hapa, Halmashauri zipo, Madiwani wapo, Wenyeviti watendaji wapo, wenyeviti wa Serikali wapo. Shule zote zitakuwa *accommodated*. Huyo huyo Diwani anayebeba Kata sita mnampa kazi kwamba ongea na walimu wako, pekua shule zako, kila shule itutolee wachezaji wawili tuanze kuchuja, sasa hizo programu hatuoni. Tunaandika kwenye makabasha makubwa kama haya mambo mengi sana lakini kwenye utendaji huwa hakuna. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye uwajibikaji. Kama nilivyosema watendaji wetu lazima wasaidie Mawaziri. Tunalipa pesa, tunapitisha haya mahela, mtu anakaa ofisini halii ambayo tunayoikabili sisi vijana, mtendaji hajakanyaga hata siku moja, Afisa Michezo yuko pale Wilayani hana pipipiki, kupewa gari na Halmashauri ni kazi, hiyo michezo itaendeleaje?

Kwa hiyo, unakuta kwamba zile takwimu za kujua shule ziko ngapi zinazocheza mipira, shule za sekondari ni ngapi, *form five* na *form six* wangapi, vyuo wako wangapi? Lakini Waingereza walisema *charity begins at home*. Humu ndani tupo Wabunge 367 tukiwaacha dada zetu na mama zetu hapa, humu ndani peke yake kuna timu ishirini za watu kumi na moja, kumi na moja. Lakini inashangaza kwamba Bunge linaunda timu moja. Kwa nini sisi tunakuwa wazembe, bila kuonyesha mfano hatuendi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naomba hata wale ambao wanaona hawawezi kukimbia. Tuanze humu, iwepo A, B, C, tuwe na hata timu tatu. Leo katika watu 367 katimu kamoja kashindane na *British Council*, ni aibu. Kwa sababu na sisi lazima tuonyeshe mfano, wacheza mpira tumo humu humu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende *TBC*, tunasema kwamba Serikali hairuhusiwi kufanya biashara, mimi hilo kwa upande huu naomba Miswada mingine iwe inakuja tunajadiliana. Mimi siwezi kukubali zile nyaraka za *TBC* ambapo ile maktaba imechoka, ukiangalia zile kanda za plastiki toka Uhuru zimo mle na zinaota ukungu. Tuwe na machungu, hii nchi ni yetu. Vita ya Majimaji, Machifu wetu akina Adam Sapi, marehemu Masanja na Fundikira nyaraka zitapotea. Mimi sidhani kama Taifa letu liltakuwa linalewa hawa wazee walitutoa vipi kwa mkoloni, zile nyaraka zinapopata ukungu zikaharibika hatuzipati tena.

Mimi ninaombala Serikali najua sina ubavu huo, ninachokiomba ni kitu kimoja, *TBC* ina jengo, Serikali itoe *guarantee* wakope hela benki, wamalizie hili jengo kubwa, kuliko hali walijonayo sasa. Wana jengo dogo ambalo ni la zamani na haliwatoshii lile jengo jipya wanatumia *floor* chache baada ya kutembelea huko unaona mafaili yanapitishwa barabarani kutoka *TBC - A* kupelekwa *TBC - B*. Yule mtu anayepitisha hayo mafaili siku akipigwa ngwala zikaibiwa nyaraka ina maana Taifa lipo kwenye janga. (*Makofii*)

Kwa hiyo, mimi naomba itafutwe namna Serikali inaweza kuidhamini *TBC* ikapewa pesa tumalize hilo jengo, wote wakae kwenye kivuli kimoja na lile jengo linaweza kuuzwa ili kusudi *TBC* ipate mtaji mkubwa kwa sababu tunaangalia miaka 50 mbele. Leo tunatimiza miaka 50 tupo watu milioni arobaini na miaka 50 ijayo tutakuwa *almost eighty*. Kwa hiyo, mimi naomba hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye michezo, *TFF* inapokea dola laki tano kila mwaka karibu shilingi milioni 600. Kwa nini haiwezi kutenga asilimia hata kumi kwa ajili vijana? Wao wamekuwa nani? Watasiwiwa sana lakini nasema hela ile inatolewa na *FIFA* kuendeleza michezo, vijana kwa nini wanatengwa? Kwa sababu taarifa ya habari ya asubuhi leo, dada zetu wanatafuta pesa wacheza gofu kwa ajili ya nauli ya kwenda kwenye mashindano. Ni aibu sana kwa Taifa na wakati *TFF* ipo na ndio chombo chetu kikuu. Kwenye utamaduni hapo ndipo panachosha, utamaduni umeisha. Kwa sababu vijana wa leo hata nchi hawajui ina makabila mangapi, ngoma gani tulikuwa tunazicheza. Ni aibu sana. Mimi ninachoomba ile dhamana yetu ndani ya maktaba, vijana wetu wajue Watanzania tunaishi kwa amani na tunacheke pamoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahante sana. (*Makofii*)

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii. Nampongeza Waziri na Nailbu Waziri na timu yake yote kwa hotuba ambayo ameiwasilisha hapa. Lakini naomba nianze kwa kutoa pongezi za dhati kabisa kwa timu ya msamaria ya mpira wa miguu ya Manyoni ambayo imefanikiwa kuingia daraja la kwanza na sasa hivi wako Tanga. Kwa hiyo, nawatakia kheri na ushindi tupo pamoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme pia Mkoa wa Singida una hazina kubwa sana ya watu wenye vipaji hasa vijana wenye mbio na mara nyingi wamekuwa wakikimbilia Arusha. Sasa ninamwomba Mheshimiwa Waziri kwa kutambua hilo naomba utuletee chuo cha mafunzo ya riadha pale Singida ili uweze kupata hazina kubwa sana katika Taifa hili na kuongeza ajira kwa vijana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba niwazungumzie na kuwapongeza waandishi wa habari wa Mkao wa Singida kwa kweli wanafanya kazi nzuri, kazi kubwa sana japokuwa kazi yenye kazi kwa mazingira magumu sana, hawana vitendea kazi wengi wamekuwa wakijitolea kwa fedha zao wenyewe, hawana usafiri, hawana jengo. Kwa kweli wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu lakini ni kazi nzuri. Niwaombe tu wadau na wapenzi wa mambo ya habari kwa ile *Press Club* ya Singida tuwasaidie waweze kuwa na jengo lao na vitendea kazi kwa ajili ya kuinua Mkao wetu wa Singida, pia kuna suala la utamaduni hasa Maafisa Utamaduni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sielewi Mheshimiwa Waziri naona amezungumza tu lakini ana Maafisa Utamaduni ambao yeche anadhani ni wa kwake lakini hana Maafisa Utamaduni. Maafisa Utamaduni walipo kwenye Wilaya wapo chini ya Mkurugenzi kwa hiyo wapo chini ya TAMISEMI

na TAMISEMI hawana fungu la utamaduni. Sasa sielewi atafanyaje nao kazi kama alivyosema kwenye hotuba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya swalii hilo mimi ninaomba nizungumze kuhusu suala la wasanii. Labda leo nizungumze maana siku zote na miaka mitano iliyopita nimekuwa nikilia ndani Bunge hili na ninashukuru sana sasa nimepata wasemaji wengi wa kutetea jambo hili. Leo naomba nizungumze lakini nikizidiwa basi nitalia, la hasha nitashindwa kuunga mkono hoja kwa mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli wasanii wengi wa Tanzania mpaka sasa hivi hatima yao haijulikani iko mikononi mwa nani. Niliwahi kuzungumza hapa, nikasema kwamba hili dawati la utamaduni kwanza linaonekana halina mwenyewe, hata fungu lake halioneckani na ndio maana hata kazi zake haziendi. Matokeo yake imebaki kuwa ugomvi kati ya wasanii kwa wasanii, kwa sababu hawana mwenyewe. Sasa mimi niliwahi kusema kwa nini isiundwe Wizara ya Utamaduni peke yake, mbona inaweza ikazalisha sana na kuleta pato kubwa sana nchini. Kwa nini bado mnaipachi pachika. Ninaomba itengwe na ikae peke yake kama Wizara nyngine ili kuweza kuainisha mambo mengi ambayo yanaweza yakaleta tija. Sanaa ni biashara, sasa niseme kwamba ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri pamoja na hayo ameweza kusimamia na kuunda mashirikisho ambayo yako manne, kuna la filamu, muziki, sanaa za maonyesho pamoja na sanaa za ufundi. Lakini hivi unawezajaze kumpa mtu mpini wa jembe na unamwambia aende akalime? Hawa watu hawana fungu lolote, hakuna Bajeti yoyote hivi wataanzia wapi hata kufanya kazi zao. Matokeo yake inabaki kwamba kuna majina, kuna mashirikisho sijui lakini vitendea kazi hakuna. Nilikuwa nazungumza nao hapo nje, hata nauli za kuwaleta hapa wamejileta wenyewe. Sasa hizo kazi watafanyaje na tunasema wazunguke nchi nzima kuangalia vipaji vya vijana ili waweze kupata ajira. Mheshimiwa Waziri ninaomba sana litengwe fungu au Bajeti kwa ajili haya mashirikisho manne wapatiwe fedha kwa ajili ya kuanzia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme kwamba kuna jambo ambalo mimi linanisikitisha sana. Sina hakika kama COSOTA kule ilipo ipo mahala pale. Sidhani kama ni mahala pake, kwa sababu imeshindwa kufanya kazi yake. Wasanii wamekuwa wakiibiwa kazi zao lakini bado sasa hivi tunasema sijui *mastering studio*, sijui Mheshimiwa Rais ameipeleka wapi na sijui imekuwaje. Hilo wala si kosa la Rais, wala si kosa la wasanii. Bali Wizara imeshindwa kutimiza wajibu wake kwenye upande wa sanaa na ndio maana mlishindwa kumwelekeza. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge kidogo samahani. Naomba u-declare *interest* yako katika fani hii, itakugharimu sana. (*Makofii*)

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni kweli mimi pia ni mtunzi na ni mwimbaji wa nyimbo za injilli. Kwa hiyo, ni msanii na pia ni mwigizaji. Nimekuwa niki-declare *interest* mara nydingi labda ndio maana leo nimejisahau. Lakini ni kweli na ninafanya hiyo biashara lakini sasa hivi inanishinda kwa sababu ya mfumo mbovu uliopo. Unapeleka kazi zako lakini hupati pesa yoyote, anafaidika mtu mwingine, tumewatajirisha watu wengine ambao hawajatokwa na jasho lolote. Kwa hiyo niseme, Wizara mlishindwa kumwelekeza Rais ni wapi apeleke kile chombo ndio maana kikaangukia mahala ambapo wao walikuwa tayari na ndio wao walioneckana mbele ya Mheshimiwa Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachosema ni hivi, wasanii Watanzania hawahitaji *mastering studio* bali wanahitaji usalama wa kazi zao zisiibiwe, wanahitaji faida ya kazi zao wanapofanya kazi zao. Kwa hiyo, wasanii hawahitaji *studio* maana zipo nydingi wanaweza wakarekodi popote hata majumbani zipo. Lakini usalama wa kazi zao. COSOTA inafanya nini? Sasa hivi amejitokeza *Msama Promotion* ndiye anayekamata kazi za wasanii, anasaidiwa je sasa? Kazi zingine zipo polisi, tunasema Sheria iletwe hapa, kazi zikipelekwa Mahakamani faini shilingi 200,000/. Yaani hivi kweli Wizara ipo *serious?*

Kwa hiyo, mimi ninaomba sana hasa mikataba hii ya wasanii na hawa wanaojiita mapromota, mameneja sijui washauri na wasambazaji, ni feki yote. Wizara wekeni utaratibu ili muweke wanasheria wa kusimamia mikataba ya wasanii na wasanii waweze kufaidika. Ninaomba sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna jambo lingine ambalo naomba niliongee mapema nalo ni kuhusu Nyumba ya Sanaa. Nyumba ya Sanaa kile kiwanja kilitolewa na Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere kwa wasanii. (*Makofii*)

Mimi mwenyewe nimefanya biasara pale kwa kupeleka kazi zangu za sanaa, kutoka kule Singida kwa akinamama walifuma visonzo, nimekuta Tatanane wapo pale, nimekuta walemavu wapo pale, wale watu walikuwa wanatafuta masoko nje. Lakini sasa hivi nataka kujua, ni nani aliyepeleka kesi Mahakamani ya jengo lile? Jengo lile lilijengwa na Wanorway na Waswedish. Nani mwenye haki ambaye amemilikishwa sasa hivi?

Mimi siungi mkono mpaka niambiwe jengo lile linarudi mikononi mwa Wizara ile ni mali ya Serikali. Wale walikuwa ni Bodi tu. Bodi unaweza ukajimilikisha kitu kikawa ni cha kwako? Sasa hivi sijui tunaambiwa wameingia ubia, unaingia ubia *who are you?* Unaingia ubia na nani?

Ninaomba jengo lile niambiwe kwamba litarudi mikononi mwa Serikali ili wasanii na vijana, walemavu, akinamama wote wakapate faida kwenye lile jengo. Tulikuwa tunatafutiwa masoko mpaka nje ya nchi. Wanawake wote Tanzania walikuwa wanapeleka bidhaa zao pale, vijana wote walikuwa wanakwenda kujifunza kazi za sanaa pale, halafu leo eti watu wanasema tunagawana, tunaingia ubia. *Who are you?* Tumuezi Baba wa Taifa, alitoa kwa nia nzuri na si kwa ajili ya mtu mmoja. Ninataka nipate maelezo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninaomba *TCRA* na *TRA* washirikiane na *COSOTA* kwa ajili ya kuweka nembo kwa ajili ya kudhibiti wizi na ujangili unaofanywa na hawa watu wanaodhulumu na kuiba kazi za wasanii. Watu wanasema eti niseme *COSOTA* ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *COSOTA* ni chama kinachosimamia Hakimiliki na Hatimiliki, lakini naamini wameshindwa kufanya kazi yao, ama kitolewe kule kiletwe kwenye Wizara yako maana naamini unaweza ukakisimamia vizuri. Lakini msimamo wangu bado ninasema utamaduni inyofoeni pale maana imeongezewa tena vijana, habari, michezo kila kitu na hela umepewa ndogo sijui utafanyaje kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, siungi mkono hoja. Ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Naomba niwakumbushe Kanuni 61(2) inayohitaji kama una *interest* na suala lolote *u-declare interest* mapema. Ni muhimu na ukisha-*declare interest* unaendelea na mchango wako.

## TAARIFA

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Tumeelekeza kwanza usimame utulie sehemu yako, nitakuona na usiongee kabla ya ruhusu. Kwa hiyo, naomba tuendelee. Naomba kumwita Mheshimiwa Sabreena Sungura.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Waislam wote wanaofunga mwezi huu Mtukufu. Pili, napenda kuwashukuru Wabunge wote humu ndani kwa ushirikiano waliotupa hasa katika mwezi huu. Hatuna cha kuwalipa ila Mwenyezi Mungu atawalipeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja hii napenda kuanza kuchangia kuhusu Idara ya Habari. Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ina Idara ya Habari ambayo wananchi wamekuwa wakituma hoja mbalimbali kupitia tovuti ya wananchi, kutuma *sms* na hata wakati mwininge kuandika barua na wakipatiwa majibu mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ningependa kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba njia hii imekuwa na changamoto zake hasa hasa kwa upande wa tovuti ya wananchi. Watanzania

wengi hawajawa makini sana katika masuala mazima ya *computer* na *internet*, kwa hiyo, sidhani kama hoja nyingi zinazohusu maslahi ya Taifa zinatumwa kwa ufasaha ama kwa uhakika na kupatiwa majibu. Kwa hiyo, nafikiri hizi njia nyinginezo za barua ama za kuonana ana kwa ana na wenzetu Maafisa Habari, zingeweza kutumika zaidi na nafikiri zinaweza zikasaidia kusogea mbele Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Wanahabari, wamekuwa ni chachu ya maendeleo. Lakini kwa kiasi kidogo wamekuwa na wenyewe ni changamoto katika maendeleo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwa namna ya kipekee kabisa kumpongeza Mwandishi wa Gazeti la Mwanahalisi, Ndugu Saed Kubenea kwa kazi nzuri ambayo amefanya katika Taifa letu. Licha ya vitisho, kumwagiwa tindikali, kutaka kugongwa na gari, lakini amesimama imara na kutetea fani yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nigosie suala zima la utamaduni. Utamaduni katika nchi yetu kwa namna moja ama nyingine unaporomoka. Pamoja na kuvisifia vyombo vyaa habari, lakini na vyenyewe kwa wakati mwingine vimikuwa vinachangia katika uporomokaji wa maadili haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba moja kwa moja sasa nigosie sekta nyeti, sekta ya vijana. Kama tunavyojua, asilimia zaidi ya 60 katika nchi hii ni vijana na ndiyo nguvukazi ya Taifa. Kulikuwa kuna msemo kwamba vijana ni Taifa la kesho, lakini hapana, vijana ni Taifa la leo, lazima wawezeshwe leo hii ili waweze kujenga nchi yao wakati bado wana nguvu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri zetu imekuwa inatengwa takribani asilimia tano ya mapato ili vijana waweze kusaidiwa na kukopeshwa. Lakini ninakotoka mimi Manispaa ya Kigoma Ujiji, hali hii sijaikuta na nilipomuuliza Mkurugenzi, akasema kwamba katika usimamiaji wa kurudisha fedha hizi kumkuwa na utata na usumbufu ndiyo maana tunashindwa kutoa kiwango hiki. Lakini mimi naona ni kuwanyima haki zao za msingi wakazi wa Manispaa ya Kigoma Ujiji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajira kwa vijana, Mkoa wa Kigoma umetengewa takribani hekta 3,000 kwa ajili ya *Special Economic Zone*. Eneo hili linahitaji wawekezaji waende wakajenge viwanda, lakini tuna changamoto kubwa, tunatumia umeme wa jenereta. Hivi ni nani ataenda kuwekeza viwanda katika umeme huo? Kwa hiyo, hii ni changamoto, lakini kama tungepata viwanda vya kutosha, vijana wetu wangepata ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule mjini tunalima, mjini tuna zao la mawese, wenzetu wa Kasulu wana zao la mhogo, Kibondo wana asali na nta, Kigoma Vijiji wana mawese. Vitu hivi vingeweza kusaidia vijana wetu kupata ajira za kutosha na kuchangia uchumi wa Mkoa na Taifa kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, suala la elimu Kanda ya Magharibi, napenda kusikitika pamoja na Tanzania sasa hivi Vyuo Vikuu vinaota kama uyoga, lakini Kanda ya Magharibi hatuna Chuo Kikuu hata kimoja. Kwa hiyo, ningeomba Serikali iweze kutuangalia watu wa Kanda ya Magharibi tuweze kupata chuo ili vijana wetu waweze kusoma na kupata ajira mbalimbali. Ningependekeza kama suala hili litafanyiwa kazi, basi chuo hicho kiwekwe Mkoa wa Kigoma ili wenzetu wa Tabora waje wasome, wenzetu wa Rukwa waje, wenzetu wa Kagera, Burundi, Kongo na Rwanda kwa sababu ni maeneo ya karibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na tatizo la Maafisa Vijana katika Halmashauri zetu. Kwanza, mimi binafsi sijamuona. Nimeenda kwenye vikao vya *RCC*, nimeenda kwenye vikao vya *Full Council*, kwa kweli sijawahi kutambulishwa kwamba huyu ni Afisa Maendeleo ya Vijana. Hii ni changamoto kubwa kwa Serikali. Jamani Serikali mna mipango mizuri, mnaweka sera nzuri, kwa nini hamfuatilii utekelezaji wake? Kwa nini hamhakikishi kwamba huu uteule mnaoutoa, mnaenda kuangalia huko?

Je, hawa watu wapo na wanafanya kazi ya vijana? Hii ni changamoto kwa Serikali. Tunaomba mhakikishe kwamba Maafisa Vijana wanapatikana na ni maeneo mengi tu ya nchi hii hawapo na waliokuwepo wanakaimu. Unakuta Afisa Utamaduni ndiye anakaimu nafasi ya Afisa Vijana. Hili ni tatizo. Ama unamkuta mtu ni mtu mzima anawekwa kwenye Idara ya Vijana. Jamani mtu huyo kweli atajua changamoto za vijana! Serikali hili ilifanyie kazi, Waziri pale uchukue kama changamoto hii, upite katika Halmashauri zako za Wilaya na Manispaa mbalimbali, tunataka Maafisa Vijana wawe vijana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa nigosie suala lingine, suala zima la michezo. Michezo imekuwa na faida kubwa sana katika nchi yetu, katika uchumi wa nchi, katika afya zetu na katika mazingira mengine. Napenda binafsi katika sekta ya michezo niugosie hasa Mkoa wa Kigoma na kama sitauongelea Mkoa wa Kigoma katika maendeleo ya michezo ya nchi hii, nitakuwa sijautendea haki Mkoa huu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kigoma tunafanya vizuri katika sekta ya michezo, lakini hatupati *support* ya kutosha kutoka Serikalini na hata inapofikia hatua tunakua na mashindano mbalimbali kwa mfano, *Taifa Cup* ama *Copa Coca Cola*, Mkoa unakuwa unakosa pesa za kutosha kuweza ku-*support* shughuli hizi za michezo. Mara nyingi tumekuwa tuaambiwa kwamba *RAS* anapata barua kutoka kwa Waziri Mkuu, anaambiwa ashughulikie masuala haya, lakini hali sivo, imekuwa wananchi ndiyo wanachangishwa na Wabunge hapa wakati mwingine tuna-*support* na wadau mbalimbali wa michezo. (*Makof!*)

Kwa hiyo, Serikali isikae pembedi ikaona hili jukumu ni la wananchi peke yake na yenye we isaidie kukuza sekta hii hasa kwa Mkoa wa Kigoma. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kigoma tunaomba tujengewe shule ambazo zitakuwa ni *Sport Academy*. Mfano mzuri Kigoma tumekuwa na wachezaji wazuri wakiwemo akina Sunday Manara, Ismail Mwarabu, Makumbi Juma, Abeid Mziba, Thomas Kipese, Hamza Maneno, Kaseja na hata akina Akilimali Yahaya. Hawa ni wachezaji wazuri katika nchi hii wakitokea Mkoa wa Kigoma. Kwa nini hamtupi vipaumbele? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona juzi juzi kwenye Shindano la *Copa Coca Cola*, timu ya vijana chini ya miaka 17 kutoka Kigoma, michezo yote kumi waliyoshiriki wamekuwa wakitandika watu bao nne, tatu, nne, tatu, michezo yote kumi, hamna aliyevimbisha kifua mbele yao. Na mwishoni wakaja kuwachapa Morogoro hapa. Kwa nini tusichukulie fursa hii kuinua michezo katika Mkoa huu? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika timu hiyo, watoto sita wameachwa wachezee timu ya vijana ya Taifa, wanne wakipelekwa chini ya *Azam FC under seventeen*. Jamani hatuoni kama Mkoa huu umekuwa na changamoto kubwa katika sekta ya michezo? Na huu ni wakati muafaka sasa tuwatengezee *Sport Academy* kwa sababu wamekuwa wanafanya vizuri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine inayotukabili kama Mkoa, Maafisa Michezo hatuna. Katika Halmashauri tulikuwa naye, lakini hapa juzi juzi tumeambiwa kaletwa Dodoma. Kwa hiyo, pamoja na kufanya kwetu vizuri, lakini bado tunahitaji Maafisa Michezo ambao wataweza kuzishauri timu zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini changamoto nyingine imekuwa ni hizi kozi za kuwafundisha wenzetu waamuzi na makocha, zimekuwa zinakuja mara chache sana na hata zikifika, vyeti vinakuwa vinachelewa kutolewa. Kwa mfano, Februari mwaka jana watu walipatiwa mafunzo mbalimbali, lakini mpaka mwaka huu, leo hii naongea, watu hawa hawajapatiwa vyeti, kwa hiyo, hii ni changamoto. Mheshimiwa Waziri, hakikisha mafunzo haya yanapotolewa, basi wananchi hawa wanapatiwa vyeti vyao. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini changamoto ya mwisho inayotukabili kama Mkoa ni Uwanja wa *Lake Tanganyika*. Uwanja ule ni mkubwa, ni mzuri, lakini Serikali mmeusahau. Uwanja umeanza kufifia, hauna *maintenance*. Mheshimiwa Waziri, tunahitaji *maintenance*, na sisi tunahitaji *maintenance* ya ule uwanja ili watoto wetu waweze kuibua vipaji mbalimbali. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, muda wangu mfupi. (*Makof*)

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuongelea hotuba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Naunga mkono hoja kabla sijaanza kuongea. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha hapa leo tukiwa katika hali ya amani na usalama. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii adhimu kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii kwa kazi kubwa anayoifanya kila siku katika kuliendeleza Taifa hili na kuidumisha Wizara hii. Mheshimiwa Waziri, Dkt. Emmanuel Nchimbi namwelewa sana kwa sababu alikuwa Mwenyekiti wangu wa Vijana Taifa, Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi. Na tunamwelewa kwa kazi yake kubwa ambayo alikuwa anaifanya katika kipindi chote. Kwa hiyo, namuamini na anaweza kufanya kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, rafiki yangu Dkt. Fenella Mukangara, anacheka cheka pale, anajua, kwa kazi kubwa ya ushirikiano na Mheshimiwa Dkt. Nchimbi kwa kuiongoza Wizara hii. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia yafuatayo, kwanza kabla sijaingia hapa, niombe Wizara hii ikisaidiana na Bunge iweze kutuletea wale wanaotafsiri lugha kwa walio na ulemau wanaotuangalia kule kwa sababu Bunge linatoka /live/. Wale ambaو wanakuwa hawasikii, hawawezi kujua sisi tunaongea nini, hawawezi kujua Wabunge wao wanaongea nini. Nawahurumia sana, naomba sana iweze kutekelezwa hiyo kwa heshima na taadhima na vilevile katika vyombo vy ya habari vyote, wawemo wale wanaotafsiri lugha zile kwa hao walemau, na wao wanataka kujua maendeleo ya nchi yao, lakini hawawezi kusikia. Naomba sana hilo litekelezwe. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kuhusu waandishi wa habari. Nawapongeza sana waandishi wa habari wa nchi yetu ya Tanzania kwa kazi kubwa, nzuri na ngumu wanayoifanya usiku na mchana katika kutuhabarisha sisi wananchi. Kazi ya habari ni ngumu sana, mimi nilijaribu kuisomea kidogo hii habari, lakini nikaiona ni ngumu sana na ndiyo maana sikumalizia kwa sababu nilliona ni ngumu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hii kazi ni ngumu sana. Hawa waandishi wa habari inapaswa Serikali iwaangalie. Iwaangalie kwa sababu bila ya waandishi wa habari nchi yetu haiwezi kwenda mbele kwa sababu hatuwezi kupata taarifa. Bila taarifa hatuwezi kujua nini kinafanya katika nchi hii. Lakini waandishi wa habari leo, hawa waandishi wa habari wananyimwa haki zao mbalimbali ingawa Serikali inajitahidi kuwasaidia kwa kila hali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ona, mfano kama kwenye maandamano pengine ya kisiasa jinsi ambavyo waandishi wa habari wanavyokuwa mstari wa mbele kutuhabarisha na mambo mbalimbali. Lakini pale huwa wanapata athari nyingi sana na mimi siku moja nilisema hapa Bungeni, kuna mwandishi mmoja wa habari alipigwa na ile *camera* yake ikapasuliwa na sijui kesi ile ilifikia hatua gani mpaka leo sijui inaendeleaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli namuomba sana Mheshimiwa Waziri alione hilo, wawe na vitendea kazi kwani hawa ni vibaya kuwa na magari? Unajua, kama wakienda kutafuta habari, waandishi wa habari wanaenda kwa miguu. Wakopeshwe magari ili waweze kuzifuatilia habari kwa uharaka. Hata kama hawana magari, basi hata *Vespa* waweze kukopeshwa katika Wizara hii, Serikali iwakopeshe, mwenzangu ananiambia hata Bajaj, lakini Bajaj hazifai. Wapatiwe usafiri ili waweze kutekeleza kazi zao kwa haraka kwa sababu ni watu muhimu sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hapa Bungeni, hawa waandishi wa habari wa hapa Bungeni, kuna sehemu yao kule wametengewa. Tulisema hapa, mimi mwenyewe nilliongea hapa kwamba angalau wapatiwe *computer* mbalimbali ziwasaidie. Lakini ukienda kule hamna, wanatumia tu *laptop* zao na vilevile kulikuwa na TV, haipo. Sasa mfano kama mwandishi hayupo

hana Bungeni, yupo kule kwenye ofisi yake, atamwona vipi Faida akiongea hapa Bungeni? Atachukua je habari? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana waandishi wa habari waangaliwe na vilevile waandishi wa habari hasa wa vyombo binafsi wawekewe bima. Kazi hii ni ngumu sana, kuna mambo makubwa yanayowapata waandishi wa habari. Kila siku tunalisema jambo hili, lakini mpaka leo halijatekelezwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunganisha hapo hapo, hivi waandishi wa habari wa Zanzibar wako wapi hapa Bungeni? Hili ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, naomba Serikali na wao waandishi wa habari wa Zanzibar wawe wanakuja katika vipindi vya Bunge hapa ili na wao waweze kuwahabarisha wananchi kule Zanzibar na vilevile waweze kuona jinsi gani Bunge linaendeshwa na wao waweze kufanya, kuandika habari za Bunge lao kwa sababu hili ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naomba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, iwaandae waandishi wake wa habari wawe wanakuja wakati wa Bunge hapa ili na wao kule Zanzibar waweze kuelimika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba kuchangia kuhusu vijana na mikopo. Vijana ni asilimia kubwa katika nchi yetu, hakuna asijejua na vijana ndiyo wapiga kura wakubwa wakiwemo akina baba na akina mama. Vijana kwa kweli wametengewa mfuko wao huu, lakini kuna mfuko mkubwa huu wa JK, lakini huoni vijana wengi ambaeo wanapata mikopo hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana vijana wapatiwe mikopo kwa sababu vijana ni Taifa la leo. Wasipokuwa na kazi hawa vijana watakuwa wanazurura zurura, mwisho watavuta bangi na unga. Itakuwa kazi bure sisi hapa nchini kwetu, itakuwa hapana salama. Naomba sana vijana waangaliwe katika mikopo mbalimbali ili kuweza kuendeshea miradi yao mbalimbali na kujitafutia maisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana na ajira. Hata kama vijana wako wengi sana, lakini huoni kwamba vijana ni wengi sana ambaeo wanafanya kazi katika sekta mbalimbali katika Serikali. Naomba sana vijana wawe wanaajiriwa. Hii Wizara iwe na *database*, ijue hasa vijana wake ni wangapi katika nchi yetu ya Tanzania na wapi hawajaajiriwa. Vijana wengi ni wasomi, lakini hawana ajira. Naomba sana vijana waweze kuajiriwa ili wasije wakapotoka. Vijana wasipokuwa na ajira inakuwa ni tatizo, sisi ndiyo wazazi, tunajua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizi wa kazi za sanaa. Jamani, wasanii ni watu muhimu sana. Msanii ni kioo cha jamii. Tunawahitaji sana wasanii kwa sababu ya kuendeleza mila na desturi zetu katika nchi yetu ya Tanzania. Kuna wasanii mbalimbali, wenye wanasemwa wale wasanii wa zamani wanaoimba taarabu za kizamani, wanaoimba muziki wa kizamani, akina King Kiki. Lakini wapo pia wa Bongo Fleva, tunawapenda na wanatoa elimu kubwa sana. Wasanii wa Bongo Fleva wanatoa fundisho kubwa sana kwa jamii. (*Makofii*)

Lakini wakifanya kazi zao hazionekani, mapato hayaonekani, wanaiba watu wanapeleka nje, wanapeleka sehemu mbalimbali. Sasa hivi kuna ufuatiliaji, lakini sjui, napenda tu kusema sjui kama utafanikiwa! Lakini Mwenyezi Mungu aujalie. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasanii akina Ferouz, Chege, Tundaman, Madee, Diamond, Lady Jay Dee, TID, wote ni wasanii wazuri sana na wengine tunawapenda na nyimbo zao wakati wa kupumzika unafurahi na una elimika. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwapendelee sana wasanii, tuwatunze wasanii, tuwawekee fungu lake na wao wasanii katika Bajeti zetu ili nchi yetu na wasanii wetu hawa waweze kuendelea mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashindano ya *Big Brother Africa*, hapa sasa ndiyo kwenye maneno. Kuna vijana wetu wanashirikishwa kwenye *Big Brother*. Hivi, mimi namuuliza Mheshimiwa Waziri, ukija ujibu, hii *Big Brother Africa* maana yake nini? Yafundisha nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sioni kama inafundisha chochote, kwa anayeangalia ile *Big Brother Africa*, jamani sisi Waafrika tunatumwiwa, tunatumwiwa ili tupotoshe maadili yetu, *Big Brother Africa* rafiki yangu mimi siikubali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana basi watu wetu Watanzania tusiwapeleke kule kwa sababu, kweli sipendi kuongea mengi unajua mimi nikisema tena inakuwa tatizo, lakini nauliza *Big Brother Africa* ina maana gani, inafunza jamii zetu hasa za Afrika? Mmh! (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu michezo, mimi na-*declare interest*, mimi ni Yanga tena Yanga damu kwa sababu ninalipia ada, napenda kuwapongeza sana Wanayanga kwa ushindi tulioupata wa Kombe la Kagame, lakini pia nawaambia Simba Mheshimiwa Sitta samahani, nawaambia Simba na wao wasinyonge roho, mwakani wanaweza wakachukua wao, lakini Yanga Oyeee. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kuipongeza timu hii, ilikuja juzi hapa Bungeni tukaipongeza hapa, lakini vilevile napenda kupongeza pia timu ya mpira ya wanawake ya Taifa, timu ya mpira ya Yanga na timu zingine zinakuwa ziko *high class*, lakini nashangaa kwa nini timu yetu ya Taifa ya mpira wa miguu ya wanawake haipewi msukumo. Hivi sasa wana mechi zao chungu mzima, hawana hela, niliona kwenye *TV* jana wanasema wanaomba wafadhili, wafadhili mpaka lin? Kwa nini Serikali haiwawekei fungu lao hawa wanamichezo? Hawa Yanga na Simba kila siku hawatengewi fungu lao, kila siku *TBL* wanafadhali. Ni vizuri *Tanzania Breweries*, *Vodacom* wanafanya vizuri sana wafadhili wetu hawa lakini haileti moyo mzuri kwa Taifa tunaomba Serikali *iji-commit* kwenye mambo haya kwa sababu michezo ni ajira. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana, ninaomba nichukue fursa hii kutambua uwepo wa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa ndani ya ukumbi huu wa Bunge, Mheshimiwa Dkt. Asha-Rose Migiro. (*Makof*)

Karibu sana mama, karibu sana Tanzania na Bunge hili lote linajivunia kazi njema unayoifanya huko duniani, tunakuombea maisha marefu ya furaha na utendaji uliotukuka katika Umoja wa Mataifa, karibu sana. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba tuendelee Mheshimiwa Stephen Ngonyani maarufu Profesa Maji Marefu na Mheshimiwa Maryam Msabaha ajiandae na Mheshimiwa Hamad Ali Hamad ajiandaye. (*Makof*)

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nimpongeze Waziri Mkuu kwa kuwa makini sana ndani ya Bunge hili, vilevile nataka nimpongeze Waziri wa Michezo na Utamaduni Ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi kuwa amepata Wizara isiyopandishiwa Bajeti kwa miaka mitatu lakini mvumilivu, Mungu akubariki.

Mhehsimiwa Mwenyekiti, kwanza nitoe fani yangu mimi ni mganga, nataka Wabunge wajue kwamba mimi ni mganga na wananchi wajue hivyo mimi ni mganga. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ngonyani, samahani naomba ukae kwanza. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa amefuatana na mume wake Profesa Migiro, tunamkaribisha sana, karibu sana. Pia amefuatana na wasaidizi wake anaitwa Mheshimiwa Tuvako Manongi, pamoja na ujumbe wote ambao mmeffuatana nao tunawakaribisha sana. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge naomba tuendelee. (*Makof*)

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru maana kazi ya uganga hata watu wengine wanashaaulika ndiyo maana yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka niwapongeze waandishi wa habari, mtu anayesema kwamba sijui waandishi wa habari wawe wanaandika mambo kwa kuzingatia mimi nataka waandike. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Naomba u-*declare interest*.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi yangu ni mganga wa kienyeji, mganga wa tiba asilia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewazungumzia sana waandishi wa habari, kwa kweli mimi nasikitika sana kuona kwamba waandishi wa habari wanapendwa wakati wa uchaguzi tu kwa ajili ya kuwaweka watu katika mazingira mazuri ya ushindi, lakini wakishamaliza uchangazi na watu wakishashinda wakianza kuandika mapungufu yao watu wanasema waandishi wa habari hawafai. Mimi nataka waandike tu kwa nini wazuiwe? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu lengo la waandishi wa habari watu wanataka kujua kwamba wananchi au Wabunge wamefanya nini au wapiga kura wamewachagua watu ambao wanafanya nini, sasa kama watakuwa wanaandika mazuri tu bila kuandika mapungufu yetu, sioni kama tunawatendea haki na ukizingatia kwamba hiyo ni kazi kama kazi ya watu wengine. Wao pia wanahitaji waonekane kwamba wanafanya kazi. Kama kuna mapungufu Mwenyezi Mungu tu anawaumba watu wanakuwa na mapungufu wamepinda miguu, ije kuwa waandishi wa habari wasiandike kasoro? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiria sana kwa upande wa waandishi wa habari tuisiwanyanyase, ninachoomba tu Wizara ya Utamaduni na Michezo waangaliwe, ili kama kuna kiwango maalum cha waandishi wa habari wapewe ili wafanye kazi vizuri zaidi kuliko kila saa akimwandika mtu vibaya matokeo yake anatishiwa kwamba atauawa au atamtishia maneno machafu au hata atamtishia kwamba wewe tuone kama uandishi wako wa habari au matokeo yake kuwamwagia tindikali, sasa hii siyo kitendo halali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nataka niongelee kuhusu wasanii, kama kuna watu wanapata matatizo sana ni wasanii, hakuna kitu kizuri ambacho msanii ataitwa, kila mtu anapofanya makosa anaambiwa wewe kazi yako ni msanii, sasa usanii ni kazi, wasilinganishe mabaya ya maji marefu ukaweka kwenye usanii. Sasa hivi kuna mtindo wa watu, mtu anafanya makosa yake na yanajulikana kwamba amefanya utapeli fulani, wanakuambia aah, hao si wasanii tu! Sasa usanii maana yake ni nini? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, usanii ni kazi kama kazi nydingine, wasiwe wanafananisha wasanii na mtu akosee basi msanii aonekane kwamba ndiye yeye ambaye anaharibu, Wabunge wengi hapa wamepitia kwenye usanii, yupo ndugu yangu Mbilinyi, yupo ndugu yangu hapa mwandishi wa habari hapa Nkamia, yupo Mheshimiwa Martha, yupo Mheshimiwa Kamata. Sasa ina maana Mheshimiwa Kamata ni msanii? Ni msanii katika fani yake lakini siyo usanii ule mnaochukua wa kuwafanya watu waonekane watu wasanii ni watu wa duni sana, ni watu wa dhiki sana, kila mfano mbaya upelekwe kwa wasanii, hii siyo halali, wasanii wapewe heshima kama vile watu wengine hata kama tunayopewa sisi Wabunge na wao wapewe heshima hiyo kwa sababu ni kazi ambayo ni sawasawa na kazi nydingine. Nataka waheshimiwe kama wanavyoheshimiwa watu wengine. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la michezo, nasikitika sana kuona kwamba michezo inafanyika mikoani tu lakini Wilayani hakuna michezo. Kitu cha kushangaza zaidi ni kwamba maafisa utamaduni hawapati nyenzo na hawaonekani kama ni watu wa busara mbele ya watu. Wanafanya kazi nzuri lakini kule hawaonekani. Maafisa Utamaduni wanaonekana wakati wa kukimbiza Mwenge peke yake, Mwenge ukikimbizwa Tanzania ndiyo Afisa Utamaduni anaonekana na yeye ana nafasi kwa nini, wakati yeye ndiye anayelea vijana wote Wilayani, yeye ndiye anajua ngoma zote Wilayani, yeye ndiyo anajua waganga wote Wilayani, yeye ndiye anajua kila kitu kinachofanyika katika Wilaya, kwa nini hawa watu hawapewi motisha na wenywewe waonekane kwamba wanafanya kazi vizuri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Maofisa Utamaduni wapewe nyenzo kwa ajili ya mambo ya michezo. Kama kweli tunaitaka Tanzania iendelee katika michezo basi ianzie kule Wilayani na Maafisa Utamaduni uwezo wa kufanya kazi zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la viwanja vya michezo, nimeona tu vinashughulikiwa viwanja vya Dar es Salaam, kwani huko mikoani hakuna viwanja? Hata kama ni viwanja vya Chama cha Mapinduzi kwani wanaofanya michezo hawaji kufanyia michezo kwenye viwanja hivyo, viwanja vya Watanzania, kama ni viwanja vya Tanzania kwa nini vinatengenezwa tu viwanja vya Dar es Salaam kiwanja cha Kirumba hakitengenezwi, kiwanja cha Arusha hakitengenezwi, kiwanja cha Maji Maji hakitengenezwi, kiwanja cha Hassan Mwinyi hakitengenezwi, kiwanja cha Kigoma sasa hivi kimekuwa gofu hakitengenezwi, uwanja wa Mkwakwani hautengenezwi. Leo hii tunataka maendeleo ya michezo ni maendeleo gani kama tuisipotengeneza viwanja, watu wataenda kucheza wapi mpira wakacheze kwenye mizimu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana mambo ya michezo yaangaliwe ili watu waendelee kupenda michezo hasa kwa kutengenezewa viwanja, kisiangaliwe kwamba kiwanja hiki ni cha Chama gani, tunachotaka ni michezo ndani ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nakuja kwenye fani yangu...

**MBUNGE FULANI:** Hapo sasa!

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana kuona kitendo cha waganga wa tiba asilia wanavyodhalilishwa. Waganga wa tiba asilia sasa hivi wanaitika sehemu mbili, wanaitika Wizara ya Afya na wanaitika Wizara ya Habari. Wakiwa Mjini wanaambiwa waende wakachukue vibali Wizara ya Afya, wakiwa vijijini wanaenda kwa Afisa Utamaduni wakachukue vibali. Sasa hawa watu kwa nini wanayumbishwa? (*Makofi*)

Mhehsimiwa Mwenyekiti, hakuna hapa ndani mtu ambaye hamjui mganga wa tiba za asili. Kama siyo kumjua kwa jina basi ni kumjua kwa maandishi, sina maana kwamba watu wote mliopo ndani mnaenda kwa waganga, hapana, la hasha! Lakini wote mnajua kwamba waganga wanafanya kazi gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku za nyuma hapa hakukuwa na hospitali, ninyi wote mlikuwa mnatumia tu. Wakati hospitali hazijajengwa watu walikuwa wanatumia majani, wanachemsha majani wanakunyuwa mtu anapona malaria. Lakini ikifika wakati wa uchaguzi wanakimbiliwa waganga, wakishapita wanawafananisha waganga ni watu matapeli na ni watu wasiokuwa na uwezo, sasa utapeli wa mganga ni nini, wakati wewe mwenyewe una shida zako umeenda kwa mganga amekutengenezea umeshinda, umekuja umepata hiyo nafasi uliyoitaka, akianza kutajwa mganga kila kibaya wanafananisha na waganga wa tiba asilia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tabia hii tafadhali naomba waangalie waganga wa tiba asilia siyo watu lelemama kama wanavyofikiria. Hospitali watu wamefanyiwa operesheni mkasi ukabakia tumboni hawakusemwa, mtu amekwenda kufanyiwa operesheni ya mguu badala yake amefanyiwa operesheni ya kichwa hawakusemwa, lakini mganga wa kienyeji akimpa mtu dawa bahati mbaya ameharibikiwa imekuwa ndiyo wimbo, sasa wapi na wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii si Shinyanga mtu akionekana tu tunaambiwa waganga, kuna uganga na uchawi, mganga siyo mchawi, msifanantishe waganga kwamba ni wachawi, mtu mkiona ana macho mekundu anaambiwa mchawi. Kuna watu wanakaa kwenye mazizi ambapo macho yanakuwa mekundu kwa ajili ya moshi, mtu akionekana mnasema akauwawe mchawi jamani hebu wapeni heshima zao waganga. Huu utamaduni umeaniza kwa waganga. Zipo aina tatu za waganga kuna asilia, kuna elimu dunia, kuna mizimu ambayo watu wanaenda kuombewa wanafanikiwa, sasa kila kitu kibaya kinafananishwa na mganga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara hii iangalie vizuri kama ni waganga wanaenda Wizara ya Afya tuje tunakwenda Wizara ya Afya, kama tunakwenda Wizara ya Utamaduni tuje

tunakwenda Wizara ya Utamaduni kwa sababu kuna vitu vingi ambavyo wanafanyiwa waganga halafu hawaonekani kama wanafanya na hawaonekani kama ni binadamu. Hakuna mganga tapeli. Mganga ni mganga unapomsaidia mtu una mawili, unamsaidia apate nafuu unamsaidia apone au la hasha Mungu hakukubali imani ya mtu ndiyo inayomsaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshangaa sana hata hapa ndani mtu akichangia anasema waganga, waganga isiwe sera ya hapa ndani wote tunafahamu mababu zetu walikuwa waganga, miti hii ndiyo inayosababisha watu mpaka leo wanakunya dawa za hospitali zimetoka kwenye miti. Babu zetu walikuwa wanakula matunda wanapona, walikuwa wanakula miti wanapona, wanakula mizizi wanapona, ndiyo maana ya tiba asili. Lakini kila kibaya kinachotokea mtu anafananisha na uganga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba ndugu zangu mimi ni mganga asilia, nimefanya kazi na waganga wenzangu hata hivi nawashukuru sana walinisaidia sana kwa hali na mali mpaka nimefika hapa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aah, ni lazima tuelezane ukweli kwani nini bwana! (*Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** Hata na Mawaziri umewasaidia. (*Kicheko*)

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Kuna watu wengi wanajua asili hiyo, hata Mwenyekiti mwenzangu wa Kamati ya ufundi anajua yupo pale, sasa mkisema kwamba waganga, siyo vizuri hivyo! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nilikuwa nataka tu kuliweka sawa suala la waganga wa tiba asili wachukuliwe kama madaktari wengine wa nchi nydinge au madaktari wengine mabingwa kama mabingwa wengine kwa sababu kuna sehemu tofauti kama yeye amesomea hospitali na vitabu na sisi tumesomea miti tunaifahamu kama wewe unatakiwa ukafanye operesheni sisi hatufanyi operesheni. Wasanii wapewe heshima zao, waandishi wa habari waache kunyanyaswa, kwa sababu mnapotwanyanyasa waandishi wa habari ina maana mnataka ule ukweli wasiuseme, wasipousema ukweli watausemea wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naungana kabisa na wenzangu walionitangulia kwa sababu wameongea vitu vizuri na ninaomba sana niwaunge mkono wenzangu walichangia mengi sana. Ndugu yangu Nkamia ninakushukuru sana kwa hotuba uliyoitoa leo asubuhi, umetoa hotuba nzuri sana ikizingatiwa kwamba wewe ni mwandishi wa habari lakini hukuyatetea yale maslahi ya waandishi. Waambie wapandishe posho kama wanavyopewa wengine, kwa sababu wakipandishiwa posho hawatakuwa wanafanya kazi kwa kusema kwamba labda nikaombe kwa mtu, na waandishi wa habari inakuwa ni maneno mnasema wanataka rushwa, sasa watafanyaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnawachukua watu mnaenda kuwalipa shilingi 5,000/=, shilingi 5,000/= inamsaidia nini, mtu unamzungusha huko kwenye kampeni zako akirudi hata nyumbani kwake watu wanamkimbia halafu akipewa hela mnasema amepewa rushwa, acheni kuwafikiria mabaya. Waandishi wa habari fanyeni mambo yenu, mkifanya makosa wenzenu watajua tumewashika, fanyeni kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana, naomba kumwita sasa Mheshimiwa Maryam Msabaha na Mheshimiwa Hamad Ali Hamad ajiandae. (*Makofi*)

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili nipaye kuchangia Wizara hii ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu *Subhana Wataallah* na Ramadhani hii kunijalia leo nimesimama hapa na ninawashukuru vijana wote wa Wilaya ya Mjini Magharibi kwa changamoto zao walizonipa wakati nilipokuwa nagombea. (*Makofi*)

Mhehsimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Wizara hii imekuwa ikifanya kazi katika mazingira magumu na ninaipongeza hotuba ya Waziri Kivuli na yale mazuri tulyoyasema pia myachukue na myafanyie kazi. (*Makof*)

Mhehsimiwa Mwenyekiti, Wizara hii imekuwa ikisahaulika sana, Wizara hii imekuwa ni Wizara nyeti lakini imekuwa ikisahaulika, hata wakati maswali ya Wizara hii yanaulizwa yanakuwa yanawekwa nyuma. Ninaomba Wizara hii ipewe kipaumbele, kwa sababu Wizara hii ndio inabeba mambo nyeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana ni Taifa la leo wala siyo Taifa la kesho. Vijana hawa tunawatumia kwa mambo mengi, ukifika kipindi cha uchaguzi tunawatumia vijana, tukifika kwenye mambo fulani fulani tunawatumia vijana, lakini kwa nini vijana wanashaulika? Nasema vijana wakumbukwe na vijana wakumbukwe kwa nafasi mbalimbali za uongozi, za ajira hata kwenye mikopo ya Rais inayotoka, vijana wapewe kipaumbele kwenye mikopo hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wengi hapa Tanzania wamekuwa ni vijana sijui niseme wanasindikiza siku, kwa sababu kuna wachezaji wa mipira, wachezaji hawa sijui wanapofikia umri wa kustaafu wanalipwa wapi kiinua mgongo, nataka Waziri aniambie wanalipwa wapi wachezaji amba wanachezea timu zetu za Taifa wapostaifu au ujira wao wa kustaafu wanalipwa wapi? Naomba muangalie suala hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri huwezi kutaja kama hujataja Zanzibar, Zanzibar ipo ndani ya Jamhuri ya Muungano, naomba mnaposiriki kwenye maonesho au kwenye michezo mbalimbali ya nje ya nchi muwakumbuke vijana wa Zanzibar na wao nafasi zao muwape. Vijana hawa wamekuwa wakilalamika, wana sema wanashaulika sana, lakini najua Zanzibar kuna vijana wazuri sana, wacheza mpira wazuri sana na Zanzibar tuna tamaduni mbalimbali, kuna ngoma za asili za Zanzibar, ngoma ambayo hata Tanzania Bara haipatikani, ngoma hii ipo Pemba, ngoma hii ya mchezo wa ng'ombe ni ngoma ambayo inaingizia Serikali Pato la Taifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba mambo mazuri ya Zanzibar yaliyopo katika Kisiwa cha Pemba na Kisiwa cha Unguja na mambo haya ni adimu kwa Tanzania Bara naomba muuenzi utamaduni wetu kwa kupitia sekta ya Muungano na sisi Wazanzibar pia tunufaikie kwenye sekta hii ya Muungano katika mambo ya utamaduni. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais kama ameamua kusaidia vijana kama studio, hii studio isaidie kwa vijana wote amba wanafanya kazi za miziki, kazi zao za sanaa. Asitoe kwa mtu mmoja au kwa vikundi vichache. Hili litaleta tatizo na litaleta malumbano kwa Rais. Nilikuwa namuumba Rais kama ameamua kusaidia vijana awasaki vijana wote bila kuwabagua. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo linaniuma kama mama na mtoto wa kiiislam leo nitalisemea katika Bunge hili na nilikuwa naomba nipaye nafasi ya kuchangia Wizara hii ndio maana nimeomba na nimeipata nashukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuipata. Mimi kwa kweli kuna mambo yanayonishangaza kwenye TV, kwenye vyombo vya habari. Sasa nasema kwa nini watoto wa kike wamekuwa wakidhalilishwa sana ndani ya TV katika matangazo mbalimbali? Ni kwa nini wanaume wao hawavai nguo za uchi kama wanawake? Utakuta hata kwenye muziki kama ni benki unakuta wale akina baba wamevaa vizuri, vijana wamevaa vizuri. Ukituka kwenye filamu unamkuta mwanaume kavaa vizuri lakini ukimwangalia mwanamke kakaa nusu uchi. Hii sheria ni ya kumlinda tu mwanaume? (*Makof*)

Nataka Bunge lako Tukufu litoe sheria hapa ya wanawake amba wanatembea nusu uchi. Ndio maana siku hizi wanaume hawaoi. Wanaume watawaoa vipi na wanawake wanawaona kila kitu chao kiko nje? Sasa huyu mwanaume atakwenda kuoa vipi na huku kila kitu ameshakiona? Naomba sheria hii ifanyiwe kazi. Naomba watoto wetu wa Kitanzania, vijana kuna mambo yale ya kulegeza suruali ngoja jamani naomba niwaambie. (*Makof/Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Naomba tumsikilize vizuri.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Wale wenzetu kule Marekani ambao wanalegeza suruali walikuwa wafungwa ambao walikuwa wanakosa mikanda ya kufungia suruali, ni kwa nini mlegeze suruali halafu mkiangalia na nguo zenu za ndani ni chafu. Kwa nini msikae katika maadili ya Kitanzania na ukakaa kama mtoto wa Kitanzania? Wewe unataka ukae kama mfungwa wa Marekani aliyekosa mkanda wa kufungia suruali? Hili mimi nalikemea kwa nguvu zote. Kaeni katika maadili ya Kitanzania. (*Makofii/Kicheko*)

Ninaomba dada zangu, watoto wangu na wadogo zangu ambao mna-act filamu mbalimbali muache kutembea uchi ndio maana siku hizi wanawake wamekuwa wengi na hawapati wachumba na hawaolewi, kisa kila kitu mwanaume anakiona ndani ya TV. Wakati mwingine umekuwa unatazama TV uko na watu wa heshima upo na baba yako, upo na watoto wakati mwingine unabadiilisha hata matangazo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matangazo, mtu akitaka biashara yake itoke anatafuta mwanamke mzuri anamdhailishwa kwenye TV. Kwa nini mwanaume naye asiwekwe pale kwenye TV akadhalilishwa? Kila tangazo anawekwa mwanamke, ni kwa nini, naomba hii sheria jamani tuige maadili ya Kitanzania tusiige maadili ya kutoka nje. (*Makofii/Kicheko*)

Naomba kuchangia kuhusu *Big Brother*, nimemuona ndugu yangu pale Faida Bakar kasema lakini kaogopa kusema. *Big Brother* ina maana gani? Kweli *Big brother* unakua unakwenda kushiriki mashindano yale yanakudhalilishwa, nyie wenyewe ni wafuatiliaji wa vyombo vya habari na mengi pia mmeyaona yaliyotokea kwenye *Big Brother* naomba kabisa kwenda kudhalilishwa Watanzania huko anadhalilishwa Mtanzania alivyokuwa mweusi. Sijui mimi nasema wazungu wanapenda ngozi yetu, kama wanapenda hii ngozi basi watuoe, kwa sababu hapa najua kuna mabinti wengi sana wa Kiswahili waolewe na hao wazungu mkaone ngozi ya Kitanzania lakini msidhalilishe kwa kupitia hii *Big Brother*. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *Big Brother* ipigwe marufuku na Waziri utakapokuja kutoa majumuisho yako uniambie hii *Big Brother* imeingizia Pato gani la Taifa? Kuna pato gani tunalopata kwenye *Big Brother* hii. Nataka uje uniambie kama kuna pato tunalopata kwenye *Big Brother*? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye haya mambo ya *Miss Tanzania*, haya mambo ya *Miss yaleta UKIMWI* na *UKIMWI* hauwezi kuisha kwa sababu watoto wetu wanadhalilishwa sana jamani. Kama ninyi ni wazazi roho lazima zitawauma. Hebu nendeni huko kwenye mahotelii makubwa watoto wanakokwenda kuweka makambi ya u-miss kama wewe una tumbo la uchungu la uzazi unaweza kuzaa bila siku zako. Naomba haya masuala yakomeshwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naomba kuchangia kuhusu waandishi wa habari. Waandishi wetu wa habari mimi nawapongeza sana. Lakini waandishi wa habari mna matatizo, humo ndani katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuna wanawake wajasiri wanaongea sana na wana hoja nzito sana na waibua hoja nzito sana. Lakini waandishi wa habari mmekuwa mkipiga picha zote ni wanaume, wengine wamesinzia, wengine yaani sijui. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini picha zile za kusinzia au picha nyingine zile za ajabu za kuonyesha tu akina baba tu, kwa nini msiweke hawa wanawake ambao wanaibua hoja nzito? Au mmetuona sisi wanawake ni mabubu humu ndani hatuwezi kuongea? Lakini najua tunaweza kuongea. Hata kama habari zetu tukiongea basi utakuta habari nzuri inauzwa kwa mtu mwingine. Naomba waandishi wa habari muwe waadilifu katika kazi hii. Najua wanawake wengi hapa ni wasemaji. Sitaki muweke picha za ajabu ajabu kwenye magazeti za akina baba mara wengine wamelala, sitaki. Wekeni picha za akinamama ambao wanazungumza katika Bunge hili. Hiyo nasema hiyo ni *message send* imekwenda hiyo. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu mambo ya utamaduni, mambo ya uasilii kutangaza wewe ni Mtanzania. Hivi leo hii ukitazama jamani kwenye TV huwezi kumfananisha Mmarekani na Mtanzania kwa sababu vijana wetu wanaiga mambo mbalimbali kutoka nchi za wenzetu. Kwa nini msiige mambo mazuri? Kuna mambo mazuri, kuna vitenge vizuri tu mkishona

mnapendeza, kwa nini mnatembea uchi? Sasa tunatangaza nini? Hata kama pale kwenye hizi *bongo flava* wanavyoimba wanaimba pale huwezi kuelewa anaimba Kiswahili, anaimba Kiingereza. Sasa imba kitu kijulikanike kama unaimba Kiswahili tujue unaimba Kiswahili, kama unaimba Kizaramo tukujue unaimba Kizaramo, kama unaimba Kiingereza basi tujue unaimba Kiingereza kuliko kuchanganya lugha ina maana gani? (*Makofi/Kicheko*)

Leo ukienda kwenye mabango yote jamani mimi nasema si Watanzania wote wanajua Kiingereza, mabango mengi utakuta yameandikwa lugha ya Kiingereza, kwani hakuna Taifa lilioendelea kwa kuiga lugha za watu. Kwa nini tusienzi lugha yetu? (*Makofi*)

Mimi nasema tuienzi lugha yetu aliyo tuachia Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wetu wa kwanza, kwa sababu kuna watu wanatoka labda vijiji huko mikoani wanakuja hapa Dar es Salaam wanatafuta shule labda shule anaweza kuipita mara tatu, tatu lakini anakuta bango limeandikwa Kiingereza hajui jamani. Kwa nini tusiwe kama Watanzania, kwani ukifika kwa Mjerumani leo unakuta anaongea Kijerumani na anakuwa na mkalimani, kwa nini ukienda kwenye maduka ya Kikorea kama Kikorea huwezi kuuziwa kitu dukani, kwa nini ukienda Japan unakuta Mjapani anaongea Kijapani kama wewe huna mkalimani huwezi kuuziwa kitu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tutafikisha wapi hili Taifa ambalo tunaliacha vijana ambao tunawaacha tunasema ni Taifa la kesho lakini mimi nasema kijana ni Taifa la leo. Hapo nimetoka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naomba kuchangia kuhusu hawa waporaji wa kazi za watoto wetu. Hawa wasanii wanafanyakazi katika mazingira magumu. Sasa nasema mtu ye yote na naomba Bunge hili lipitishe Sheria atakayekamatwa na kazi ya msanii ambaye hajaitolea jasho basi achukuliwe hatua. Siyo apigwe faini ya 200,000 halafu arudi tena kwenda kuiba sitaki. Hawa watoto nataka waenziwe kwa kazi zao na wapate ajira. Kwa kweli vijana hawa wanakata tamaa. Kukata tamaa kwa vijana wanakwenda kwenye magenge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli siungi mkono hoja hii mpaka vijana hawa wapate ufumbuzi wake. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa michango yako mizuri ya kizalendo. (*Makofi*)

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru kupata nafasi hii ya kuchangia Wizara hii ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. (*Makofi*)

Awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia waislam wote tukamaliza kumi la rehema, namuomba Mwenyezi Mungu atulipe rehema kwa kumaliza siku kumi hizi za awali. Lakini nimuombe Mwenyezi Mungu atuwezesha kuifunga Ramadhan hii kwa salama na amani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo kwa Mwenyezi Mungu naomba nichangie Wizara hii na naomba nianze kwa kusema kwamba michezo ni kazi na michezo ni ajira. Mataifa yote duniani wana michezo wanafaidika na wanakuwa na uwezo wa hata kusaidia mambo mbalimbali katika nchi nyingine kwa sababu ya vipato wanavyopata kwa sababu ya kazi za michezo.

Lakini kwa nchi yetu ya Tanzania michezo inaonekana kama ni burudani ndio maana hakuna wachezaji wa michezo mbalimbali ambao wamestaafu michezo na wanamu maisha yao hivi leo. Inasikitisha kwamba mchezaji siku akitundika jezi anakuwa jina lake nalo limepotea. Vinginevyo labda kwa imani yake aseme kwamba bado nina hamu ya kufundisha michezo fulani fulani katika nchi yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata pale mchezaji anapopata bahati mbaya ndani ya michezo ya kuwakilisha Taifa inasikitisha kwamba hakuna chochote kinachomlinda kwa maslahi ya maisha yake baada ya kupata bahati mbaya ya kuumia kwenye michezo. Naiomba Wizara izingatie

jambo hili la kuhakikisha kwamba kuna bima kwa wachezaji wanapopata bahati mbaya katika michezo hasa pale wanapowakilisha Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaja Tanzania katika nafasi ya michezo maana yake pia unaizungumza Zanzibar lakini pia unaizungumza Tanganyika. Nchi hizi mbili zina vyama vyao vya michezo, kwa Zanzibar kuna ZFA ndio chama kinachosimamia mambo ya michezo Zanzibar. Lakini kwa Tanzania Bara kuna chombo kinaitwa TFF. Lakini Tanzania Bara kutumia neno hili la TFF na wakalipa tafsiri ya Tanzania kwamba ni Chama cha Mpira cha Tanzania hapa mimi nadhani si sahihi. Lakini kwa kuwa imezoleka na ndio wanavyoitumia wenzetu wa Tanzania Bara imepelekea kupoteza haki nydingi za Wazanzibar. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Kuna Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Hatuna Tanganyika.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani naomba iingie kwenye *Hansard* Tanzania Bara. Tanzania inaposhiriki kwenye michezo ya Kimataifa, TFF inatumia jina hili kana kwamba ni mwakilishi wa Tanzania. Lakini hata pale tunapopata misaada ama ruzuku kutoka vyama vya mpira duniani (FIFA) ruzuku hizi au mgao huu unaokuja kwa jina la Tanzania unaishia Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar hatuambulii chochote. Ni miaka mingi sasa FIFA imekuwa ikitoa fedha kwa nchi wanachama na kwa sasa inasadikika kwamba ni dola 500,000 kwa mwaka, fedha hizi pia inasemekana Tanzania tunapata. Lakini Zanzibar sijui kama kuna hata asilimia ndogo inayopatikana kutokana na fedha hizi. Taarifa nillyonayo ni kwamba Zanzibar imefaidika kidogo hivi karibuni kwa fedha ambazo zilitumika kwa kuotesha nyasi katika uwanja wa Gombani Pemba. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kuikandamiza na kuidhalilisha Zanzibar kimichezo. Isingekuwa inastahiki TFF kutumia koti la Jamhuri ya Muungano kama wakala/mhusika kwenye michezo ya Kimataifa. Naomba sana jambo hili lifikie mwisho na tunaposhiriki kwenye michezo ya Kimataifa kama Tanzania basi Zanzibar kwa maana ya ZFA ishirikiane na Tanzania Bara (TFF) ili tuone ni vipi tutakuwa tunaiwakilisha Tanzania kwenye michezo ya Kimataifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la watalaan ndani ya michezo kwa Tanzania tumekuwa na tabia ya Tanzania kuona kwamba wenzetu wa Mataifa ya Ulaya kwamba wana viwango vizuri na utaalam mzuri katika mambo ya michezo, mimi silikatai hilo. Ni kweli kwa sababu wenzetu walianza tangu awali wakiamini kwamba michezo ni kazi. Lakini kama tunaamini hivyo na tunaona kwamba wanaweza kuisaidia Tanzania si vibaya kuwa nao kama makocha wa michezo mbalimbali. Lakini wakati huo huo ingekuwa vema sana tukawachukua wazalendo wetu tukawapeleka katika Mataifa hayo kwenda kupata na wao utalaam na ujuzi wa kuja kuisaidia Tanzania katika mambo haya ya michezo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna wachezaji wa mpira wa miguu ambaa walikuwa na majina hapa Tanzania na baada ya kuona kwamba wameshindwa kuendelea na michezo wameamua kulisaidia Taifa hili kwa fani hii waliyonayo na sasa ni makocha. Tuna makocha ambaa wamesaidia sana Taifa hili.

Lakini tunapomchukua kocha wa kigeni kuja kumweka pale na kocha mzalendo Julio maana ni kumdumaza Julio ama kocha mzalendo katika fani ile ya kufundisha. Tunapomfanya kocha wa kigeni kwamba ye ye ndio awe kocha mkuu maana yake ni kupunguza kiwango cha ufundishaji cha kocha wetu mzalendo. Tatizo linakuja kwamba mgeni yule anapoamua kuondoka kwa namna yoyote tunafika mahali tunakuwa tunajiliza tufanyeje kuziba pengo lilitokuwepo baada ya kuondoka? Hali kadhalika kwa upande wa wachezaji tumekuwa na taratibu za kuchukua wachezaji na sheria inasema kwamba timu inaruhusiwa kuchukua wachezaji si zaidi ya watano, klabu iweze kusajili wachezaji wasiozidi watano wa kigeni, sawa sawa lakini mimi naona ni tatizo, naishauri Serikali kuititia Wizara kwamba kama kuna ulazima basi tuchukue angalau wachezaji wasiozidi watatu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale wanaolewa mpira na hasa wale wachezaji na waliopitia kwenye kucheza mpira unapowachukua wachezaji watano wa kigeni ukawaweka uwanjani, ukaweka kwenye kablu maana yake ni kwamba unawachukua wachezaji wazalendo

watano unawaweka *bench*. Unapowaweka *bench* wazalendo unaua viwango vyao vya mpira. Kwa namna yoyote mchezaji *profession* uliyemchukua unapokosana naye kwa mkatuba vingineyo na mchezaji mzalendo tayari umemdumaza kiuwezo wake maana yake una kazi ya kujiuliza tena kwamba nitawezaje kuziba pengo la *position* hii ambayo alikuwa anacheza mgeni ambaye amekimbia. Utaratibu huu unadumaza viwango vya michezo kwa wachezaji wetu. (*Makofii*)

Lakini kama hilo halitoshi tungekuwa na utaratibu wa kuibua vipaji vya wachezaji tangu watoto wadogo tukaweza kuwaendeleza na wakafikia mahali tukawa tunajua kwamba tukihitaji wachezaji eneo fulani tunaweza tukapata wachezaji wazuri wa kulitetea Taifa hili katika fani hii ya michezo. Naomba nizungumzie suala la Baraza la Michezo la Taifa (BMT) kama jina lake ni chombo cha Taifa.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mbunge. (*Makofii*)

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Nakushukuru.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupata nafasi hii ili na mimi nitoe mchango wangu kutokana na hoja ilio mbele yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze moja kwa moja na vyombo vya habari sijui *declare interest* kuwa nilikuwa mwandishi wa habari lakini bado ni mwandishi wa habari, taaluma huwa haifi. Nianze kidogo kuzungumzia vyombo vya habari kama wenzangu walotangulia wamesema. Vyombo vya habari vimefanya kazi kubwa sana kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu tangu na baada ya Uhuru. Naamini vitaendelea kufanyakazi yake ipasavyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa maoni yangu tu yapo mambo machache sana ambayo kama Taifa tukirekebisha vyombo vyetu vya habari vitafanya kazi yake vizuri sana. Leo Tanzania tuna *Media Council of Tanzania*, tuna *Tanzania Media Fund*, tuna Wizara/Serikali. Nilikuwa najaribu kuangalia naona hawa wa *Tanzania Media Funds* wanatoa ruzuku/misaada kuwasomesha waandishi wa habari kwa kiwango kikubwa. Lakini vilevile wamekuwa wakitoa ruzuku kwa baadhi ya vyombo vya habari vya watu binafsi. Lengo ni kuboresha taaluma yenewe ya waandishi wa habari. Imani yangu na niombe Wizara pamoja na Serikali kama watashirikiana vizuri katи ya *Tanzania Media Funds* na *Media Council of Tanzania* naamini tutafanikiwa na tutafika mahali pazuri zaidi kuboresha taaluma hii ya waandishi wa habari. (*Makofii*)

Kwa mtazamo wangu na hali ninavyoiona niliwahi kushauri siku moja, nashauri tena leo ni vizuri tukawa na Sera ya Habari ndani ya Tanzania. Kwa nini nasema hivi, sasa hivi vyombo vyetu vya habari vinakwenda tu, vingi vinaandika maoni badala ya habari. Nina wasiwasi kwamba kama kuna baadhi ya watu watafariki dunia katika nchi hii baadhi ya vyombo vya habari navyo vitakufa. Vyombo vya habari vinaandika maoni badala ya habari kitu ambacho nadhani tukiwa na Sera ya Habari tutafanikiwa sana. (*Makofii*)

Kwa mfano Rwanda mwaka 1994 leo wapo waandishi wa habari na wahariri watatu walikwenda kwenye Mahakama ya Kimataifa ya Rwanda ya Makosa ya Jinai kwa sababu vyombo hivi vilichangia sana yale matatizo ya mwaka 1994 pale Rwanda. Tukiachia hali hii hapa kwetu kama inavyokwenda uwezekano wa kufika huko ni mkubwa na sisi ni binadamu pia. Nadhani jambo hili lazima tuchukue hatua haraka sana kama Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanazungumzia kuhusu rushwa kwenye *media* inawezekana ikawepo. Lakini sisi ndio tunaoendekeza waandishi wa habari, tunawapa sisi fedha ili watuandike vizuri kutujenga lakini ni hawa hawa watakaotubomoa pia kesho. (*Makofii*)

Katika nchi zilizoendelea, mimi bahati nzuri nimefanyakazi kwenye *media*, *giants* zote duniani, wakati wa vita vya Iraq nilikuwa nafanya kazi BBC pale ilipokuja vita ya Iraq vyombo vyote vya habari vya Uingereza vilikuwa vinai-support nchi yao kwamba tunakwenda kupigana kwa ajili ya Taifa la Uingereza tofauti na kwetu sasa hali ilivyo. Waziri Mkuu siku anahitimisha Bajeti yake hapa lilikuwa ni jambo zito sana, lakini vyombo vya habari hasa magazeti, kichwa cha habari

na yakizungumza habari ya *interest* ya Taifa, walikuwa wanazungumza habari za watu wachache. Hili lazima tuliangalie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka huko nije kidogo kwenye Baraza la Michezo la Taifa (BMT) sheria za michezo zinabadilika siku hata siku. Huwezi kuwa na watalaan wa mwaka 1962 leo ukategemea wata-produce kitu kizuri kwa maendeleo ya Taifa hili katika michezo. Hatuna fungu la kutosha lillotengwa kwa ajili ya kuwasomesha watalaan wetu, Baraza la Michezo lillishamaliza muda wake kutoka mwaka 2009, jengo lao walilonalo pale linavuja, mvua ikiwa inanyesha wanakimbia kwa sababu zile nyaya za umeme pale zinaleta matatizo. (*Makofi*)

Mimi nilikuwa nashauri tuna uwanja mzuri sana pale uwanja wa Taifa, tuna vyumba zaidi ya mia moja na kitu kwa nini BMT wasihamishiwe pale wakatumia zile ofisi pale *TFF*. Amesema Mheshimiwa Hamad kwamba *TFF* wanapata fedha kutoka *FIFA*, ni ruzuku ambayo kesho na kesho kubwa inaweza ikafa. Lakini fedha hizi haziendi katika mikoa ipasavyo. Kwa mujibu wa kumbukumbu zangu vyama vya mikoa vimepewa shilingi milioni mbili tu na kompyuta tangu fedha hizi zianze kutolewa na *Tanzania Football Federation*. Viongozi wa vyama vya michezo vya mikoa kazi yao ni kwenda kupiga kura kumchagua Rais wa *TFF*. Hatuwezi kuendeleza michezo namna hiyo. Ile fedha ishuke huku kwenye *grassroots* ili tuweze kuwatengeneza vijana katika mikoa tuwe na timu nzuri za Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, timu ya Taifa ya Tanzania zamani Serikali illikuwa inatoa ruzuku timu inapokwenda kwenye mashindano ya Kimataifa, siku hizi haipo. Nchi nyingine zote zilizopiga hatua maendeleo ya michezo katika timu zao za Taifa kuna fedha zinatengwa kwa ajili ya maandalizi ya timu za Taifa. Ningombaa sana Serikali ione hili, michezo ni ajira na sisi tunavyofahamu kwamba michezo umuhimu wake leo kila Mbunge, Bunge likivunjwa ataondoka na mipira kwenda jimboni kwake hapa kwa ajili ya vijana wanaompigia kura kule. Ningombaa Serikali itazame jambo hili iweze kusaidia ili timu zetu za Taifa zifanye vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watalaan wanaokuja kutoka nje, ikiwa tuna watalaan wapo pale watu kutoka Cuba, tuna Paulsen wa timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu tuna wengine. Kuna mwingine anaitwa Paulsen wa vijana tungewa-task hawa na *TFF* wakisaidiana na Wizara kwamba wanasaidia kuafundisha makocha wetu wa ndani walau kozi fupi fupi ili wanapoondoka *at least* tuwe na makocha kadhaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza napenda niwashukuru wote kwa ushirikiano wenu kwa michango mizuri mliyoonyesha kwa ajili ya nchi yetu. Kabla sijaahirisha shughuli naomba niwataje ambaa kesho baada ya Maswali na Majibu watachangia. Tutaanza na Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Moza Saidy pia Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kahigi na wengine watatajwa na watakaokuwa mezani kesho.

Naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi. (*Makofi*)

(Saa 12.29 jioni Bunge lillahirishwa hadi siku ya Ijumaa, Tarehe 12 Agosti, 2011 saa tatu asubuhi)